**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Kamal Basha Pandu | Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo. |
| 2.Mhe. Ali Mzee Ali | Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais. |
| 3. Thuwaybah Edington Kissasi | Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake. |
| 4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe. |
| 5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge. |
| 6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni. |
| 7.Mhe. Haji Omar Kheri | Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu. |
| 8.Mhe. Haji Faki Shaali | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni. |
| 9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani. |
| 19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais. |

| | |
|---|---|
| 11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe. |
| 12.Mhe. Hamza Hassan Juma | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura. |
| 13. Mhe. Machano Othman Said | Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni. |
| 14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki | MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais. |
| 15.Mhe. Samia Suluhu Hassan | MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake. |
| 16.Mhe. Burhan Saadat Haji | MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni. |
| 17.Mhe. Asha Abdalla Juma | MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais. |
| 18.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi. |
| 19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry | MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais. |
| 20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki. |
| 21.Mhe. Zainab Omar Moh'd | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake. |
| 22.Mhe. Idi Pandu Hassan | Mwanasheria Mkuu wa Serikali. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae. |
| 24. Mhe. Mzee Ali Ussi | Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani. |
| 25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari | Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu. |
| 26.Mhe. Khamis Jabir Makame | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni. |
| 27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole. |
| 28.Mhe. Tafana Kassim Mzee | Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini. |
| 29.Mhe. Zahra Ali Hamad | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake. |
| 30.Mhe. Zakiya Omar Juma | "Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake. |
| 31.Mhe. Said Ali Mbarouk | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando. |
| 32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga. |
| 33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake. |

| | |
|---|---|
| 34.Mhe. Hamad Masoud Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole. |
| 35.Mhe. Omar Ali Shehe | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake. |
| 36.Mhe. Rashid Seif Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani. |
| 37.Mhe. Mohamed Ali Salim | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani. |
| 38.Mhe. Asaa Othman Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete. |
| 39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake. |
| 40.Mhe. Najma Khalfan Juma | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake. |
| 41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile. |
| 42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. |
| 43. Mhe. Abass Juma Muhunzi | Jimbo la Chambani. |
| 44.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini. |
| 45.Mhe. Ali Denge Makame | Jimbo la Amani. |
| 46.Mhe. Ali Haji Ali | Jimbo la Mkwajuni. |

| | |
|---|---|
| 47.Mhe. Ali Moh'd Bakari | Jimbo la Tumbe. |
| 48.Mhe. Ali Suleiman Ali | Jimbo la Kwahani. |
| 49.Mhe. Ame Mati Wadi | Jimbo la Matemwe. |
| 50.Mhe. Ame Ussi Juma | Jimbo la Nungwi. |
| 51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake. |
| 52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila | Jimbo la Fuoni. |
| 53. Mhe. Asha Moh'd Hilal | Jimbo la Magogoni. |
| 54.Mhe. Ashura Abeid Faraji | Nafasi za Wanawake. |
| 55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Nafasi za Wanawake. |
| 56.Mhe. Dadi Faki Dadi | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba. |
| 57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim | Nafasi za Wanawake. |
| 58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | Jimbo la Mji Mkongwe. |
| 59.Mhe. Haji Mkema Haji | Jimbo la Koani. |
| 60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji | Uteuzi wa Rais. |
| 61.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani. |
| 62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba. |
| 63. Mhe. Juma Duni Haji | Uteuzi wa Rais |
| 64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope. |
| 65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma | Nafasi za Wanawake. |
| 66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga | Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja. |
| 68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake. |
| 69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | Uteuzi wa Rais |
| 70.Mhe. Omar Ali Jadi | Jimbo la Kojani. |
| 71.Mhe. Pembe Juma Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja. |
| 72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu | Jimbo la Muyuni. |
| 73.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake. |
| 74.Mhe. Said Khelef Ali | Jimbo la Bumbwini. |
| 75.Mhe. Salim Abdulla Hamad | Jimbo la Mtambwe. |
| 76.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni. |
| 77.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni. |
| 78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde. |

| | |
|---|---|
| **Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi.** |

**Kikao cha Tatu – Tarehe 15 Juni, 2010**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 48**

**Kero za Muungano**

**Mhe. Ali Abdalla Ali –** Aliuliza:-

Pamoja na faida nyingi zinazopatikana katika Muungano wa Zanzibar na Tanganyika lakini bado Muungano huo unakabiliwa na changamoto nyingi zinazotokana na kasoro kadhaa zilizopo katika masuala mbali mbali ambazo kwa njia moja au nyengine zinatia dosari katika Muungano wetu na kuathiri. Tume ya pamoja ya kushughulikia kero hizo inayohusisha pande zote mbili za Muungano imeundwa, lakini bado Tume hiyo haijazimaliza kero hizo.

(a) Je, Mhe. Waziri tangu kuundwa kwake Tume hiyo imeshughulikia kero zipi na imefanikiwa kutatua kero ngapi kati ya hizo.

(b) Kwa kuwa kero hizo ni nyingi. Je, kuna mkakati gani wa kuzishughulikia ili kuzipunguza.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi) -** Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 48 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Ni kweli usiofichika kwamba Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar uliofanywa na Waasisi wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume na Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1964 una faida nyingi. Kutokana na upevu wa Muungano huu, tunakiri kusema kuwa Muungano huu unakabiliwa na changamoto. Ili kukabiliana na changamoto hizi na zijazo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete katika

kikao chake cha Semina Elekezi huko Ngurdoto Arusha aliamua kwa makusudi kuanzisha Kamati maalum ya kujadili kero za Muungano inayohusisha pande zote mbili za Muungano.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa majibu kama hivi ifuatavyo:-

(a) Kamati hii mpaka hivi sasa inashughulikia masuala tisa (9) kama ifuatavyo:-

1. Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.
2. Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia.
3. Ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za Nje.
4. Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano.
5. (i) Mgawanyo wa Mapato yatokanayo na:-

    (a) Misaada kutoka Nje ya Nchi;
    (b) Misamaha ya Mikopo ya Fedha kutoka *IMF*; na
    (c) Faida ya Benki Kuu.

   (ii) Uwezo wa SMZ kukopa ndani na Nje ya Nchi; na
   (iv) Hisa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki.

6. Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili.
7. Utekelezaji wa sheria ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora Zanzibar.
8. Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu.
9. Utekelezaji wa *Merchant Shipping Act* katika Jamhuri ya Muungano na uwezo wa Zanzibar kujiunga na *IMO*.

Aidha, Kamati hii imefanikiwa kukamilisha kero zifuatazo ambazo mbili zimeshatayarishiwa hati za makubaliano na kuwekwa saini na Mawaziri husika wa SMZ na SMT. Kero zenyewe ni :-

1. Utekelezaji wa Sheria ya Haki za Binaadamu Zanzibar.
2. Utekelezaji wa *Merchant Shipping Act* katika Jamuhuri ya Muungano na uwezo wa Zanzibar kujiunga na *IMO*.
3. Mgawanyo wa Mapato:-

(i) Misamaha ya Kodi ya Fedha kutoka *IMF*;
(ii) SMZ imeshapata fedha za misamaha ya madeni;

(iii) Uwezo wa SMZ kukopa nje ya nchi, tayari SMZ inakopa kupitia *BOT* na Wizara ya Fedha na Uchumi SMT na SMZ zimetakiwa kuandaa utaratibu mzuri utakaoondoa urasimu katika SMZ kupata mikopo hiyo; na

(iv) SMZ tayari imeshaanza kunufaika na mikopo ya misaada ya Kibajeti (4.5%) kuanzia mwaka 2009/2010.

(b) Mhe. Spika, kwa kero zilizobakia kutatuliwa Kamati ya Pamoja ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi zinaendelea kuzitafutia ufumbuzi. Pia sekta na Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa pamoja wana utaratibu wa kukutana katika Vikao vya Mashirikiano katika mkakati wa kuzipatia ufumbuzi kero zilizopo kati yao.

Vile vile kamati ndogo ndogo za wataalam zimeundwa baina ya SMZ na SMT ili kushughulikia baadhi ya hoja na kutoa ushauri utakaopelekea ufumbuzi wa kero hizo kupatikana.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Muungano wa Tanzania umekuwa ni Muungano wa historia katika Bara la Afrika, lakini pia niseme hata katika nchi za nje. Tunaamini katika uhai ambao upo mpaka sasa hivi ni tegemeo kwamba kama kulikuwa na makero yoyote yawe yameondoka au yabakie machache kuliko ilivyoelekezwa katika makero tisa yakapatikana ufumbuzi mawili.

Je, kwa kuwa hivi sasa dunia ni utandawazi na kila nchi inategemea kupata maslahi yake kwa njia zake zinazokubalika. Katika jibu Mhe. Waziri ametwambia kwamba katika kero mojawapo, mengi tu lakini moja suala la mafuta na gesi asilia ambalo hili bado limo katika mchakato. Hivyo, haoni Mhe. Waziri kulichelewesha hili na kwa kuwa Wazanzibari wengi au wote wanalitaka liachiwe Zanzibar yenyewe ili ifaidike. Haoni kunarudisha nyuma juhudi hizo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi):** Mhe. Spika, kama tulivyosikia katika hotuba ya Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi ni kwamba kero zilizokwishakupatiwa ufumbuzi mpaka sasa hivi ni sita na zimebakia tatu. Zilizotiwa saini kukamilisha moja kwa moja kwamba tumeshakaa sawa sawa ni mbili. Kwa hivyo, zilizopatiwa ufumbuzi sio mbili kama alivyoeleza Mhe. Mjumbe.

Mhe. Spika, suala la mafuta na gesi tumelizungumza hapa katika Baraza la Wawakilishi na limekwenda katika vyombo mbali mbali vinavyohusika na utekelezaji wake. Nataka nimkumbushe kwamba hata Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Sherehe za Mapinduzi Pemba alisema kwamba suala hili sasa hivi kazi inayotakiwa kufanywa ni kuliondoa katika masuala ya Muungano. Kwa hivyo, kinachohitajika sasa ni marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Mhe. Spika, nakushukuru asubuhi hii na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa roho ya serikali yoyote au dhima ya serikali ni mapato. Kwa kuwa suala muhimu ambalo linaikosesha serikali yetu mapato inahusiana na suala zima ambalo limo ndani ya Katiba la kuanzishwa kwa chombo kinachoitwa *Joint Finance Commission* ambayo ndio itakayotatua jinsi gani mapato ya Muungano yachangiwe na vipi yagaiwe kwa nchi hizi mbili.

Lakini hadi tunasomewa bajeti juzi tumearifiwa kwamba wenzetu hawajawa tayari katika suala hilo kulizungumza. Je, Mhe. Waziri sisi kama serikali ndio tutakalia hapo hapo kwamba wenzetu hawajawa tayari au mkakati gani upo wa kuona kwamba suala hili linamalizwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Aisi ya Waziri Kiongozi):** Mhe. Spika, suala la *Joint Finance Commission* sisi tumeshaipitisha kwenye Baraza la Mapinduzi na mawazo yetu tumeshatoa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kwa bahati nzuri, Zanzibar ina bahati ya kuwa na Wabunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, Baraza la Wawakilishi Zanzibar lina bahati ya kuwa na Wabunge hao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. Sasa tunawaomba watuwakilishe vizuri kudai kwamba na kule likamilike. *(Makofi)*

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Katiba ya Zanzibar kifungu cha 18 katika uhuru wa maoni naomba kunukuu:

Kifungu cha 18:

> "Kila raia ana haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matokeo mbali mbali nchini duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii".

Mhe. Spika, haya masuala ya kero za Muungano ni muhimu sana katika jamii. Vyombo ambavyo vinatoa taarifa ama Baraza la Wawakilishi au Serikali yenyewe na kwa bahati nzuri katika makero tisa sita yamepatiwa ufumbuzi.

Hivyo, Mhe. Waziri alitoa taarifa kwa chombo gani ili kuijulisha jamii kwamba makero yanashughulikiwa na sita tayari yamepata maamuzi.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Aisi ya Waziri Kiongozi):** Mhe. Spika, jambo lolote linaloshughulikiwa na serikali likikamilika hutolewa taarifa. Kwa bahati nzuri yale yaliyokamilika Mhe. Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi ameshatoa taarifa na wajumbe hivi sasa wanachangia katika shughuli ile. Ni vizuri tu waongeze michango yao lakini taarifa ndio imeshatoka ndani ya Baraza la Wawakilishi na imetolewa na Mhe. Waziri wa Fedha.

**Nam. 70**

**Ndoa za Mkeka**

**Mhe. Hija Hassan Hija -** Aliuliza**:-**

Katika uislamu sharti moja la kukubalika kwa ndoa ni kuwepo Ijabu na Kabuli. Lakini wakati mwingine hutokea mazingira ya kufanyika na kufungwa kwa ndoa kwa haraka mno bila ya mashauriano (ndoa za mkeka).

(a) Je, Mhe. Waziri, ndoa kama hizo zinafaa kwa misingi ya Kiislamu?

(b) Utafiti unaonesha kuwa ndoa kama hizo mara nyingi hazidumu na hata watoto wanaopatikana, basi hutelekezwa na wazazi wao hasa wa kiume. Je, nini tamko la Serikali kwa suala hilo?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora -** Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 70 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, suala hili ni la kiusomi kidogo na ni vizuri Mhe. Hija Hassan Hija ameliuliza na ametumia *terminology* zile zile za kiusomi, ametumia ijabu na ametumia neno kabuli. Hizo ni nguzo katika ndoa na bila ya hizo ndoa haisihi. Ijabu ni lile tamko la kwanza linalotamkwa na muozeshaji “Nakuozesha fulani binti fulani”. Kabuli ni lile tamko la pili linalotolewa na anayeoa anaposema “Nimekubali”. Hukaririwa kwa kusema “Nimekuozesha” na wa pili akajibu “Nimemuoa”. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, naendelea kujibu swali. Mhe. Spika, tunakiri kuwepo kwa ndoa zinazofungwa kwa haraka (ndoa za kukamatiwa). Ndoa kama hizi hazipendezi kwa kuzingatia heshima ya ndoa na pia mafundisho ya Mtume Muhammad

(SAW) aliyetaka Waislamu kuzitangaza ndoa zao na sio ndoa kufungwa kimya kimya. Ndoa inahitaji maandalizi na kufanyika kwa shamra shamra za kihalali, mambo ambayo hukosekana katika ndoa za haraka au ndoa za kukamatiwa. Lakini pamoja na ndoa hizo kutopendeza, bado zitakuwa ni sahihi iwapo nguzo za ndoa zitakamilika. Nguzo hiyo ni pamoja na kuwepo kwa Walii, Mashahidi wawili, Mke na Mume, kuwepo na kauli za pande mbili kwa walii kuozesha na mume kukubali kuoa. Iwapo nguzo hizo zitakamilika basi ndoa itakuwa ni sahihi japo kuwa itafungwa Kituo cha Polisi au kwa Sheha.

Mhe. Spika, juu ya suala la tamko la serikali juu ya ndoa hizi na wito unaotolewa kwa jamii kuzingatia maadili yetu na kuongeza juhudi katika kuwafunza vijana wetu tabia njema na umuhimu wa vijana na jinsia zote kutojihusisha na mapenzi katika umri mdogo. Jamii inapaswa kuelewa kwamba ndoa zinazofungwa bila ya maandalizi kama hizi mara nyingi huwa hazidumu kwa sababu ya kukosa misingi madhubuti. Hii ni kazi yetu, *"Kullukum rai wa kullukum mas'ulan raiyyati".*

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba ndoa husihi kwa kupatikana ijabu na kabuli. Kwa kuwa tumeshuhudia baadhi ya vijana wanapopata mtihani huo wa kukamatiwa wazee wao hugoma kuwaozesha watoto wao na hupelekea sasa ndoa kufungwa Polisi, kwa Sheha au kwa Kadhi. Je, ikitokezea kesi kama hii hiyo ijabu na kabuli itakuwepo?

Swali (b) katika uislamu mahari ni haki ya mke anayeolewa. Ikitokezea kesi hii fedha za wengine hutolewa kwa Sheha, Polisi au kwa Kadhi. Je, mahari haya huwafikia wale wake walioolewa?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa kuwa nimejibu katika swali la msingi kwamba mambo mawili haya lazima yapatikane. Mimi nadhani huko polisi inapofika kesi huwa kapelekwa huyu na kapelekwa na wazee wake. Huko kwa sheha inapofika kesi huwa kapelekwa na kapelekwa na wazee wake. Sasa katika hali hiyo mambo haya hukamilika pale, yakikamilika pale basi ndoa hiyo imesihi. Kama hayakukamilika pale hapo ndoa ndio haikufanyika.

Inatokea hali wakati mwengine kuozesha Kadhi lakini ziko sababu zake za msingi ambazo ni madhubuti na zimepangwa katika sheria, zikitimia ndio Kadhi huchukua uwezo wa kumuozesha. Sasa kwa hizi za kukamatiwa kamatiwa mara nyingi wazee wanakuwepo isipokuwa pengine hasa anayekataa kuoa huwa mara nyingi huyu anayeoa, lakini atakataa vipi wakati mtu anampenda.

**Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kuna ndoa zinazofungwa Mahakama ya Kadhi na ndoa hizi huwa mzazi haziridhii. Baada ya kufungwa ndoa hizi mzazi humsusa mtoto wake na kinachotokea ni kumkataa yule mtoto wake. Je, suala hili serikali inalijua, kama inalijua watoto hao wenye hali ngumu kama hii serikali inawasaidia nini?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, katika swali la kwanza la nyongeza nililojibu nimesema kwamba zipo sababu ambazo Kadhi huchukua uwezo wa kumuozesha mtoto. Hata kama wale wazee wanakuwa wanakataa lakini huwa hawana sababu ya msingi ya kukataa. Kuna sababu zake maalum ambazo hizo ziwepo, akizitaja yule mzee sababu hizo hapo tena Kadhi huwa sababu ya kuingilia. Lakini kwa kuwa sitaki tu kwa sababu tunagombana na mzee wake, tuna kisa chetu huko zamani tulikotoka, basi Kadhi huchukua nguvu pale.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe alitaka kujua serikali inasaidia nini kwa watoto wanaotelekezwa namna hii.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kinachotaka kufanywa hapa ni usuluhishi baina ya hawa watu wawili waliokosana. Usuluhishi huwa unafuatana na maelezo mbali mbali na kulainisha kwa kutumia baadhi ya hadithi zilizotokea huko tunakotoka katika dini na mambo mengineyo mpaka wanafika pahala wanakubaliana na suluhu inapatikana. Tuwaombee kwa Mwenyezi Mungu watu kama hao wapatane kabla ya mmoja kufariki, maana akifariki mmoja hawasikilizani inakuwa mbaya sana.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, siku za hivi karibuni kumetokea kesi nyingi za aina hii za watoto kwenda kushtaki Mahakamani kutokana na malalamiko ya kwamba wazee au mawalii wao hawataki kuwaozesha watoto. Mara nyingi hutokezea kwamba Makadhi wanachukua hatua ya kuwaozesha bila ya idhini ya walii wake.

(a) Je, ni sababu zipi za msingi ambazo Kadhi analazimika kumuozesha yule mtoto na sababu zipi ambazo zinasababisha Kadhi asimuozeshe yule mtoto?
(b) Nini maana ya idhini ya walii katika ndoa ya uislamu?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, wajumbe wako leo wameniweka kwenye darsa. Mhe. Spika, nasema sitaweza kujibu moja kwa moja hapa juu ya sababu za msingi zinazomfanya Kadhi achukue

jukumu la kumuozesha yule mtoto lakini zipo. Tusomeni, twendeni kwenye madarsa, tujifunzeni.

Mhe. Spika, binadamu tumeambiwa tusiwe katika kundi la nne, tuwe katika moja ya makundi matatu. Tuwe wasomaji, wasomeshaji au wasikilizaji, tusiwe katika kundi la nne ambao hawako katika yote hayo. Kuna *aliman, aumu taaliman, aumu stamiaa. (Makofi)*

Sasa ni vizuri tusomeni, kujibu hivi haraka haraka hapa haiwezekani, lakini zipo sababu za msingi zinazomfanya Kadhi achukue jukumu la kumuozesha mtoto yule. Sasa tutakuwa tunawalaumu sana Makadhi wanapozitumia hizo sababu za msingi. Mhe. Spika, jukumu la walii ni kwamba wakati walii anapokuwa anakwenda kinyume na sheria za kiislamu katika kukataa kumuozesha mtoto walii anakuwa Kadhi. *(Makofi)*

**Nam. 23**

**Vikosi vya SMZ**

**Mhe. Said Khelef Ali (Kny: Mhe. Haji Mkema Haji) -** Aliuliza**:-**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeanzisha vikosi vya KMKM, Valantia, JKU, Zimamoto na Mafunzo kwa maelekezo ya Katiba ya Zanzibar.

(a) Mhe. Waziri, Idara na Taasisi zetu za Serikali zinapohitaji huduma ya ulinzi kutoka vikosi vyetu hutakiwa kulipa. Je, bajeti ya vikosi haitoshi kuhudumia vikosi hivyo;

(b) Kwa nini vikosi vyetu visitoe huduma ya ulinzi bure kwa taasisi za serikali kama ni sehemu ya wajibu wao wa kazi; na

(c) Mhe. Waziri, huoni kwamba vikosi hivyo vingeweza kuiokoa Serikali na hasara ya mali na vifaa ambavyo huibiwa ovyo kwa kukosa ulinzi wa uhakika wakati vikosi vyetu tunavyo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ -** Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Mwakilishi kuwa vikosi vyote vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) vimeanzishwa kwa mujibu wa Katiba. Kimsingi kila kikosi kimepangiwa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.

Miongoni mwa majukumu ya msingi ya vikosi vyetu ni kutoa huduma ya ulinzi kwa raia na mali zao pamoja na shughuli za uzalishaji mali.

Mhe. Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Vikosi, Taasisi za Serikali zinazopatiwa huduma ya ulinzi hazilipi kama taasisi nyengine za watu binafsi lakini hutakiwa kuchangia huduma za shughuli hiyo hasa gharama za usafiri.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa kuwa vikosi vyake kazi yake kubwa na wajibu wao kulinda taasisi za serikali na nyenginezo. Mhe. Spika, katika jibu lake Mhe. Waziri ametwambia taasisi za serikali huwa hazitakiwi kulipa ni sahihi, lakini kwa watu binafsi hulazimika kulipa. Je, haya malipo yanaingia katika mfuko gani wa serikali.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Spika, kutokana na taasisi hizi ulinzi hufanywa kwa utaratibu maalum na sehemu kubwa ya ulinzi unaofanywa na vikosi vyetu gharama hizi hutokana na taasisi zisizokuwa za kiserikali. Kwa hivyo, kutokana na ufinyu wa fedha za kuhudumia walinzi wetu, kuhudumia katika taasisi zetu, basi fedha hizi zote karibu asilimia 90 au zaidi huwa zinatoka kutokana na taasisi za nje ya serikali.

Kwa hivyo, vikosi vyetu vinapotoa huduma ya ulinzi bure kwa taasisi za serikali huwa taasisi zile huchangia angalau mafuta au vitu vidogo vidogo ili kuwezesha vikosi hivi kufanya kazi yao ya ulinzi kwa taasisi hizo.

Vikosi vyetu pia vinatoa huduma kwa taasisi za serikali na wizara mbali mbali. Lakini utoaji huduma huo huwa unachangia lakini ni sehemu ndogo sana kama nilivyokwisha kusema hapo mwanzo.

Kwa hivyo, kwa wale taasisi mbali mbali ambazo zipo tunawahimiza kwamba wanapochangia wachangie kwa kiwango kikubwa kidogo kuliko hivi ambavyo wanavyochangia.

**Mhe. Spika:** Mjumbe alikuwa anahitaji fedha inayochangiwa hii inaingia mfuko gani?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Spika, mfuko huo ambao unaotoa huduma kwa taasisi zisizokuwa za serikali ndizo huingia huko.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika kulinda huku

vijana wetu wanapata ajali mbali mbali wengine hufariki na wengine huwa walemavu. Je, serikali inamsaidia vipi mtu kama huyo aliyekwishafariki kifamilia na huyu aliyepata ulemavu.

Swali (b) katika ulinzi huo baadhi ya vijana wasiokuwa waaminifu huwa wanadokoa hapo hapo wanapolinda. Je, kama hawa wakibainika wanachukuliwa hatua gani za kisheria.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Spika, unapofanya biashara yoyote utegemee kupata na kukosa, unaweza ukapata faida au ukapata hasara. Unapopata hasara inataka utumie ubongo wako kurudisha zile ulizopata hasara. Kwa hivyo, wapo ambao waliokwenda katika malindo wanapata vilema vya maisha, wapo wengine wanakwenda kulinda lakini vifaa vyao huwa vinachukuliwa au vinaibiwa. Hiyo ni moja kati ya biashara, kama hutaki itokezee hivyo basi itabidi uihame kabisa hiyo biashara usiifanye.

**Nam. 18**

**Uvamizi wa Shamba la Makurunge**

**Mhe. Hija Hassan Hija -** Aliuliza**:-**

Kumekuwa na kilio kwa wananchi wa Zanzibar kwamba nchi inapoteza samani *(assets)* nyingi na muhimu kama vile magari, mashamba na majumba. Kilio cha karibu ni kuhusu upotevu wa sehemu ya shamba la Makurunge lilioko Bagamoyo Tanzania Bara linalodaiwa kuvamiwa na wananchi kwa shughuli za makaazi na kilimo. Inawezekana uvamizi huo unatokana na SMZ kutokuwa na hati miliki ya eneo la shamba hilo.

(a) Mhe. Waziri, ni kweli kwamba SMZ haina hatimiliki ya Shamba la Makurunge;

(b) Kama Serikali haina hatimiliki ya shamba hilo hatua gani zimechukuliwa kupata hati hiyo; na

(c) Wale tunaosema wamevamia shamba hilo inasemekana kwamba wamepewa kihalali. Je, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilihusika katika ugawaji huo?

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira** – Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 18 kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika , ni kweli hadi sasa bado Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haina hatimiliki ya shamba la Makurunge;

b) Hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo: Hivi karibuni wenzetu wa Tanzania Bara walituomba hekta 20,570 za shamba lile kwa kuwapa wawekezaji Kampuni ya SEKAB kutoka Sweden kuotesha miwa kwa kutengeneza nishati. Tumewapa hekta hizo na sasa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imebakiwa na hekta 6,217

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeunda Kamati Makatibu Wakuu wa pande mbili za Muungano kutafuta njia za upatikanaji wa hatimiliki ya shamba hilo. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wametaka hati ya shamba lile itolewe kwa taasisi moja wapo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ikamuandikia Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuipatia hatimiliki ya shamba hilo Chuo cha Kilimo Kizimbani. Lakini bado Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haikujibu barua hiyo. Tunapofuatilia Katibu Mkuu huyo hutwambia bado hajakutana na Wanasheria wake kumaliza mchakato huo. Bado Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaendelea kuwasiliana na Katibu Mkuu huyo; na

c) Waliovamia shamba hilo ni wananchi wa vijiji jirani na SMZ imefanya mazungumzo nao ya kuwaondosha na imewapelekea barua za kuwataka wahame. SMZ haihusiki na uvamizi huo.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nikiri kwamba

hekta 20,000 zimegaiwa kwa kampuni moja na SMZ na SMT imeshiriki kutoa eneo hili:-

a) Je, nini faida ya SMZ kwa kutoa eneo hili kama kweli ilikuwa ni letu?

b) Maeneo ambayo yamebakia ya hekta 6000 tumeona baadhi ya uvamizi wa wananchi na kwa kuwa SMZ haikushiriki kwenye uvamizi huo ni nini tamko la serikali kwa wavamizi hawa.

c) Kwa kuwa maeneo ambayo yamebakia sasa zaidi ni yale maeneo ya ufukwe na maeneo haya wahalifu wamekuwa wakiingia siku hadi siku na kutoa malalamiko kwa halmashauri ya eneo lile. Nini hatua ya serikali kwa ajili ya kulitumia eneo lile na kuondosha ufalifu?

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Spika, nakumbuka Mhe. Mwakilishi ni Mjumbe wa Kamati ya PAC na pia nakumbuka tumelitembelea eneo lile sote kwa pamoja na tumegundua ukweli wenyewe ulivyo. Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo tulikubaliana nao na tumezungumza kwamba moja katika kazi ambayo watatusaidia katika kipindi hiki ni kuhakikisha kwamba wale watu ambao wamevamia eneo lile wanawapatia eneo jengine ili wawaondowe rasmi. Kwa hivyo, jukumu la kuwaondoa SMZ tulikuwa tunalo lakini sasa wenzetu madhali wameshatwambia watatusaidia tunasubiri utekelezaji wao.

Mhe. Spika, suala la pili kuhusu hatua za serikali ni kwamba kama nilivyosema kuwa sasa hivi moja katika hatua kubwa iliyochukuliwa na serikali ni kuhakikisha kwamba eneo lile tunawakabidhi wenzetu wa Chuo cha Kilimo – Kizimbani, na bahati mbaya walikuwa wamechelewa kidogo kutokana na muundo wa bodi. Hivi sasa bodi imeshaundwa na tayari tumeshaunda kamati ya watu 8 ambayo itasimamia suala la kupatikana hatimiliki, kama Mhe. Mwakilishi anakumbuka tulivyokubaliana na wenzetu wa Wilaya ya Bagamoyo kwamba wao watakuwa hawana tatizo watatukabidhi ardhi ile tuweze kuitumia na tutapata hati na tutaondokana na lile suala la Katibu Mkuu ambaye alikuwa anatubabaisha kupata hatimiliki.

Mhe. Spika, tukishapata hatimiliki mikakati yetu ambayo tumejipangia. Moja ni kuhakikisha kwamba tunazalisha tena ng'ombe chotara kwa ajili ya kuwauzia wananchi wa Zanzibar. Jengine ni kuhakikisha kwamba tunatafuta wawekezaji, maeneo ambayo tumeyakagua sote tumeyaona ni mazuri na yanafaa sana kutokana na masuala ya utalii. Kwa hivyo, tutawatafuta

wawekezaji wawili waweze kuweka mahoteli ambayo yatatusaidia kupata fedha zaidi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kuna mambo mengine mawili ambayo tumekusudia pia kuyafanya. Moja ni kuhakikisha kwamba tunaweka viwanda vyetu vya kutengenezea chumvi, pia tunataka tuweke suala zima la ufugaji wa samaki.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ardhi tuliyonayo hapa Zanzibar ni ndogo. Je, Mhe. Naibu Waziri una mpango gani wa kuliendeleza shamba hilo kwa maendeleo ya mifugo, uwekezaji, kilimo na shughuli nyengine.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Spika, hivi muda mfupi nilikuwa nikijibu kwamba moja katika lengo letu ni kuhakikisha tunaliendeleza kwa kilimo na ufugaji. Wale ambao tumelitembelea lile shamba kwa kweli ni shamba moja zuri sana, hata mimi kama nakatiwa kipande basi nitaliendeleza vizuri zaidi.

Mhe. Spika, moja katika tatizo ambalo limetukabili kipindi kirefu ni kwamba unalima pahali ambapo panakuwa sio pako, ni sawasawa na kama yule mtu unayekaa nae nyumbani kumbe hana cheti cha ndoa siku anayoamua kuondoka ndio utajua kwamba sio mke wangu. Kwa hivyo, ndio huwezi kwenda kuliendeleza shamba hilo ukaweka mambo yako mengi ukafanya kubwa ya kilimo baadae unakuja kuambiwa hilo eneo sio lako uondoke. Mhe. Spika, nafikiri ingekuwa tuna hatimiliki tokea mwanzo, suala la kuombana ombana lisingekuwa na nguvu.

Mhe. Spika, madhali sasa hivi Chuo chetu cha Kilimo Kizimbani kina vijana ambao wataliendeleza lile shamba na litakuwa zuri na pia tunatafuta wawekezaji kama tulivyosema mwanzo ili tuliendeleze kwa manufaa ya Zanzibar.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, wakati huu ni wakati wa ukweli na uwazi, mwaka juzi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi tukatembelea shamba la Bagamoyo pamoja na Kamati yetu ya Fedha kwa wakati ule. Moja katika mambo ambayo tumeyahoji ni hiyo hatimiliki ya shamba hilo la Makurunge.

Mhe. Spika, jibu tulilolipata ni kwamba Zanzibar haiwezi kupewa hatimiliki kwa sababu ardhi ya Tanganyika haiwezi kumilikishwa Serikali ya Mapinduzi

ya Zanzibar. Hivyo, Mhe. Naibu Waziri kujibu vile leo ana uhakika au anawadanganya wananchi.

Mhe. Spika, jambo jengine la pili ni sheria gani ambayo inaweza ikatusaidia tunapokwenda Mahakamani wakati ardhi tunayoililia sio yetu. Ninachokijua kwamba shamba la Makurunge wameazimwa Wazanzibari ili waendeshe shughuli zao za mifugo kwa wakati huo na wakashindwa kuliendeleza. Hivyo, tutakuwa na hoja ya kulidai shamba hilo.

Mhe. Spika, ni kwamba serikali ilitakiwa ilitumie shamba lile kwa wakati na kwa manufaa na nilitarajia kwamba mwaka jana katika mpango wa mkakati wa uhakika wa chakula moja katika mambo niliyohisi kwamba serikali itatilia mkazo ni kuliendeleza shamba lile, lakini ule mpango wa mkakati wa uhakika wa chakula umekufa hauna maelezo katika kitabu cha kwanza na cha pili.

Hivyo, serikali inapopanga mipango yake kwa wakati ule wa shida tu haitizami kwamba shida inaweza kuondoka na baadae ikarudia.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira:** Mhe. Spika, kwanza nataka nimwambie mambo ya kijeshi yanakwenda kijeshi, unapozungumza la nyuma linapokuja lile la mbele huwa la mbele ndio linalochukuliwa. Kamati ya PAC nafikiri ni mashahidi wakiwemo Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, Mhe. Omar Ali Shehe tumekwenda kwa pamoja na ninachokijibu hapa sijibu kwamba ninadanganya. Mhe. Spika, hivyo ndivyo tulivyokubaliana na Mkuu wa Wilaya kwamba kwa taasisi itaweza kupewa hatimiliki, serikali kwa serikali haipeani waraka. Kwa hivyo, ninachojibu hapa ni cha uhakika wala sidanganyi na wala sitowadanganya wananchi wa Zanzibar. Mhe. Spika, ni kwamba mipango yote iko sawa na kwa sasa hivi tunategemea wakati wowote kuweza kupata hatimiliki kupitia Halmashauri ya Wilaya.

Mhe. Spika, kuhusu swali lake la pili ni kwamba Zanzibar haikuazimwa ilipewa lile eneo, utata ukaja pale pale kwamba tulikuwa hatujapata hatimiliki na limetumika kipindi kirefu sana shamba lile kwa ajili ya kuzalisha ng'ombe wengi sana. Ni kwa nini tumesita hatukuliendeleza ni mambo ambayo siwezi kuyasema huko nyuma kumetokezea nini. Lakini nafikiri hilo ni bahati mbaya kwa sababu wameshapita Makatibu Wakuu wengi na wengine wamo humu humu wanaweza kunisaidia sababu zilizopelekea mpaka ile miradi iliyokuwepo ikafa.

Mhe. Spika, hapa nimejibu mara mbili, moja juu ya maazimio ya serikali kupitia Chuo cha Kilimo Kizimbani bado lengo letu ni kuliendeleza shamba lile kwa mambo zaidi ya matano. Moja nimesema kuliendeleza kwa njia ya utalii kwa sababu ni eneo linavutia na ni zuri. Pili ni ufugaji wa ng'ombe chotara

ambao utatusaidia hapa Zanzibar. Tatu tunaweza kusema kwamba kutakuwa na ufugaji wa samaki na nne pia kutakuwa na suala utengenezaji wa chumvi.

Kwa hivyo, mambo mengine yatakayojitokeza kama nakumbuka Kamati ya PAC hivyo ndivyo tulivyokubaliana kwamba tuliendeleze kwa mambo ambayo yanakubalika, wao hawatotoa hatimiliki ya lile shamba labda tuseme kwamba tunalo sisi tu tusiweze kumkodisha mtu mwengine. Kwa hivyo, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba shamba lile ni letu na wenzetu wametukubalia kutupa hatimiliki kwa sasa hivi.

**Nam. 4**
**Wodi ya Wazazi**

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji -** Aliuliza:-

Wodi ya Wazazi ya Hospitali ya Rufaa Mnazi Mmoja ni ndogo mno ukilinganisha na mahitaji ya sasa. Kwa kuwa hii ni wodi muhimu kwa kutoa huduma kwa wazazi wa kawaida, wazazi wapya, wazazi waliokwisha kujifungua watoto watano na pia wale wanaohitaji kujifungua kwa operesheni.

Je, Serikali ina mikakati gani ya makusudi ya kujenga Hospitali ya Wazazi ambayo ni maalum kwa huduma hizo na ambayo itakidhi haja kwa sasa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa hivi sasa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii haina mpango wa kujenga hospitali nyengine ya wazazi, bali inaendelea na jitihada zake za kuiimarisha huduma za uzazi katika hospitali na vituo mbali mbali vya afya vilivyopo Unguja na Pemba miongoni mwa jitihada hizo ni:-

- Kufanyiwa matengenezo makubwa pamoja na vifaa sehemu ya wazazi (*Maternity*) katika hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ushirikiano na *ZAYEDESA*;

- Matengenezo ya vifaa pamoja kuweka *theatre* mpya katika Hospitali ya Wazazi ya Mwembeladu;

- Wodi mpya ya wazazi katika Hospitali ya Kivunge;

- Ujenzi wa nyumba 40 za wafanyakazi katika vituo mbali mbali vya afya Unguja na Pemba;

- Upanuzi wa Chuo cha Afya Mbweni ambao utaongeza idadi ya wafanyakazi wakiwemo wakunga; na

- Mpango wa uhakika wa upatikanaji wa damu salama kwa wazazi wanaojifungua kwa upasuaji (*operation*).

Mhe. Spika, hatua hiyo iwapo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itaona kuna haja ya ulazima wa kujenga hospitali ya wazazi hapo baadae haitasita kufanya hivyo, kwani ni jukumu la wizara yangu kutoa huduma bora za afya na zilizo katika mazingira mazuri kiafya kwa wananchi wetu.

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Mhe. Spika, nakushukuru naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ni kwamba hali ilivyo sasa katika wodi ya wazazi ya Mnazi Mmoja ni ya msongamano kiasi ambacho kile chumba kinachotakiwa kitumiwe kwa wanawake kwenda kujifungua huwa hakitoshi, inabidi wanawake wengine wajifungue katika chumba kile kile ambacho wengine tayari wameshajifungua au huwa wanaugua wakisubiri kwenda katika chumba cha kujifungua.

a) Je, serikali inachukua mkakati gani wa madhubuti na wa haraka kuona kwamba msongamano huu unaondoka?

b) Kwa kuwa wanawake ni zaidi ya asilimia 50 ya idadi ya watu wote wa Zanzibar na kwa kuwa tendo la kujifungua huwa ni kuzalisha nguvu kazi ya taifa, na kwa kuwa hali ya Wazanzibari ni ya umasikini?

c) Je, serikali haioni umuhimu kwamba sasa wodi ya wazazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ikapewa kipaumbele katika bajeti ili ikageuzwa kuwa ni idara ili shughuli ya wazazi kwenda pale kwa kuchangia ikaondoka na vile vile matatizo mengi ambayo yanaikabili wodi hiyo yakaondoka?

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, mikakati ambayo wizara yangu imeiweka ni kama tulivyoelezea. Kwanza tumeshaiona hiyo hali ya msongamano katika wodi za wazazi na ndivyo tulivyoamua kuiboresha Hospitali yetu ya Mwembeladu ili kupunguza huu msongamano unaokuja Mnazi Mmoja uweze kupungua kwenda Mwembeladu. Pia kuziboresha hizi hospitali zetu nyengine kwa sababu kinachoonekana inawezekana wakati mwengine katika suala alilouliza mheshimiwa ni kwamba

wengine wanakuwa katika wodi za kawaida. Pia nao huwa wanakuja wanasongomana pale katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, tutakapoiboresha hii Hospitali ya Mwembeladu hali hii itapungua itakwenda huko.

Mhe. Spika, suala jengine ni kwamba kwa kuanzisha idara sasa hivi naona hakuna haja kwanza tuache hii hii wizara na hiki kitengo chetu cha wazazi na nafikiri shughuli zitakwenda vizuri kama tunavyotegemea.

**Mhe. Ahmed Nassor Mazrui:** Ahsante Mhe. Spika, mimi mwenyewe nilikwenda kutembelea juzi nikaona hali ni ngumu kweli msongamano ni mkubwa sana. Mhe. Spika, pale kuna jengo lilikuwa la Kiwanda cha Kuzalisha Madawa, sasa hivi ni mazalio ya paka na panya. Haoni mheshimiwa kama hili jengo linafaa kwa kuzalishia wazazi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, jengo hilo tunalifahamu lipo, lakini labda niseme kitu kimoja. Sasa hivi kama nilivyosema suala letu hili ni kwamba tunahakikisha kwamba tunatengeneza wodi za Mwembeladu na kuboresha vituo vyetu vilivyopo vijijini. Mhe. Spika, kama italazimika kufanya hivyo basi haina haja kwenda kwenye hiyo hospitali inayozalishwa panya. Mhe. Spika, ni kwamba tutakachokifanya pale katika wodi ya wazazi ya Mnazi Mmoja lile jengo lililojengwa juu jipya linauwezo wa kupandisha ghorofa mbili, na hivi karibu Mwenyezi Mungu alinijaalia nilikwenda Washington katika mambo tuliyoyazungumza basi jambo hili nalo tumelizungumza.

Ni kwamba tunafanya jitihada lakini bado tunahisi hili suala huenda likahitajika hapo baadae kuongezwa hayo majengo. Kwa hivyo, tumeliombea hili suala Mungu akitujaalia tuweze kupatiwa kuongezewa ghorofa mbili katika jengo hilo. Kwa hivyo, tunategemea hapo baadae baada ya haya tunayoyafanya na hilo nalo litaendelezwa na hali nafikiri itakuwa nzuri.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kidogo niongeze kwa ujumla kumjibu Mhe. Mwakilishi. Mhe. Spika, ni kwamba chumba cha kuzalisha sasa hivi cha Mnazi Mmoja ni cha aina yake, kwa kushirikiana na ZAYADESA pamoja na Wafaransa ni kwamba chumba hicho kimejengwa jengo jipya, zuri na vimetiwa vifaa vya kisasa ni kwamba mzazi akitiwa pale kuzaa basi na yeye anajisikia katika raha iliyoje. Nafikiri Mhe. Mwakilishi ipo haja uende ukatembelee wodi hiyo mpya.

Mhe. Spika, baada ya hayo jumba lile lililokuwepo sasa hivi si pahali pa paka kuzaa au kutoa kinyesi. Sasa hivi Mhe. Spika, tunatumia na tumeweka maabara

ya chakula, dawa na vipodozi, mchele wote mbovu sasa hivi unapimwa pale, tumetia vifaa vya kisasa na vitu vya kisasa, ni kwamba tunatengeneza kidogo kidogo kwa mujibu wa uwezo wetu tuliokuwa nao.

**Nam. 14**

**Ujenzi wa Njia za Ndani (*Feeder Roads*) - Pemba**

**Mhe. Rashid Seif Suleiman -** Aliuliza:-

Kwa vile baadhi ya njia Pemba zinaendelea kujengwa na Wakandarasi na nyengine kwa ushirikiano kati ya Wizara na NORAD.

Je, nini muelekeo wa njia nyengine za Feeder Roads kama njia ya Pembeni, Ndagoni na Birikau katika Jimbo la Ziwani?

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Mawasiliano na Uchukuzi -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kwamba ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajenga barabara sita za Mkoa wa Kusini Pemba kwa kushirikiana na Serikali ya Norway (*NORAD*). Ujenzi wa barabara hizo unaendelea kwa awamu, hivi sasa ujenzi unaendelea katika barabara ya Mtambile- Kengeja hadi Mwambe na barabara ya Mtambile hadi Kangani. Kuhusu ujenzi wa barabara za Pembeni, Ndagoni na Birikau katika Jimbo la Ziwani ujenzi wake unatarajiwa kutekelezwa na Wizara yangu kupitia fedha za mfuko wa barabara.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa wizara imeingia mkataba na hili Shirika la NORAD kujenga hizi njia tano zilizoko Mkoa wa Kusini wamepungua sana uwezo wao kwa sababu zana zote zinapelekwa katika maeneo hayo, na muda wa mkataba ni miaka mitatu au zaidi.

a) Je, anatuhakikishia vipi kwamba na hizi njia ndogo ambazo zimeachwa kabisa sasa hivi zitashughulikiwa pamoja na upungufu huo?

b) Tulipata taarifa kwamba fedha hizi zingetumika vile vile kununulia vifaa vya ziada. Kuna jambo gani lililokwamisha vifaa hivi havijanunuliwa lakini vinatumika vile vile vya zamani na

kwa nini bado havijanunuliwa na hali ya kuwa njia zinaendelea kujengwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika mkataba wetu na NORAD baadhi ya vifaa vitanunuliwa na vyengine vitatengenezwa na vyote vinafanyika hivi sasa vyengine vimeshanunuliwa na vyengine viko njiani. Lakini hata vile vifaa vya Idara ya UUB vimo katika mkumbo wa kufanyiwa matengenezo kupitia NORAD.

Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba ujenzi wa barabara za NORAD hausimamishi kazi zetu kwa barabara za SMZ na kwa barabara hizi za Jimbo la Ziwani ni kwamba kazi zinakwenda vizuri, barabara ya Ndagoni imo katika barabara inayotoka Wesha kwenda Mkumbuu nafikiri Mhe. Mwakilishi ni shahidi mzuri barabara ile ina kama kilomita 15 na tumeshafanyia matengenezo kama kilomita 10, lakini bado inahitaji matengenezo mengine ya ziada tunaahidi kwamba tutaitengeneza kwa sababu mfuko wa barabara fedha wameshatupatia. Kwa bahati nzuri barabara hii Shirika la Umeme nalo liliingiza nguvu zake tumenunua *culvite* kwa ajili ya barabara hizo kutokana na fedha za Shirika la Umeme.

Mhe. Spika, barabara ya Birikau fedha tayari zimeingizwa kwa robo ya nne kutoka mfuko wa barabara ile barabara ya Pembeni bado fedha hatujapata.Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi asiwe na wasi wasi uwezo wa kufanya kazi hiyo tunao na *inshaallah* tutaufanyia kazi.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi nina wasi wasi ule ule wa Mhe. Rashid kwamba ujenzi wa barabara hizi za NORAD umeifanya sasa hivi serikali ishughulikie barabara hizi na kuziwacha zile barabara nyengine nyingi ikiwemo ya Kangani, Mkanyageni. Kwa hivyo, mheshimiwa hawaoni kwamba kwa kweli kitendo cha serikali kukubali kujenga barabara hizi kwamba kutaathiri barabara nyengine za *feeder road* hili hawakuliona na mapema.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, tunazipenda sana barabara zote ziwe na ujenzi tofauti lakini kutokana na kiwango cha fedha ambacho tumepata kutoka Norway na makubaliano yetu yalitulazimisha lazima na sisi tushiriki katika ujenzi huo ili kazi hiyo iweze kufanyika.

Mhe. Spika, hizi barabara za NORAD zote ni za Mkoa wa Kusini Pemba na hiyo aliyosema Mhe. Mwakilishi ni ya Mkoa wa Kusini Pemba, bahati nzuri barabara hii ujenzi wake unategemea mpaka imalizike barabara ya Mgagadu Kiwani ndio tutakwenda katika barabara ya Mkanyageni – Kangani ndio

programu yetu inavyosema. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi asiwe na wasi wasi kwa hilo tunakwenda kwa awamu kwa muda wa miaka mitatu.

**Mhe. Suleiman Hemed Khamis:** Mhe. Spika, na mimi nina swali moja la nyongeza naomba kumuuliza Mhe. Waziri. Mhe. Spika, miongoni mwa *feeder road* ambazo zimetajwa hapa ambazo zinategemewa kutengenezwa nataka nimuulize Mhe. Waziri ile barabara ambayo inaelekea Msuka ni moja katika *feeder road* ni lini barabara ile itatengenezwa. Ya pili ni ile ambayo inatoka Konde kwendea Makangale lini *feeder road* ile itatengenezwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, kwanza barabara ya Konde – Msuka sio feeder kwa sababu ndi ile ile barabara ya Wete-Konde, mkataba wetu na mjenzi wetu ni kwamba mpaka Wete-Konde lakini pale tuna uwezo wenyewe SMZ kumalizia mpaka tukafika kule Msuka usiwe na wasi wasi. Hili la Makangale pale kuna matatizo ya kimazingira wakati mwengine wataalamu wa mazingira hawajutuwekea wazi wazi kwamba je tuweke lami au tusiweke lami, nafikiri hili ni mjadala mkubwa. Hata hivi juzi tuliwahi kuwasikia wananchi wa kule wanazungumzia suala hilo kwamba tukijenga sijui itakuwaje.

Mhe. Spika, ni kwamba bado mjadala unaendelea kuna kipindi Wizara ya Mawasiliano tulikuwa tuko tayari lakini Wizara ya Kilimo ikawa na wao wana mashaka na suala hili. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Mwakilishi tushirikiane tukae meza moja tuangalie ili tupate jibu la pamoja kwamba je, inawezekana kujenga na watu wa mazingira wakaturuhusu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi:** (anaendelea) Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii na nitachukua muda mfupi sana. Kwanza naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kuna jambo moja ambalo Waheshimiwa Wajumbe wako wengi wamelizungumza ambalo linahusiana na mafuta, napenda kulizungumza mwanzo.

Wajumbe wako wengi wamekuwa na mashaka kwamba labda wizara au serikali imeanza kuhofia au kuogopa kuhusiana na suala hili la mafuta. Mhe. Spika, napenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wajumbe wote, yaani wa CCM, CUF, wananchi wa Pemba na Unguja, wananchi wa Tanzania, Afrika ya Mashariki pamoja na dunia kwa jumla.

Kwa kweli bado serikali kupitia wizara inaendelea na mikakati yake ya kuhakikisha tunaendelea na zoezi zima la utafutaji wa mafuta. Kwa nini Mhe. Waziri kwenye bajeti yake hakulitaja ndilo sio langu, lakini napenda nikuthibitishieni hilo na wala hakuna wasiwasi wala woga. *(Makofi)*.

Mwezi mmoja uliopita tulikuwa na semina nyengine pale Mbweni ambayo ilihusisha mawaziri wote, ambapo tulizungumzia juu suala hili.

Mhe. Spika, inawezekana kabla ya kikao hiki hakijamalizika na tutaangalia na mazingira, kuna sheria ambazo zinatakiwa kupitishwa na Baraza lako tukufu hili izipitishe na inawezekana zikaja hapa, kwa ajili ya kuendelea na maandalizi hayo. Kwa hivyo, inawezekana tukaja na Sheria ya *Petroleum Supply Act and Zanzibar Energy Act* hapa, hizo tumeshajiandaa na wala hakuna hofu hiyo. Waheshimiwa Wajumbe hilo nataka mlielewe na tunaendelea.

Suala jengine ni kuhusu miongoni mwa kero ambazo zipo na zimezungumzwa. Mhe. Spika, mara nyingi wajumbe wako wamekuwa wakizungumzia juu ya suala la kuwa na umeme mbadala, pamoja na kwamba juzi tumekuwa na *cable* kutoka Tanga na kesho kutwa tutakuwa na *cable* nyengine ya *megawatts* 100 itakayokuja hapa Unguja. Lakini bado kuna haja ya lazima na kwa hivi sasa haja hii imeongezeka zaidi.

Sote tunakumbuka hivi sasa wenzetu kule *TANESCO* wanatu-*bail* kwa asilimia 168 tofauti na wenzetu *TANESCO* wao wanawa-*bail* kwa asilimia 21. Hali ambayo imepelekea hivi sasa *ZECO* inadaiwa na *TANESCO* karibu shilingi 29 bilioni, kitu ambacho si kweli kwamba *ZECO* itaweza kulipa deni hilo. Sasa ile haja ya kuwa na umeme mbadala lazima ishughulikiwe kwa nguvu zote.

Mhe. Spika, tukiacha hii ya 168, wiki iliyopita *TANESCO* wameanza kuleta *tariffs* nyengine ya asilimia 34. Kwa hivyo, asilimia 34 tukijumlisha na asilimia 168, yaani tutakuwa na asilimia 202. Kwa kweli barua yao kidogo si nzuri, maana yake wamesema kama tunayo hoja basi twende *EURA*, lakini sisi makubaliano yetu na *TANESCO* na wala si *EURA*. Hii ndio hali ambayo tunayo hivi sasa *(Makofi)*.

Kwa hivyo, Afisi ya Mhe. Waziri Kiongozi na Mhe. Waziri Mkuu kule ambao walikuwa walishughulikia suala hili, basi ni lazima sasa waongeze kasi mara kumi zaidi na wala sio mara mbili *(Makofi)*.

Kwa upande wa wizara mtakumbuka huko nyuma kwamba tulikuwa na Miradi ya *CUF* na wenzetu wa Israil, nashukuru mimi mwenyewe kwa bahati niliongoza ujumbe kwenda nchini Israil. Kwa kweli tunaendelea na hali hiyo na tuko pahala pazuri.

Hivi sasa Shirika la Umeme tayari limeshawalipa Idara ya Mazingira shilingi 15 milioni kwa ajili ya kukamilisha tathmini ya kimazingira. Kwa upande wao wameahidi baada ya miezi miwili kazi hiyo itamalizika. Lakini wale wenzetu wa Israil Kampuni ya *SDE* na Mr. Weba juzi alikuwepo hapa kwa ajili ya kuendelea na zoezi hilo. Kwa hiyo, tunaendelea kutafuta umeme mbadala.

Mhe. Spika, huu wa *CUF* ilikuwa uanze na *megawatts* 10 na pole pole uendelee hadi kufikia *megawatts* 40. Hali hii tunategemea kuifanya kwa visiwa vyote vya viwili Unguja na Pemba.

Jambo jengine ambalo litakuwa ni la mwisho ambalo lilizungumzwa na baadhi ya wajumbe, juu ya suala la kilimo hasa kilimo cha mboga mboga, ambapo kuna dhana mara zote hivi sasa hoteli za kitalii zinachukua mboga kutoka Bara.

Mhe. Spika, kupitia Jumuiya ya Wazalishaji wa Mboga Mboga hapa Zanzibar, zaidi ilikuwepo kwenye Wilaya ya Magharibi na hivi sasa imeingia kwenye wilaya nyengine. Kwa kweli tayari wameweza kujipanga vizuri na wanazalisha mboga mboga hizi na nadhani kuna eneo wamejenga hapa kwa ajili ya kuhifadhi.

Kutokana na hali hiyo, hivi sasa wamiliki wa mahoteli wengi wamekuwa wakinunua bidhaa hizi za mboga mboga kutoka kwao moja kwa moja, wanaepuka sana kununua zile bidhaa kutoka Bara, ambazo mara nyingi zinakuwa na *chemicals*.

Mhe. Spika, mchango wangu ulikuwa ni huo. Isipokuwa nataka nirudie tena kusema kwamba Waheshimiwa Wajumbe wasiwe na wasi wasi juu ya suala la utafutaji wa mafuta na kwamba linaendelea.

Kwa hivyo, hivi sasa tunaendelea na mchakato wa kuwapata vijana ambao watakwenda kusoma kwa ajili ya kujiandaa na shughuli hiyo, ingawa jambo hili si la leo wala kesho. Kwa sababu lazima kufanyike mambo mbali mbali, kama vile *environmental study* yasijekutokea kama yale ambayo yametokea

kule Marekani, ambapo Kampuni ya *British Petroleum* (*BP*) tumesikia ilikuwa ikihangaika kutokana na uvujaji wa mafuta.

Kwa maana hiyo, lazima kuwa na uangalifu wa kutosha kuona hali ya mazingira hatoharibika, wavuvi wataathirika vipi au hawatoathirika na kama wataathirika nini kifanyike.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru, ahsante sana *(Makofi)*.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia nafasi asubuhi hii ya kuweza kutoa mchango wangu kuhusiana na Bajeti yetu ya Serikali.

Mhe. Spika, kama bajeti ilivyojieleza kuwa ni Bajeti ya Demokrasia na Maendeleo. Kiujumla kadri nilivyosikiliza mawasilisho ya bajeti ya wenzetu jirani hapa na bajeti yetu, basi bajeti yetu pamoja na yote ni nzuri kuliko ya kwao. *(Makofi)*.

Isipokuwa jambo moja ambalo naomba sana Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa ujumla ijitahidi kuona jinsi gani tunaweza kujikwamua na suala zima la utegemezi, kwa sababu bado uchumi duniani haujatulia na unaweza kutuharibia mambo yetu mengi.

Lakini katika hili napenda kuchukua nafasi hii pia kuwapongeza sana kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Amani Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad kwa kufikia uamuzi wa busara wa maridhiano. Sambamba na wao nimpongeze sana Mhe. Rais wa Tanzania Jakaya Mrisho Kikwete, kwa sababu na yeye anaunga mkono suala hili pamoja na Jumuiya za Kimataifa, ambazo zinaunga mkono *(Makofi)*.

Sasa kwa kupitia maridhiano haya tukiweza kufanikisha masuala yote haya, basi inawezekana hata bajeti yetu inaweza kupata unafuu fulani kutokana na misaada ambayo tunaweza kupata kwa wahisani.

Mhe. Spika, nikitoka kwenye pongezi hizo nataka nizungumzie suala dogo tu, lakini kubwa. Katika hotuba yetu kama wengine walivyozungumza kwamba suala la karafuu halikuguswa, pamoja na kwamba hivi sasa karafuu pengine imeshuka au kauli yoyote ambayo inatumiwa, lakini bado ni zao kuu la biashara nchini petu.

Kwa kweli wasi wasi wangu hapa Mhe. Spika, napenda atakapokuja Mhe. Waziri kufanya majumuisho asijekulisahau, kwa sababu sitaki nipige buti. Mwaka juzi tarehe 8 mwezi wa Oktoba, 2008 Mhe. Waziri naomba unisikilize

vizuri hapa, tulimshuhudia Bwana Membe akitiliana saini ya Mashirikiano ya Kiuchumi na Kijamii na nchi ya Madagascar kuhusu uuzaji wa zao la Karafuu, wala Mhe. Waziri hakutueleza chochote kuhusiana na hili.

Kwa kweli sijui suala hili kwa sababu tayari wameshatiliana saini hawa, linaendelea kuuzwa kwa utaratibu upi na makubaliano gani baina ya SMZ mpaka mtu wa kusaini alikuwa Bwana Membe wakati wa kusaini karafuu zetu.

Kwa hivyo, hapa nataka kupata maelezo mazuri, ili niweze kufahamu, kwa sababu tokea asubuhi Mhe. Spika, tunazungumza mambo haya, yaani kila pahala yanagusa kero hizi na haya ni matatizo. Kwa mfano, mtu anapoingia ndani ya nyumba bila ya kupiga hodi wakati mwengine inakuwa shida kidogo.

Sasa suala hili la karafuu wakati niliona kwenye televisheni akisaini Bwana Membe sikuona kama kuna mjumbe kutoka SMZ na wala hatujapata tamko la SMZ kuhusiana na hili. Vile vile nakubali kukosolewa kama imefanyika hivyo, lakini napenda kupata maelezo ya kina na hususan ninapoona kwamba halipewi nguvu wakati tunajadili hotuba kama tunavyofanya hivi sasa na Hotuba yenyewe ni ya Serikali.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo napenda nizungumzie kidogo juu ya suala la uhusiano wa kifedha, ambapo maelezo yake katika kitabu yapo kwenye kifungu cha 143 ukurasa wa 73 na kuendelea, inasema kuhusu gawio kutokana na Fedha za *BoT*.

Mahusiano haya ya kifedha pamoja na kwamba kitabu hiki kinatuambia kuna mambo sita ambayo tayari yameshapatiwa ufumbuzi. Naomba radhi sana Mhe. Spika, maana kila mtu anafahamu vyake na akili ni nywele. Lakini kadri ya ufahamu wangu na ninavyoyaelewa haya mambo kwa kiasi, basi naona miongoni mwa haya mambo sita yaliyokubaliwa labda ni mawili tena ninazosababu.

Mhe. Spika, tukiangalia kifungu cha 145 ambacho ndicho kinachoeleza hayo mambo kuanzia (a) mpaka (f). Suala la (a) linazungumzia kuhusu gawio la 4.5 na kwamba Zanzibar nayo imeruhusiwa kukopa, kutafuta mikopo au misaada. Sasa hapa huwa ninajiuliza na ninapenda kutoa historia ndogo tu, naomba radhi sana.

Kwa mujibu wa kuundwa kwa *BoT* wakati ilipovunjika hiyo *East Africa Currency Board*, ambayo ilikuwa ikisimamiwa na Waingereza, Zanzibar ilikuwa na *assets* zao pamoja na *share* ambayo ilianzisha hiyo *BoT* na kwa bahati nzuri takwimu ninazo.

*Assets* zake Zanzibar baada ya kutolewa ile *dividend* ilikuwa ni Paundi za Kiingereza laki 950. Lakini na *share* yake ambayo kila mwanachama aliyokuwemo kwenye hiyo *East Africa Currency Board*, Zanzibar ilipewa Paundi za Kiingereza 82,810 na wenzetu Tanganyika, Uganda pamoja na Kenya wao walipewa Paundi za Kiingereza 668,884. Sasa unapofanya mahesabu hapa unakuta hisa ya Zanzibar kutoka *BoT* ni 11.02.

Kwa hiyo, nikikuta hii 4.5 ambayo kwa kweli Mhe. Spika tumeshachoka kuipigia kelele, lakini tutaendelea mpaka pale tutakapoona hatima inakuwaje. Jambo la msingi nadhani wenzetu wawe wasikivu pamoja na kuheshimiana katika hili, yaani tusing'ang'anie kitu kwa sababu wengine wanapenda, lakini tuwe na hoja za kufanya hivyo.

Kwa mfano, mimi nilipokuwa nikisoma vitabu na kuiona hii asilimia 4.5, basi niliiona lakini kwa mgao mzima na wala sio kwa upande au sehemu moja tu. Tukija kwenye Tanzania unaikuta Zanzibar *share* yake kwa *BoT* ndio hiyo 11.02, unaposoma ile *overall* iliyokuwa ikitolewa ya *East Africa* yote kwa wakati huo, ikiwemo Uganda na Zanzibar ilikuwa nchi kamili, basi kule mgao wa pamoja ndio Zanzibar ilikuwa inapata hiyo 4.5. Sasa sijui kwa nini wenzetu waichukue hiyo na kuiweka hapa.

Kwa maana hiyo, ndipo ninaposema kwamba hatujafikia muafaka na wala hili tusilichukulie kuwa limetatuliwa. Kwa sababu hii sio haki yetu kwa mujibu wa *shares* pamoja na *assets* ambazo Zanzibar imechangia kwa kuundwa hiyo *BoT*.

Mhe. Spika, na suala hili nasisitiza sana kwamba liendelee kupigiwa kelele, kwa upande wangu napongeza kwa kuanzishwa ile Tume ya Kutatua Kero, lakini bado tume ile inazo kasoro. Karoso yake ni kwamba pamoja na kuwa na uwakilishi wa Zanzibar na Tanganyika, lakini ile Zanzibar haijakamilika. Kwa sababu Wazanzibari wanaowakilisha pale wana-*share common interest* na wale kule, yaani inafika pahala mtu anaambiwa hiyo sio sera ya chama chetu, inakuwa bado anazuiwa na vikwazo.

Kwa hivyo, nadhani tungeliongeza nguvu hizi kamati kwa ajili ya kuona maslahi ya nchi hii yanapatikana.

Nikiendelea na mchango wangu nataka nizungumzie kidogo tu, kwa sababu Mhe. Mjumbe aliyekaa kitako amekaribia kunifilisi kuhusu suala zima la utafutaji wa mafuta pamoja na uchimbaji.

Mhe. Spika, katika hili kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Amani Abeid Karume kwa kuliweka wazi tena wakiwepo wote, yaani pale alijiamini kwamba yeye ni Rais wa Zanzibar. Kwa

hiyo, hakuna mjadala wala hakuna mtu ambaye anaweza kusema maneno. *(Makofi)*.
Sasa nimuombe Mhe. Waziri pamoja na wanaohusika wote kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba suala la mafuta si la utafutaji tena ni uchimbaji. Kwa sababu maeneo ambayo mafuta yapo mambo yako nje na wala sio suala la kutafuta tena. Isipokuwa ni kufanya utaratibu wa kukamilisha hayo mambo ambayo alisema atayaleta na mafuta kuchimbwa.

Mhe. Spika, pia nigusie kidogo kuhusiana na suala zima la umeme. kwa kweli suala hili linayo matatizo ya *tariffs* hizi na nilitegemea Mhe. Waziri labda angelitueleza chochote.

Kwa sababu mimi ni miongoni mwa wanakamati tunaoshughulikia masuala haya, tulikwenda kufuatilia na tulikuwa na miadi na waziri husika Mhe. Ngeleja na kutupangia mpaka muda tukutane lakini bahati mbaya. Lakini ninapata usahihi sasa baada ya Mhe. Naibu Waziri kusema hata barua tunazoletewa zinakuwa za kijeuri.

Kwa sababu alitupangia twende, basi tulitoka na kwenda kule Waheshimiwa tumeacha yetu na baada ya kufika yeye alitafuta safari zake na kuondoka tena bila ya taarifa. Mhe. tumeshafika uliposema tukutane, basi anatoa visingizio vyengine. Sasa hii inaonesha ni dharau, kwa sababu kama yeye ni mkubwa ambaye tunamheshimu angalau angetupa taarifa kabla na wala sio kutusumbua, kama mtu aliyechoka anamwambia mtoto akija fulani mwambie sipo, mtoto atasema baba kasema nikwambie hayupo, ndivyo hali ilivyokuwa.

Mhe. Spika, hapa napenda kidogo niseme kwamba, suala hili lilizungumzwa kwa kiasi chake na alifikishiwa mpaka Rais wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, baada ya kuelezwa hali halisi kwa sababu ni habari ndefu sana wala sitaki niitoe hapa. Lakini kutokana na hali ilivyo Mhe. Rais aliona kwamba Zanzibar inayo haki ya kupata *share* ya kulipia umeme sawa na wenzao, kwa sababu *EURA* ilipandisha viwango hivi kwa asilimia 21.7 kwa upande wa Tanganyika na sisi labda alijua kwamba tunayo mafuta basi walitupandishia asilimia 168.

Katika majadiliano ya nenda rudi, basi Mhe. Rais alimuagiza Mhe. Waziri Mkuu wake awaandikie *EURA* kwamba na sisi tulipishwe, yaani *tariffs* ziwe sawa baina ya Tanganyika na Zanzibar. Lakini hilo mpaka leo liko kimya na wala sijui kama Mhe. Waziri anacho chochote cha kutueleza hapa.

Jambo la msingi la kuzingatia hapa kwamba ukimya wao pengine sijui niseme na jeuri kidogo iliyokuwemo inatupeleka pabaya. Kwa sababu mpaka tunaondoka pale kamati yetu tunaondoka nayo kwamba Zanzibar inayo deni la

zaidi ya shilingi 30 bilioni wakati huo tulioambiwa ilikuwa ni shilingi 30 bilioni ina maana mpaka hivi sasa imeshaongezeka.

Vile vile na *surprise* nyengine ni hii ambayo aliyoitoa Mhe. Naibu Waziri kuwa ipo na asilimia nyengine ya 34 iliyoongezwa ambayo inafanya sasa inakuwa asilimia 200 ya umeme Mzanzibari alipie. Kwa kweli hii sio haki, lakini ni changamoto kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwamba tuone kuna haja ya kupata umeme wetu wenyewe bila ya kungojea kutoka Tanga au Ras Kilimoni.

Kwa sababu hata huu wa Tanga Mhe. Spika kulikuwa na changamoto zake mpaka umewaka, yaani ulikatwa na wengine wameshazuia na wala hawataki kufanyika chochote ikabidi kamati tutoke kama jeshi hapa. Kwa kweli tulikwenda na tulifanyakazi nzuri sana na baadaye tuliacha kazi inafanyika na umeme *Alhamdulillah* hivi sasa.

Mhe. Spika, nadhani katika masuala haya yanayohusu mambo ya muungano, basi ni sisi wenyewe kuwa majasiri pamoja na kuwa na uhakika wa kile ambacho tunakifanya.

Kwa mfano, mambo ya sheria sioni kama ni tatizo, kwa sababu sheria si msahafu inaweza kubadilishwa, pia ikiwa ni muungano Mhe. Spika, napenda kutoa mfano rahisi tu, pamoja na nguo nzuri sana niliyoshonewa wakati *birthday* yangu nilipotimia umri wa mwaka mmoja, basi siwezi kuivaa hivi sasa, yaani sijui nitoke vipi nje au mkono wangu utapita vipi kwenye kanzu hiyo ya mwaka mmoja. Sasa ndivyo ninavyoufananisha huu muungano wetu.

Wakati ambao tumeungana na hivi sasa kwa kweli kuna mambo mengi hapa ambayo yanasababisha tubadilike, ikiwa ni kukaa upya tukaanza moja au kuanza na ile *original* tukaifanyia marekebisho kwa hali ambazo tunazo hivi sasa basi hii inaweza kutuondoshea kero. Vyenginevyo ushauri wangu ni kwamba tufanye kama tulivyofanya suala la mafuta, yaani kila tunaloliona linatukwaza Baraza ni hili na waamuzi ni sisi na Kiongozi wetu ni wewe Mhe. Spika pamoja na Mhe. Rais ndiye atakayekuwa msemaji wetu.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende kidogo kwenye suala la mwisho kuhusu maakaazi bora. Jambo hili kwangu naona bado pamoja na hatua zinazochukuliwa na hivi sasa *Block No*. 10 tayari limeshamalizika na watu wameshapewa nyumba, sasa na tunapongeza hilo. Lakini bado Wazanzibari wanashida kubwa ya makaazi.

Kwa hivyo, katika shida hii naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Spika kwamba serikali ikae na kufikiria upya sera ya kupanga hayo makaazi

yenyewe. Kwa kweli nimeshashauri sana na ninakubali serikali kama serikali haina uwezo wa kutujengea sote ikatupa nyumba. Lakini ni vyema kupanga maeneo na kila eneo lijengwe vipi, yaani ramani watoe wao, ili mfumo mpya wa kisasa wa kupitisha miundombinu pamoja na kuweka majengo katika hali ya kupendeza.

Mhe. Spika, kwa mfano kama hivi viti ambavyo tumekaa hapa, kama ingekuwa kila mmoja anacho kiti cha aina yake sijui ingekuwaje, lakini viti vyote viko sawa. Kwa hivyo, hata viwanja vingekatwa na kuwa na ujenzi wa aina hiyo, basi tungeweza kuwapatia makaazi mazuri Wazanzibari wengi zaidi pamoja na kupanga mji wetu na kupendeza.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja hii. Ahsante sana *(Makofi)*.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, ahsante kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa. Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kutoa mawazo yangu kidogo, kwa sababu michango mingi imeshazungumza maeneo mengi sana.
Vile vile nisiwe mwizi wa shukurani lazima nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar pamoja na wasaidizi wake wote wawili, Mhe. Waziri Kiongozi pamoja na Mhe. Naibu Waziri Kiongozi kwa juhudi yao ya kuisimamia Ilani ya CCM na kuweza kufika hapa tulipo *(Makofi)*.

Mhe. Spika, ni kweli kabisa kwamba katika awamu hii imechukua nafasi nzuri ya kuishughulikia Ilani na kufikia pahala. Ijapokuwa pamoja na mambo mengine ya amani na utulivu, lakini juhudi zimefanywa na ushahidi wa wazi upo. *(Makofi)*.

Kwa mfano, siku hizi ukitaka kuja mjini unachagua pa kupita, yaani ukitaka upite Mkwajuni, Kiwengwa, Pongwe, Kusini na kutokezea mjini, vile vile ukitaka unaweza kupita Kandwi unafika mjini. Kwa kweli juhudi zimefanywa na sisi wananchi wa Zanzibar tunapaswa kuziunga mkono kweli.

Vile vile ninawaomba watendaji wafanyekazi zao kwa mujibu wa utaratibu na sheria zilivyo na wala wasijegawika makundi. Maana watendaji wakigawika makundi ni sawa na wanasiasa kama hawasikilizani basi kazi hayendi. Kwa kweli ninayo hofu hii sijui itamaliza vipi, kwa sababu jana niliona timu ya urais walivyovaa jezi, basi nimeona hapa kipindi kilichobakia sijui kama tutafanyakazi vizuri na lile gazeti nimeliacha.

Kwa sababu kuna washambulizi Maalim amewekwa mbele kama mlinda mlango, Mhe. Waziri Kiongozi yupo nyuma ya Waziri Kiongozi Mstaafu Mhe. Moh'd Gharib Bilali, Mhe. Ali Juma Shamhuna katikati, sasa ninaoona hee! Kazi itafanyika hapa. Kwa kweli niliona mchakato mkubwa tena ni mgumu. *(Kicheko/Makofi).*

Lakini mawazo yangu kwa mujibu wa Baraza hili lilivyo.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, Dk. Mwinyi yumo?

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, Dk. Mwinyi hayumo, lakini Dk. Sheni yumo na alikuwa akihema sana, sijui kwa nini. *(Kicheko/Makofi).*

Sasa mambo haya yakiwafika watendaji tutakuwa na tabu kubwa sana katika kukamilisha ilani yetu hatua iliyobakia. Kwa hivyo, nawaomba wanasiasa watulie kidogo, watangaze dhamira zao, lakini bado wasubiri ili tukamilishe Ilani yetu ya CCM kama ilivyopangwa.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa niende kwenye ukurasa wa 50 kifungu cha 54 ambacho kimenipa wasi wasi kidogo, ukurasa huu unazungumzia kuhusu mfumko wa bei. Kwa mujibu wa takwimu alizozitaja Mhe. Waziri alisema kwamba kwa kiasi kikubwa mfumko wa bei umepungua sana nchi petu. Kwa kweli ni jambo la kupigia mfano tena la kulifurahia sana. Lakini mimi linanitia wasi wasi kwa zile sababu tatu alizozitaja.

Sababu zilizotajwa ni kuwa na hali ya hewa nzuri, kupungua kwa bei za bidhaa za chakula pamoja na kupungua kwa bei za mafuta. Mhe. Spika, mambo haya yaliyotajwa sijui yamechukuliwa lini kwa ajili ya kufanyiwa kigezo kuhusu mfumko wa bei.

Kwa sababu hivi sasa bidhaa hasa vyakula bei zimepanda sana. Sasa Mhe. Waziri anapoleta bajeti na sisi tukaichangia na sote tukasikilikana na kitu kikawa kiko wazi wazi kwamba hakisemi kweli, yaani hakilingani baina ya matamshi na hali halisi ilivyo ni kosa kubwa sana.

Kwa mfano, hivi sasa mchele bei ya chini ni shilingi 1,000/- kwa baadhi ya maeneo si bei ndogo wakati mchele huu hauna sifa lakini watu wanakimu hali halisi ilivyo. Kwa ufupi wanaita mapembe bei yake elfu moja haijashuka lakini sukari imetoka shilingi elfu moja mpaka shilingi elfu moja na mia nane ni bei kubwa sana.

Hivi sasa mtu wa kawaida anashindwa hata kumiliki robo kilo ya sukari, anauziwa shilingi mia nne kwa robo kilo. Sasa haya mambo ambayo tunayataja

katika bajeti lazima tuyafanyie utafiti na tusione tabu kufanya marekebisho hafla wakati bajeti yenyewe haijasomwa.

Chengine ni kupanda bei kwa mafuta ghafla kutoka elfu moja na mia mbili sasa hivi *disel* ni shilingi elfu moja mia nne na thalathini na tano ni bei kubwa sana. Hapa nasahihishwa ni shilingie elfu moja na mia sita na kitu, sasa mambo haya niliyotaja yanaweza kusababisha mfumko mkubwa wa bei hapo mbele na jambo ambalo linaweza kuleta mfumko wa bei ni mafuta, kwa sababu kwa mujibu wa wataalam wanasema kwamba mfumko wa bei unashuka pale tu wakati bidhaa za vyakula vinapokuwa nafuu.

Lakini sasa hivi bei za vyakula ziko hivyo na tulitegemea labda serikali itaangalia katika sekta ya kilimo ili kupunguza huu mfumko wa bei, kwa sababu siku zote kutegemea dukani tu basi tutakuwa na matatizo makubwa bei itakuwa haishuki na tutaendelea kuwa na hali ngumu ya maisha.

Mhe. Spika, pamoja na yote tunayoyaona lazima tukubali kwamba suala la kilimo ndio mti wa mgongo. Lakini kwa hali hii tunayokwenda sio mti wa mgongo tena, sijui itakuwa ni nini tena. Kwa sababu siku zote tunazungumza kwamba tutabadilisha mazingira ya kilimo kutoka kilimo tulichokizoea na kutumia kilimo cha kileo. Lakini hadi leo kama utakaa pale Mkwajuni Kinazini au Potoa, Mkwajuni Sokoni utaona hali ya wakulima wanavyosumbuka sana. Wanasumbuka kwa sababu sio hiyari yao, kwa sababu kilimo sio jambo la hiari akitaka mtu atalima na kama hataki atalima kwa sababu masikini yoyote hana uwekezaji utakaomsaidia isipokuwa kilimo.

Sasa ipo haja serikali ikaona kwamba badala ya kuwapunguzia misamaha wafanya biashara au wawekezaji, sasa tuone kwamba tunaingia katika fani ya kufidia gharama za kilimo. Gharama ya kilimo inaweza kufidiwa kama tuna utaratibu mzuri, ni kudhibiti hali ya mfumko na serikali kupanga fungu la kuona mkulima kama kaona kwenye bajeti mafuta yamezidi zaidi ya hapo. Lazima serikali ione kwamba ina fungu la kudhibiti ile hali halisi ilivyo mpaka tukaifika bajeti nyengine.

Kwa mfano, kama serikali imetangaza bei ya mafuta ni shilingi elfu moja na mia sita, lakini serikali ina uwezo wa kuona kwamba kwa muda wote huu kinachopanda juu basi serikali ifidie mpaka tufike kwenye bajeti nyengine. Hapo tutakuwa tumewasaidia sana wakulima kuliko kuwapunguzia misamaha hawa wafanya biashara na wawekezaji. Kwanza wawekezaji wengine mimi siwapendi wanakera kweli kweli, baada ya kutokea msukosuko wa fedha, wawekezaji wamekuwa maadui kwa huko kwao. Wamekula hasara wamekuja kwetu wanawatafuta mameneja ambao sio ndugu zetu.

Mameneja wale wanaagiza vyakula na vitu vyengine mahotelini mwao lakini mtu wa chini anafika kudai milioni kumi mpaka kumi na mbili ni jambo ambalo serikali imetulia haishughulikii, juzi nilijaribu kumtania Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Uwekezaji kwamba zipo hoteli zaidi ya tano katika ukanda huu wa Mashariki wanadaiwa kila hoteli zaidi ya shilingi milioni mia nne.

Mhe. Spika, hivi mtu zaidi ya milioni nne umekuja kuwekeza katika nchi hii ya kimasikini bado maana yake hulipi unaondoka nazo karibu wawili wameondoka nazo pesa na waliobakia wanakusanya waondoke nazo, bado serikali inaona kwamba muwekezaji aje tu. Hili ningemuomba Mhe. Waziri akamtaka Waziri wa Biashara, Viwanda na Uwekezaji kufuatilia hili tatizo kwa sababu hizi zipo. Kuna hoteli juzi zilitajwa hata kwenye mawio na wananchi wetu wanatutegemea sisi sana kwamba wametuwakilisha humu ili tuwasemee matatizo yao. Tunaposema wenye mamlaka ya kufuatilia ni serikali na serikali ndio zile Wizara. Kwa hivyo hili namtaka Mhe. Waziri aje alitolee maelezo baada ya kufanya utafiti ambao sio mkubwa kwa sababu ripoti hizi wilayani zipo, shehiani zipo na hata serikalini kwenyewe zipo.

Mhe. Spika, muwekezaji ambaye ana nia ya kuwaibia Wazanzibar afutiwe kibali mara moja kwa sababu sisi tumetoa ardhi zetu kwa manufaa ya nchi yetu na wananchi wake, isiwe kwamba tumetoa ardhi zetu lakini manufaa yaende huko huko wachukue wawekezaji ambao hawatusaidii kitu. Nafikiri Mhe. Spika, kwa hili nimeeleweka.

Jengine nilitaka kuzungumzia kitabu cha pili ukurasa wa 48 sekta ya elimu. Sekta ya elimu tunaisifu sana na imejitahidi sana kuondoa matatizo ya wanafunzi katika madarasa na sehemu nyengine, sasa hivi wanafunzi wote wenye haki ya kusoma darasa la kwanza wanapatiwa nafasi ni jambo zuri, hata katika *millennium* sisi tumetangulia maana yake malengo ya *millennium* ni mwaka 2013. Lakini sisi tumeshatangulia na tumeshakaa kitako tunasubiri wenzetu waje tuwapokee.

Lakini sekta hii ina matatizo makubwa na tatizo ambalo linaweza kuzuka hivi sasa na kuzua mgogoro ni chama cha walimu na Wizara ya Elimu. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inavyodaiwa na Chama cha Walimu hakiwasikilizi matatizo yao na wanavyohisi ni kwamba chama cha walimu kinawatatiza kinyume na utaratibu.

Mhe. Spika, hiki chama cha walimu kipo kihalali na kimo katika katiba kwenye kifungu cha 20 (1). Kifungu hiki sikinukuu kwa sababu kina maelezo marefu lakini kinazungumzia uhalali wa walimu au uhalali wa kujikusanya na kutoa

maoni, kwa hivyo Wizara ya Elimu kupitia chama chao kinawanyima haki hiyo kuwashirikisha zaidi katika bajeti na mambo mengine.

Haya mimi sibuni lakini jana tu baada ya kumaliza kikao hao wadau wa chama cha walimu wametutafuta na wametwita na kutuletea ushahidi ambao wao wenyewe wanao, kwamba yapo mambo na wamemtaka Mhe. Waziri wakae nae pamoja wayazungumze ili kuondoa migogoro.

Moja kati ya matatizo hayo ni maslahi na hili sio walimu tu peke yao na watu wengi huwa wanadai hata Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wamedai lakini tayari imetengenezewa ile *scheme of service* inasubiriwa iwekwe vizuri. Sasa sijui hawa walimu wao wamezingatiwa vipi katika *scheme of service* kwa sababu na wao ni wadau wakubwa wa kupeleka nchi mbele.

Lakini pia walizungumza kwamba walikuwa wanataka maelezo kuhusu namna ya michango ya walimu inavyokwenda na inavyotolewa na inavyotumiwa. Sasa wakati huu niwa uwazi na ukweli, sasa basi angalau wawekwe uwazi wawe wanaona angalau sio vizuri japo wanachungulia, lakini sasa ukiwakandia kabisa unaweza kuzuka mgogoro.

Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri wa Elimu pamoja na kamati yetu tuone na tukae ili tutafakari hili kabla halijaleta mgogoro kwa sababu inavyoonekana linapanda juu kidogo kidogo na linatafutiwa pahala. Sisi jana tuliwaamulia kwamba hili kubwa sio dogo sana na msema peke hana makosa kwa hivyo wacha tukae na Mhe. Waziri pamoja na nyie na sisi ili tulizungumza nafikiri limeeleweka.

Mhe. Spika, chengine ninachotaka kukizungumza ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, mimi shahidi kwamba imefanya mambo mazuri, imejenga majumba yale ambayo yamezungumzwa katika ukurasa wa thamanini na nne na mambo mengine, lakini kutaja yote mazuri ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kama hujataja kuwepo kwa madawa nchini bado hujasema kitu kwa wazanzibar. Kwa sababu yaliyobakia yote yanapamba tu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii cha msingi tiba na hivi sasa tuna upungufu mkubwa wa madawa.

Hata yale madawa ya kuhami hamna kwa sababu nilishuhudia juzi katika jimbo langu kuna gari fulani lilianguka na wachezaji wa mpira ilisababishwa na hawa jamaa wanaofanya misereko. Mimi kwa kuwa nina hamu bado ya kurejeshwa jimboni nikaingia gari ya majeruhi niende nao Mnazi Mmoja nilijuta, kwa sababu shindano moja ya tetnasi shilingi elfu nane na mia tano mara thalathini na tatu wagonjwa wale ilibidi zote nizitoe mimi.

Lakini pia niwashukuru sana hawa wenye kuuza madawa nilipoona mambo yamenizonga nimempigia Mhe. Ali Suleiman Ali usiku hana, nikampigia Waziri wa Afya simpati na diwani mmoja akanambia usipate tabu nenda utapoa kajaribu kukopa utapata nashukuru nimepata karibu laki nne na hamsini nimekopeshwa. Sasa hospitali kama ile kubwa ya rufaa kwamba nayo haina dawa ya akiba ni dhambi kweli kweli.

Ukiona ilivyopambwa mapaa, chini *tiles* na afisi nzuri unapita juu kwa juu na unatokeza chini lakini yale yote mwananchi hayaoni kinachoonekanwa ni dawa. Mhe. Spika, naiomba sana serikali itenge fungu maalum la kununulia dawa kila mwaka na zitumike vizuri kwasababu dawa wakati mwengine serikali huwa inatenga fungu lakini linakuwa halipatikani vizuri.

Jengine nililotaka kuzungumza haraka haraka kwanza ni miradi ya wananchi lakini na CDF katika ukurasa wa kumi na sita, katika upande wa miradi ya wananchi waziri hafanyi haki na kama hafanyi haki aambiwe hadharani. Itakuwaje fungu tumelipitisha hapa la miradi midogo midogo ya wananchi unapeleka barua hata kujibiwa hujibiwi sio tunasema wale wenzetu wana dharau lakini hata Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi una dharau, kwa sababu sisi wajumbe na ndio tunaopitisha fungu lakini mtu akileta barua hujibu maana yake hii ni kebehi au dharau sisi tunakutegemea sana hujaingia katika ile timu lakini najua mwaka 2015 huenda ukaingia na wewe ukajaribu. Lakini kama tunafika hali hii waheshimiwa wenzio tunahitaji kupatiwa pesa za miradi ya wananchi kama zilivyo ndani ya kitabu cha bajeti hatuzipati.

Mhe. Spika, changine inavyoonekana hizi pesa ulizozitaja wala hazikutumika vizuri kwa sababu umeshindwa kuzifafanua na umeshindwa kueleza miradi mingapi, miradi hii iko wapi na wapi. Kwa hivyo hilo kwa uchungu nasema utaje utakapokuja kutoa maelezo, Mkanyageni kupitia kamati ya maendeleo kiasi fulani, Konge hizi huko Matemwe usitaje kwa sababu hazijatiwa mimi ndio ninajua kwamba hujatia usitaje, lakini mwengine wataje ili tuone kwamba zile fedha zinatumika kihalali kwa sababu ni fedha za wananchi na zinasaidia nguvu za wananchi.

Bado nasisitiza zinapoletwa barua ujibu kwamba barua yako tumeiona lakini kwa bahati mbaya kwa mradi ulioutaja huwezi kupata fedha. Mtu anaridhika kwa maneno tu sasa wewe hata kwa kalamu humridhishi. Sisi ndio wadau wa nchi hii kwa kuwa tunawakilisha watu. Sisi hamsini ni watu wakubwa sana na tuna mchango mkubwa wa kumwambia mtu kaa madarakani. Sasa kama tuna madaraka ya kumuweka mtu madarakani na mtu yule kakuteua wewe basi huoni kwamba sisi tunapewa kipaumbele.

Lakini Mawaziri wengi ukienda kwenye Maofisini mwao ukimwambia, hapa kaja Mwakilishi wa Matemwe anakwambia ni mtu wa kawaida huyo lakini sio mtu wa kawaida lazima mtuheshimu kama tunavyoheshimiwa na watu wetu. Kuheshimiwa kwenyewe sio asante na karibu tu, labda kile kufungu cha dhifa au takrima namsitumie kwa sisi, lakini sisi tunakuja na shida zetu nyengine hicho wekeni pembeni wenyewe, mtumie kwa mipango yenu na haulisheni. Lakini sisi tunachokifuata ni maneno mazuri na ukiwa na maneno mazuri na vitendo vizuri ndani ya utendaji utapata sifa nitatoa mfano wa watu wawili si mawaziri.

Mhe. Spika, ukienda kwa ndugu yetu huyu Mustafa Aboud Jumbe una mradi mdogo ukifika pale anakupokea na anakusikiliza na kama kipo anakwambia utapata na kama hamna ndio hamna. Lakini utamkuta waziri ana mambo lakini ya kwake yanajaa kwa wenziwe hashughulikii waziri huyo hafai. Waheshimiwa mliokuwemo katika timu, Mungu akikujaalieni kuja basi Waziri kama huyu usimtizame mimi najua mtashinda tu mkiwa na msimamo ndani ya Baraza na sisi ndio haja yetu kwa hivyo tunawaomba sana.

Mwengine ambaye ana sifa sana ya ukarimu na kuwasiliza watendaji ni Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi. Sijui kwa nini hawa wana sifa nzuri, lakini wengine wanapokwenda atakuwa yumo chumbani anamwambia yule sektari wake mwambie hayumo. Siku moja niliwahi kusikia anaambiwa, mwambie hayumo na mimi nikaona bora nisiende. Kwa sababu kule mtu haendi kwa mambo yake binafsi anakwenda kwa shughuli za kutekeleza hiyo hiyo ilani. Lakini ukisema mwambie hayumo na mlango uko wazi maana yake si unataka tusiende.

Mhe. Spika, chengine nilichotaka kuzungumza ni mradi wa CDF ukurasa wa kumi na saba. Mhe. Waziri CDF inakuja na tusipendelee kuwaiga CDF wa Tanzania Bara ambao wanao wabunge wetu yatakuwa haya haya. Tunapitisha hatupati, lakini CDF ya hapa tuifanye kama ile iliyokuweko Kenya, yao ni safi sana. Kwanza kuna fungu la serikali la kuingiza zile pesa, lakini liko fungu kwa pesa ya kwao ni mbili *percent* kwa ile miradi ambayo iko eneo la jimbo lile basi inachangia mfuko ule kuutunisha.

Lakini kwa utaratibu ambao tumeuona hapo Tanzania Bara, hapo tutakapokuja kutengeneza rasimu ya sheria, hatuutaki na lazima mje mtushirikishe, katika kuona kwamba mmeuandaa vipi mpango ule wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Hautufai kwa sababu Wazanzibar tuna choyo hatupeyani, hata ukipewa inakuwa karibu ya mwisho wa mwezi wa sita ukokolewe kokolewe kidogo hata mradi wenyewe huendi kuufanya.

Lakini utaratibu wa Kenya ni mzuri na unasukuma kweli kweli maendeleo. Tulipata nafasi ya kwenda kutembelea eneo moja ambalo wamepata mradi mashariki kule wanakuita Naivasha. Wameendelea kweli kweli na miradi inafanywa wewe mwenyewe utashtuka, kwa sababu wanafanya kazi vizuri na kamati zao zimepangika na hakuna sababu kwamba kwa nini wasipige hatua. Lakini mimi leo hapa nashangaa Kijini ina mahoteli zaidi ya matatu yaliyokuwepo pale, hakuna umeme ukiomba unaambiwa utatizamiwa awamu ya ngapi.

Hakuna barabara hao watalii wavumilivu tu lakini ni mambo ambayo yanakera. Mambo yote hamna na yapo maeneo ambayo yamewekwa au yametengwa hasa kwa madhumuni ya kuwekeza lakini miundo mbinu haiendi sio kwamba serikali inataka hivyo lakini ule mpango hatuna kwamba asilimia fulani ya miradi iliyoko kule ichangia miradi iliyokuwepo pale.

Kwa hivyo napendekeza Mhe. Waziri kwamba mtakapotengeneza utaratibu wa CDF msije kuiga utaratibu wa Tanzania Bara wa kutia fungu la fedha. Kwanza unaweka fungu la fedha baadaye asilimia fulani ya mapato yanayotokana na ukanda ule wa jimbo kuongeza nguvu ya mfuko. Isiwe kwamba sisi tunachuma nyinyi mnatumia, hilo hatuwezi. Huo ni utawala bora wa zamani, sasa hivi utawala bora kila mtu anaona kwamba hapa nadhulumika hapa naenda safi.

Mhe. Spika, baada ya hapo kwa kuokoa muda nitakuja hali ya biashara. Hali ya biashara hatuifanyi ya ndani biashara zetu zote. Tunategemea nje na hali ya biashara ambayo ina sifa sana kwa nchi ni ile inayozalisha. Nakusudia kusema kwamba katika maelezo yote katika vitabu vyetu, bahari kuu tunaeleza kwa maneno tu. Hakuna dalili kwamba serikali inajitahidi kutafuta muwekezaji wa kuvuna mali ziliomo ndani ya bahari kuu.

Kazi yetu ni kugombana gombana tu hapa hapa nchini kwa wavu wa nchi moja mshare na nini sijui, pamoja na kuwa serikali inajitahidi kidogo. Lakini bado uone kwamba bahari kuu ina mali nyingi na kama ina mali nyingi, tuone basi tunatafuta njia ambazo zinaweza kuonekanwa kwamba Zanzibar mazao ya bahari kuu yanavunwa.

Mhe. Waziri uje kutuambia tu katika uwekezaji kuna dalili za wawekezaji wangapi katika bahari kuu ya Zanzibar. Utwambie  na kama hakuna utwambie sababu nini. Unaweza kutia katika kitabu lakini utekelezaji haupo unaweza kuweka 2010 unamalizika. Tunaingia kwenye uchaguzi na 2011 inakuja bajeti itakayosomwa mwa 2011/2012 inaweza kuisha hivyo hivyo.

Lakini ninachouliza ni mikakati ipi iliyowekwa na ishara gani inaonyesha kwamba sasa hivi tunaelekea kuwekeza bahari kuu.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru sana mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa Jimbo la Matemwe bajeti ya serikali tunaiunga mkono mia kwa mia, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Ame Mati Wadi inshaalla si muda mrefu utapata meza iliyokuwa nzuri.

**Mhe. Abass Juma Muhunzi:** Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwanza naomba nitangulize maneno haya katika bajeti hii, nasema bajeti hii pamoja na kwamba ni mpango wa kawaida wa mwaka kuhusu mapato na matumizi kwa ajili ya mambo ya kawaida na maendeleo, lakini vile vile bajeti hii ndio inayohitimisha awamu yetu ya uchaguzi ya miaka mitano hii iliyopita. Lakini bajeti hii hii ndio itakayoanza na awamu nyengine ambayo tunakwenda.

Mhe. Spika, bajeti hii hii inakuja wakati ambapo kuna mageuzi makubwa ya kiuchumi katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na sisi tukiwa ni sehemu. Kwa maana hiyo, ni bajeti ambayo tuna wajibu wa kuijadili kama kawaida yetu. Lakini ni bajeti ambayo tunahitaji baada ya mjadala huu kuifanyia uchambuzi yakinifu kuufanyia mapitio ili kuangalia mfumo mzima wa bajeti na kuona iwapo mfumo huu ndio ambao utatuvusha katika mabadiliko haya ambayo tunakwenda nayo.

Mhe. Spika, nasema hayo kwa sababu kwa maoni yangu, mimi nadhani tuna tatizo la mfumo au muundo wa bajeti kuliko haya ambayo tunayajadili ya hapa kidogo. Hapa kingi na hapa kidogo na hapa kingi ni mfumo mzima. Nasema hayo kwa sababu ukiangalia kwenye muundo wa sasa hivi, tuseme mapato ya ndani kama *percentage* ya pato la taifa kwa Zanzibar ni 18.3%.

Nimeangalia wenzetu wa Tanzania ni 17% hayo ni mapato ya ndani. Ukiziangalia figa hizi zinakupa maoni ya kwamba angalau tunakwenda sambamba basi katika mfumo huu wa bajeti wa sasa hivi, ukiangalia mapato yote kwa bajeti ya Tanzania ni 33% na kwa bajeti yetu sisi Zanzibar ni 36% ukiangalia unaona ya Zanzibar ni makubwa zaidi kuliyo ya Tanzania.

Mhe. Spika, kama utaangalia kwa upande wa matumizi na nimechukua matumizi ya kawaida tena matumizi ya mishahara tu basi Tanzania ni asilimia 17% ya JDP lakini Zanzibar ni 9% ya JDP sasa ninachotaka kusema hapa ni kwamba ukiangalia kimahesabu unaweza kuona kama bajeti yetu inakwenda angalau kuweza kuilinganisha na wenzetu walioko karibu. Lakini ukiangalia undani wake unaweza kuona matatizo tuliyonayo Zanzibar ni makubwa zaidi hata kulinganisha na yale ya Dar es Salaam hapo ndipo utakapobaini kwamba

usitosheke na hizi *percentage*, pamoja na kwamba ndio kipimo *ratio very strong* katika upimaji

Lakini *ratio* ni *ratio* tu mbili kwenye tatu ni 66% na 4 kwenye sita ni hivyo hivyo. Hapa ni lazima tuangalie kwa nini ukiangalia *ratio* hizi na takwimu ambazo tunapewa unaweza kuzipa maana, lakini ukiangalia uhalisi wa kiuchumi wetu katika nchi yetu bado unaonekana kwamba unadumaa.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu matumizi ya mshahara kwa Tanzania 17% kwenye JDP ya kwetu sisi ni 9% inaonekana namna gani pamoja na kwamba JDP yetu tunaweza kuona kwamba imekua lakini matumizi yanayotumiwa kwa kuwalipa watu mishahara ni asilimia 9 tu Mhe. Spika, wakati wenzetu wana 17%. Ni sababu gani inayotupa kwamba kimapato ya ndani tunalingana ambayo mapato haya ndiyo yanayolipa mishahara pamoja na mambo mengine lakini ukija katika ulipaji mishahara wale wanaopata mishahara kwenye keki hii ya pato la taifa ni asilimia 9 tu. Wenzangu walikuwa wakilinganisha haya mapato ya matumizi ya mishahara wakiangalia na yale mapato yote wakasema ni *percentage* kubwa. Ni kweli mimi nakubali ni *percentage* kubwa ukiilinganisha kama utaichukulia *with respect to* mapato yote ambayo unayapata.

Lakini ukiangalia kwenye kipimo cha GDP na kipimo cha GDP ndio chenye maana zaidi kwa sababu hichi ndio kipimo cha uchumi wetu katika nchi. Unaona kwamba mishahara ni asilimia 9 tu. Na hapa unaona namna gani Wazanzibari pamoja na kwamba kuna keki ya taifa ambayo inaambiwa kila siku inakuwa lakini wanachokipata katika mishahara ni asilimia 9. Pamoja na *over imployment* kubwa ambayo ipo katika nchi lakini wanachokipata ni asilimia ndogo. Tatizo hapa liko wapi?

Mimi bado narejea maelezo yangu ambayo nimekuwa nikiyatoa. Kwamba kwa Zanzibar uchumi ni tatizo kubwa kuliko hili tunaloliona la kukusanya mapato TRA sijui na ZRB itaunganishwa kwa hivyo itakuwa inakusanya mahala pamoja tu *one stop center*. Bado haitokuwa ni suluhisho la matatizo yetu. Kwa sababu ni suala la kukusanya tu lililozingatiwa kwenye bajeti hii halikuangalia hicho kitakachokusanywa kinakuwa kinapatikana vipi, viwango vyake vitakuwa vipo vipi. Kama Baraza hili pamoja na serikali itakuwa ni kuunda chombo cha kukusanya, lakini yale mamlaka ya kupanga kiwango cha ukusanyaji ya kuwa hakipo, hilo linakuwa ni tatizo.

Mhe. Spika, tatizo hili linaonekana kwamba haliwezi kupata suluhisho katika Baraza wala katika SMZ peke yake inaonekana hili ni tatizo la kikatiba la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa sababu wenzetu wanaokaa katika

Bunge inaonekana kwamba upeo wa kazi tunaowapa hauwezi kufika mbele ya kuliona hili kwa hivyo ni tatizo ambalo linatuzonga siku zote.

Mhe. Spika, kwa kweli kwa sisi Zanzibar ni lazima tusikitike sana. kwa sababu tunawatumikia wananchi katika majimbo na wananchi hao wana wawakilishi wawili wawili mmoja anakuja kwenye Baraza la Wawakilishi na mwengine anakwenda katika Bunge. Hao tunaowatumikia katika kila jimbo pengine hawazidi elfu kumi (10,000) wakati mtu mmoja kwa Dar-es-Salaam au kwa Tanzania Bara anatumikia pengine zaidi ya watu lakini moja. Lakini ikawa watu hao wawili wanaoingia hapa na wanaoingia Bungeni ikawa tumeshindwa kuona njia ya kutatua matatizo yetu kwa kweli ni lazima tusikitike sana.

Mhe. Spika, mimi nafikiri wenzetu ambao wapo katika Bunge wangelijaribu kuziangalia *augments* kama hizi hasa zinazohusu namna ya kupanga viwango vya ushuru wakaviona kama ndio misingi. Kwa sababu tutaipitisha bajeti hii naipite sawa. Tulikuwa siku zote tunadai. tunasema *finance Beal* ni moja katika sehemu ya bajeti, sababu zote zinatolewa kwamba haipo, maana yake imechelewa, zinatolewa tu sababu lakini ukitaka kupanga kama tunataka ushuru kutoka kwenye Ushuru wa Forodha, tutakachopata maana hapa katika Baraza ni kusema kwamba tuwapunguzie wananchi kima hichi. Katika kupunguza sio kwamba unapoteza ilipokuwa VAT asilimia 20 ikapunguzwa mpaka asilimia 18 inasifiwa leo na waliopunguza kwamba wamefanya hivyo ili kupata *complains*, walipaji kodi walipe kwa hiari na hiyo haijapunguza VAT. Haya yangewezekana kufanyika kwenye ushuru mwengine, kuna ushuri wa forodha na kila kitu ambacho kinahusu bajeti yetu, lakini Mhe. Spika, hatuna mamlaka hayo. Sisi tutakuja kupanga hapa kukamuana tu kwa ushuru wa ndani na mwisho tunafika pahala hatuoni pahala pa kukamua zaidi katika ushuru wa ndani. ZRB, TRA, iunganike bado tutakuwa tuna matatizo.

Mhe. Spika, ukitaka uangalie namna ambavyo hii TRA kwamba ina uwiano katika kukusanya. mapato, angalia *percentage* inayokusanywa kwa kodi za TRA kwa Tanzania na uiangalie Zanzibar. Kasma kubwa ya mapato yanapatikana kwenye Jamhuri ya Muungano kupitia TRA kuliko pengine popote, hapa ni ZRB haya ya ndani ya kumkamua mwenye hoteli. Tukiendelea na mfumo huu Mhe. Spika, hizi kodi za VAT zina *discourage* uwekezaji, tutakwenda kwenye mahoteli leo tukamkamue, tutakwenda kwenye *dispensary* tukamkamue VAT, tuende kila pahala sisi tuna VAT tu. Lakini mwisho kutokana na sababu ya matatizo mengi ya kiuchumi ndani ya soko letu la Zanzibar ambalo ni dogo lakini vile vile ule uwezo wa soko nao ni mdogo. Wawekezaji watafika pahala wataona sio pahala pa kuwekeza. Wawekezaji wa nje na wa wawekezaji wa ndani.

Mhe. Spika, labda nimalizie tu kwa kusema katika hapa bado sisi tunashauri sana. zimesifiwa sana sera za CCM na ilani yake hapa lakini katika hili linalohusu roho ya uchumi wetu hapa bado hamjaweza kujisifu. Ni lazima mkae tena kwa sababu nyinyi ndio mnaokaa pamoja muone ni namna gani wenzetu watakuwa wanalegeza kamba katika kuipa Zanzibar mamlaka zaidi ya kujipangia mambo yake *effectively* and *efficiently* vyenginevyo tutakuwa tunawalaumu tu watu wa mipango, watu wa fedha lakini yale mamlaka halisi hayapo wao wanayo yale madaraka tu.

Mhe. Spika, leo tuna bahati hiyo ya kwamba muungano wetu ni wa nchi mbili, wataondoka hapa wakubwa watakwenda zao Dar-es-Salaam wakifika pale watazungumza, watachukua walichokipata, walichokikosa haya hakipatikani kitakuja hapa waziri atakitetea. Maana hata akikosa kule lakini bado hakubali kwamba yeye uwezo wake ni mdogo, atalitetea kwa sababu ni sera ya chama, atatudanganya, atatwambia sijui kuna mikopo ya nje karibuni hivi tunatengeneza. Atatwambia GFC, mambo hayo yamezungumzwa humu miaka kumi na tano tunaizungumza GFC tu. Na GFC imekuwa ikibadilishwa kila baada ya muda katibu mwengine, wawakilishi wengine wa Zanzibar wengine wamechukua vyeo vyengine mpaka wamefika wengine wamekuwa makatibu. GFC ipo hata ripoti moja kwa zaidi ya miaka 15 haijatoka iliyo ya maana ya kusaidia, lakini waziri akija atai-*defend* tu GFC inafanya kazi vizuri na wawakilishi watatoka waende kwenye GFC.

Leo nasema angalau tuna bahati kwamba ni muungano wa nchi mbili tunakwenda, tunakosa, tutakuja hapa tutaambiyana. Lakini kesho kuna muungano wa kikanda, muungano wa soko la pamoja, Zanzibar jamani zikishakukaa nchi tano, zikishakupitisha sera na zipo sera, hawawezi kukaa tu kama jumuiya ya kikanda isiwe na mipango na mikakati na sera zake. Sisi jamani tutakwenda kumuuliza nani? Maana yake tutakwenda hapo hapo Bara, lakini tukifika hapo tutasema ngoja na miye niende Kenya.

Mhe. Spika, baada ya muda fulani hili ambalo leo tuna hofu nalo kusema kweli Zanzibar itaondoka kabisa kabisa litabakia jina na hilo jina sijui litafikia pahala gani. Kwa hivyo wakati tukiingia katika muungano wa kiuchumi wa kikanda kuna kila haja ya Zanzibar kurudi nyuma, kukaa na wenzetu wa Tanzania Bara ni kwa kiasi gani Zanzibar itakuwa ina nafasi yake.

Mhe. Spika, haitakuwa vizuri hata siku moja, sisi leo tutadanganyana halafu tutaondoka watakuja waliowakali zaidi, watakuja vijana wetu ambao wanasoma historia maskuli, vyuo vikuu vinakuja watasema ulio ukweli. Ukweli utabakia hatuwezi kukaa tukausifu ukoloni lakini kama wakati wa ukoloni kama Zanzibar ilikuwa inaweza ikakaa na wenzake na ikajinasibu huyu ni Waziri wa Fedha wa Zanzibar amekaa katika East Afrika na anakuja anatoa

ripoti nimekwenda East Afrika nimeambiwa hichi. Lakini leo tunaambiwa kwamba tuna uhuru, tumejitawala lakini tunakosa maamuzi haya, hapa ni kurudi nyuma. Hatuwezi kila siku kuingia katika aibu ya kuusifu ukoloni lakini hatuwezi kusifia maendeleo yetu haya wakati tunajua kwamba tunarudi nyuma. Yanayoturudisha nyuma yamo ndani ya uwezo wetu kuyarekebisha.

Mhe. Spika, hofu zilizokuwepo katika muungano hapo zamani leo zimebadilika na ndio maana tumebadilisha mpaka sera zetu, sera ya mambo ya nje imebadilika, tulikuwa tuna sera ya ukombozi leo tuna sera ya kiuchumi, wazi wazi. Hapa ni kwa sababu tunakubali sasa maingiliano ya nchi zetu na nchi nyengine katika kujitafutia riziki za watu wetu. Sasa Zanzibar kama ni chombo kama ni nchi yenye vyombo vyake vya kupanga uchumi lakini fursa hizi bado hadi leo zinakuwa zinabinywa.

Mhe. Spika, safari yetu ni fupi mno na tunaweza tusifike kabisa. Hapa ni pahali pa kukaa na kuzingatia na nikasema kwamba bajeti hii pamoja na kujadili haya ambayo yameletwa humu ambayo. ukiyaangalia *constitutively* unaweza ukasema yanakwenda vizuri. Lakini bado kuna matatizo yaliyo makubwa ambayo kwa kweli yapo nje ya uwezo wetu Zanzibar. Ni kwa nini hayo kwa sababu hivi tusipate uwezo wa kuyashuhulikia ili tukikosea tukajilaumu sisi wenyewe.

Mhe. Spika, hatuwezi kila siku katika Baraza ikawa tunakaa sisi ndio wapangaji, ndio watekelezaji, ndio wasimamiaji lakini ikawa tunamlaumu mtu mwengine Tanzania Bara, maana yake kuna katiba hii. Vitu hivi vyote ni vyetu.

Mhe. Spika, jengine nalo limegusiwa na wenzangu hapa. Kwa sababu ya kutegemea sana biashara huduma hizi kwamba ndio masuala, ndiyo nyenzo ya uchumi wetu. Tumekwisha kufanya hivi sana, lakini bado tunaona uchumi wetu hauendi mbele. Tuna tatizo kubwa la *capacity* ya uchumi hii ni lazima kuangalia maeneo mengine na sio wigo wa ushuru. Mimi nafikiri wote wataalamu wa ushuru tukusanyike na wengine wana siasa na wataalamu wa kwenye vyuo vikuu halafu tukaeni pamoja kwamba jamani tutanuweni wigo wa ushuru hatuwezi kupata kutanua wigo wa ushuru Mhe. Spika, tusijidanganye. Tutakwenda humo humo tutasema tuwatoze watu, mwisho tutakwenda kupiga watu virungu pale Darajani tuseme kuwa ushuru ndio unapotea pale kumbe hamna kitu. Lakini *capacity* ya uchumi ndio tatizo.

Wenzetu uchumi wao katika kipindi hichi umeimarika zaidi Tanzania Bara kwa sababu tulikuwa tunakwenda hivi hivi pamoja wao wanasikitika na sisi tunasikitika lakini wameondoka huku juu wamekwenda chini ya ardhi wamekuta pale kuna gesi, wamekuta kuna mafuta na vyengine hatuwezi kuvipata tanzanait na mambo chungumzima. Lakini kwa nini vitu hivi kila siku

tunapiga kelele humu basi hata *sentence* moja ya kusema kwamba azma ya serikali ya mara hii ije hivyo tu. Tujue kwamba ilikuwa ni azma haukuwa mpango ambao hatutupata hata nafasi ya kuuhoji. Haiji pamoja na kelele zote tulizokuwa tunapiga sera ya mafuta weka sijui keshokutwa Kampuni ya mafuta waliopata (A) katika *chemistry* watakwenda kusomeshwa. Hamna jambo hata moja linaloonesha kwamba kuna jambo hili ambalo tulikuwa tupo *serious* .

Mhe. Spika, haya nasema ni mambo ambayo yangekuwa ni muhimu sana. Lakini Zanzibar kilimo kwanza ambayo ni sera nzuri sana na ni muelekeo mzuri lakini kwa nchi ambayo inayo ardhi. Kwa Zanzibar tunayo ardhi lakini bado tumeshindwa ardhi yetu iliyo ndogo kuifanya kwamba iweze kutoa kilicho kingi, lakini kilio kama walivyolia wenzangu kwa nini baharini bado tunakuchezea. Uvuvi haujapewa nafasi.

Uvuvi unakwenda sambamba na ufugaji wa samaki pamoja na usindikaji wa mazao ya baharini. Haya ni mambo ambayo tungekuwa tunayajaribu kabisa na hapa Zanzibar tuna *import* ya kamba kutoka Komoro tena wanakuja kwa wingi. Lakini na Zanzibar tumefunikwa na bahari lakini hakuna kitu tunachokipeleka, kuna pweza wawili watatu nao pia wamekwisha. Niwambieni waheshimiwa wenzangu, kwamba pweza vile ambavyo wanavuliwa tokea kwa michomo ile mpaka sasa kwa bomu, hakuna tena hata yai. Wenzetu wanavyofanya ni kufuga mashamba ya pweza. Kwa sababu haya mapweza makubwa tunayataka sisi tu watu wa Zanzibar tunaita mkuyati. Wenzetu wanakula vipweza vidogo vidogo ambayo hata huvijui kama vipweza kweli. Hawaendi kuwavua baharini ni pweza ambao wamefugwa katika mabwawa. Tunayo *opportunity* hiyo ya kwamba tuangalie kilimo na tukiunganishe na ufugaji sio wa ng'ombe kwa sababu hatuna maeneo ya kufuga ng'ombe lakini hata maeneo ya kufuga kamba na pweza. Hilo nadhani ni suala la utaalamu na serikali ingeliangalia sana hasa kwenye Wizara ya Kilimo.

Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Waziri Kiongozi, alikuja katika jimbo langu miezi mitatu iliyopita na katika mradi alioutembelea ulikuwa ni mradi wa ufugaji wa samaki. Naweza kusema sasa hivi kwa Zanzibar ule mradi ilioko Chambani ndio ulio mkubwa na aliyasikia maneno yaliyokuwa yakizungumzwa. Mradi ule umekusanya vijana karibu 200 ambao walikuwa wanazurura kabla ya kuanzishwa mradi huo, hao wote wanashughulikia mradi wa bwawa moja tu yaani mradi wa kufuga samaki na chumvi. Lakini vijana badala ya kwenda pahala ambapo hawana kazi ya uhakika wanaamua kwenda pale na wanashughulikia. Sasa tungekuwa nayo miradi kama ile *across the country* tungekuwa tumepiga hatua.

Mhe. Spika, naishukuru sana Wizara ya Kilimo baada ya matukio yale ya pindua wingi ilichukua samaki wengi lakini Wizara ya Kilimo kupitia kwa

mwakilishi ilikabidhi boti pamoja na mashine pamoja na nyavu, karibu zina thamani ya miolioni ishirini. Kwa hivyo *estimate* ya vijana waliyokupa siku ile Waziri Kiongozi karibu milioni 11 samaki wetu wamepotea. Nataka nikwambie kwamba kupitia kwenye Wizara yako ya Kilimo kumefanywa jambo ambalo limefuta kidogo yale maumivu ambayo vijana wale walikuwa wameyapata. Kwa hivyo na mimi naungana sana na Mhe. Ame Mati, kuisifu sana Wizara ya Kilimo hasa kupitia hii idara ya uvuvi.

Mhe. Spika, tusimalize hapo lakini tutakabiliwa na matatizo ya kiufundi na kiutaalamu katika ufugaji wa samaki kama kweli tutakuwa tupo *serious* ni lazima twende kwa wenzetu wenye uzoefu wa kazi Wajapan, Tailand, tumekwenda kutembelea mashamba yao ya ufugaji. Kama utakwenda kulitembelea shamba la ufugaji wa kamba Tailand au Japan ukirejea hapa hii kazi Uspika utaiacha utakwenda zako kutengeneza bwawa. Kwa sababu unawauliza baada ya muda gani mnavuna, mnapata kiasi gani kwa kweli ni pesa zilizo nyingi mno. Hivi ni vitu tunapaswa tuviangalie sana.

Mhe. Spika, lakini zaidi ni kwenye *capacity* ilivyokuwa *geographer* yetu historia inasema kwamba hapa ndio kitovu cha biashara. Bado tuitumie *geographer* yetu kama ni *comparative advantage* ya kuhakikisha kwamba hapa ndio panakuwa kitovu cha biashara. Sasa kitovu cha biashara kimeondoka, kwa Mzanzibari kutoka akenda Kenya, Tanzania Bara, akenda Uganda kwa kwenda kununua shati kwa kweli hili ni jambo la ajabu sana. Ninachosema hapa ni kwamba mazingira ya biashara yametiribuka. Kama sisi tuna *forcus* katika ushuru kama ndio *engine* ya chumi wetu hata hao wafanyabiashara walio *serious* wanaondoka na wakiondoka hata na hilo suala la ushuru nalo litakuwa limeondoka. Ni lazima mazingira ya biashara tuyarekebishe ili yawe ni mazuri ya kuweza kupata ushuru uliyo mzuri.

Mhe. Spika, sambamba na hayo Bandari pamoja na *Airport*, sasa hivi ni Bandari na *Airport* za kusafirisha watu ndio *forcus* pale hakuna *forcus* ya mizigo na ukipewa *forcus* ya mizigo ya Bandari usijiangalie wewe ukaleta *container* moja, mawili au matatu kwa ajili ya matumizi yako. Uwaangalie na wenzako ambao hawana Bandari, wewe ungeitumiaje bandari katika kuwasaidia na usaidie uchumi wako.

Mhe. Spika, bado tuna haja kubwa tena bandari nikizungumza sizungumzii Bandari ya Malindi tu bandari zetu tulizonazo hii, Bandari ya Malindi, Bandari ya Mkoani, Bandari ya Wete, ni bandari bado zilizo kubwa ambazo zikiimarishwa hizi Mhe. Spika, zitastawisha uchumi kwa haraka sana. Maana mfanyabiashara aliyekuwepo Pemba ukiangalia hizi *pries index* kama utaangalia kwa Pemba hapa mapembe ambayo tunayanunua hapa kwa 1000 au 1200 basi ongeza mia 200 au 300 kwa Pemba. Kama utakwenda uangalie hali

ya umasikini na kama utaangalia *efficiency* zinazozungumzia umasikini utaweza kuona kama kule umasikini unakuwa ni mkubwa kidogo. Lakini bado bei za vitu ziko juu, tatizo kubwa ni bandari, bandari ipo lakini haina vifaa. Kwa hivyo *flexibility* itapatikana pamoja na kwamba wafanyakabiashara nao wanapendelea zaidi kwenda katika soko lakini bado na pale patakuwa ni pahala pazuri.

Mhe. Spika, nizungumzie suala la CDF, tumepata taarifa nzuri na tumpongeze sana Mhe. Waziri ya kwamba sasa kutakuwa na mifuko hii ya majimbo, nitanabahishe kitu kimoja. Najua mifuko hii ya majimbo kwa nilivyoiangalia bajeti itakuwa ni ku-*shift* fedha zile za miradi ya wananchi na kuifanya mfuko wa majimbo na kuzipeleka katika majimbo. Mimi nasema *shifting* hii ni nzuri kwa sababu hapo zamani palikuwa kuna malalamiko jimbo hili sijapata mradi jimbo hili limepelekwa huku. Sasa hili litakuwa limeondoka kwa sababu kila jimbo litapata *check* yake.

Mhe. Spika, wasi wasi wangu ni mmoja, tukiangalia hotuba za Bungeni na hata zetu sisi hapa, wawakilishi na wabunge sasa watakuwa wanachukua nafasi kubwa ya kusimamia miradi hii. Hili linaweza likawa tatizo kubwa sana. Kikatiba bado wawakilishi na wabunge ni wasimamiaji. Tuangalie hili neno wasimamiaji halafu tulitofautishe na watekelezaji, ndio maana linatupa nguvu leo ya kusimama na kuirushia mishale serikali, tutakapokwenda tukajiingiza sasa sisi ndio wenyeviti wa kugawa hii keki, itatuzonga hii na hakuna mtu mwengine wa kuja kusema.

Sambamba na hilo Mhe. Spika, tunayo *role* ya ku-*play* sasa katika Baraza hii Kamati ya PAC ambayo imekuwa ikifika mpaka chini kule kwenye serikali za mitaa sasa inaweza ikapunguzwa kazi, tukaunda kamati nyengine inayohusu *local government authority publical accounts* nadhani hilo litatusaidia sana. kwa sababu moja katika matatizo makubwa ambayo hadi leo tunayo hatuna mfumo mzuri wa serikali za mitaa. Ndio maana leo mpaka zinatokea pesa mwenyekiti awe mwakilishi, katibu awe mbunge ni kwa sababu mfumo wetu wa serikali za mitaa bado zipo dhaifu. Serikali hapa imefeli lazima niseme. Kwa sababu ahadi ya ku-*reform* serikali za mitaa ni ahadi ya siku nyingi, lakini hadi leo bado ni ahadi ile ile, tuta-*reform*. Tunachokiogopa ni kitu gani? Hii ni kwamba tunaipunguzia *central government* kazi, tunawakabidhi wenyewe na hiyo ndio *participation* na baadaye Baraza la Wawakilishi likiunda kamati itakuwa imetanua kazi zake ya kusaidia katika. uangaliaji ya *accountabilities* lakini vile vile ya ku-*improve* ile *reform* hatua kwa hatua. Hili lingekuwa ni jambo lililo muhimu sana na ingelikuwa hii pesa inayotokea jimboni tungekuwa na pahala pa kuiweka, Mhe. Spika, pamoja na uzuri huo lakini ni lazima tuliangalie.

Mhe. Spika, mwisho ni suala la sera ya mikopo kwa Zanzibar haipo *clear* na kwenye mikopo ni mwahala ambako tunapata fedha kwa ajili ya maendeleo yetu. Unataka kwenda kukopa Uingereza lakini kwanza Mhe. Mwinyihaji anakwenda kwa Mustafa Mkulo, akimwambia kwanza ngoja kwa sababu katika kipindi hichi mimi kutokana na ratiba zangu, kwanza anakwenda kwenye jimbo lake anakwenda kwenye Bunge kwanza arudi. Atapata kwenda kukopa kupitia kwake lakini sio kwa wakati ule ambao anahitaji.

Mhe. Spika, Baraza la kutunga sheria lina mamlaka kamili sio ya kuiambia serikali ikakope hapa na hapa lakini angalau inaiwekea *limit* serikali kwamba kiwango chako cha kukopa baada ya kuangalia mfumo huu wa mapato iwe ni kiwango hiki, iachie serikali iende inapotoka. Lakini na nayo serikali iwe inayo mamlaka ya kwenda au inayo uwezo wa kwenda. Sasa sisi leo hatuna uwezo wa kuiambia serikali kwamba kopa mpaka hapa na kwa nini tuihoji serikali leo umekopa wapi na madeni yapo vipi. Wakati hata hiyo siku ya kupanga hatukushirikiana leo tunakwenda kuihoji vipi. Tumepunguziwa nguvu Mhe. Spika, lakini na serikali nayo imepunguzia mamlaka makubwa ya kujitanua, ya kwenda katika nchi ambazo inahisi zinauhusiano zikaenda zikakopa mpaka uende pale pahala ambapo SMT itataka kwenda.

Mhe. Spika, hapa lilipokuja suala la OIC ambalo leo lingekuwa linatusaidia kwa sababu tu serikali ya Muungano ilisema OIC usende kwa hivyo na Zanzibar ikarudi nyuma. Sababu chungumzima zilikuja za kidini ambazo kuwa hazina maana hata kidogo. Tunakosa fedha kutokana na *structure* yetu ya muungano. Sisi hatuhoji muungano kwamba labda tunaukataa, muungano una faida kubwa sana lakini ni lazima marekebisho makubwa yafanywe na haya mambo ya makero. Kwa nini kuwe na kero katika jambo zuri. Jambo zuri mnakaa katika *structure* zenu ambazo mmezikubali, kuna Bunge, kuna Baraza la Wawakilishi mnarekebisha jambo linamalizika. Kwa suala la kero hatuwezi hapa tuka-*allocate* pesa za watu kila siku wanakwenda kushuhulikia makero. Leo tumekuwa tunahesabu makero 1,2,3,4,5 yakiondoka mawili yanaingia tena matatu, kila siku itakuwa ni idara ya makero. Hatuwezi kuwa na idara ya makero katika nchi, tuwe na idara ya kupanga mipango yetu ili twende vizuri.

Mhe. Spika, mwisho kabisa miradi ya barabara ya Chambani imetajwa sana mwaka 2005, ninacho kipeperushi, wakati ule wa kampeni za Urais. Barabara hii ni kilomita 3.2 kutoka Kenya mpaka Miamboni itakapofika mwisho wa mwaka, sasa hivi ni miaka mitano na vipeperushi vile bado ninavyo, lakini leo sitovitoa nitavitoa October tukijaaliwa bado barabara ile Mheshimiwa iko vile vile. Mimi najua kuna matatizo ya upatikanaji wa fedha, panapokuwa na matatizo ya upatikanaji wa fedha, kile kinachoweza kufanyika kidogo basi kifanyike kwa wote. Mhe. Spika, mimi ningefurahi sana hizo fedha zilizokuwepo kama ma-*grader* yangesawazisha kwanza na kuondosha yale

mawe, angalau yakaweka kifusi, halafu ikaja lami kidogo kidogo, wala hakuna mtu ambaye angesema chochote. Lakini leo barabara sita zile zilizoko Kusini, barabara tatu ndio unaambiwa zinashughulikiwa na katika barabara tatu hizo ni moja tu ambayo inashughulikiwa kikamilifu, nyengine zote zimeachwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili nadhani lingekuwa ni jambo la busara kuona kwamba miradi yetu kutokana na uwezo wetu, basi tuondoshe kwanza shida za watu.

Mhe. Spika, kuna sehemu gari fulani tu ndio ambayo inaweza kuingia, gari nyengine haiwezi kuingia. Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na niseme tu kwamba pamoja na yote ambayo tumeyazungumza, lakini niseme wizara ukiiangalia bajeti na ukaangalia na zile bajeti ambazo zimepita, basi kuna-*improvement* kubwa sana katika wizara, lakini matatizo kama nilivyoyaeleza ni matatizo ambayo tunataka sasa tusiyaelemeze peke yake kwenye wizara, lakini tuyaelemeze yawe ni matatizo ya kinchi ya kurekebishwa ili wizara ifanye kazi vizuri zaidi. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

**Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi:** Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kuchangia katika hotuba hii muhimu sana ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba ambayo ameisoma, kama walivyotangulia kusema wenzangu bila kuchoka kwa masaa mawili na nusu na kwa kusoma huko sote tumeweza kuifahamu.

Mhe. Spika, michango yangu ilikuwa mingi kiasi, lakini kwa kuwa mingi imeshachangiwa, basi nitajaribu kuchangia yale ambayo hayajaguswa, labda nisisitize yale ambayo naona kwa upande wangu yanafaa kusisitizwa.

Mhe. Spika, nianze na suala zima la kipengele kile cha mizania ya biashara. Nimesoma baada ya Mhe. Waziri kuelezea na mimi nikapitia tena. Nadhani kwa kuwa si mchumi, sijafahamu sasa kwamba kutokana na mizania ile tumefaidika au tumepata hasara. Kwa sababu kwa ufupi nilivyoelewa Mhe. Spika, ni kwamba katika suala zima la uingizwaji wa bidhaa kutoka Bara kuja Zanzibar umeongezeka. Lakini wakati huo huo bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Bara imepungua.

Sasa mimi nikajiuliza hapa Mhe. Waziri anakusudia kutuambia nini. Amezungumza kwamba nakisi nayo imeongezeka. Mimi nahisi bado inanichanganya, lakini nataka kujua tu kwa lugha zetu nyepesi kwamba tumefaidika na mwenendo huu au hatujafaidika na mwenendo huu na kadri inavyokua sasa anatushauri nini katika mwenendo huu ambayo sasa bidhaa kutoka hapa Zanzibar kwenda kule Bara imepungua, lakini kutoka kule Bara

kuingia nchini kwetu Mhe. Spika, imeongezeka. Kwa hivyo, nitamuomba Mhe. Waziri akija hapa anielezee tu ili nipate kufaidika na hilo.

Pia Mhe. Spika, katika kipengele kile cha 59 Mhe. Waziri alizungumza suala zima la huduma za fedha. Nataka nimpongeze sana kwamba ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi limeongezeka kwa asilimia ambazo nilivyofanya mimi hapa imeongezeka kwa asilimia 29.6 kutoka mwaka jana hadi mwaka huu wa fedha. Lakini nikajiuliza katika hawa wafanyabiashara binafsi ambao wamepewa hii mikopo. Kwa sababu taifa letu tunalipigia sana kelele ya kuwanyanyua wananchi, lakini zaidi wanawake. Ndio maana ya msemo ule kwamba ukimsaidia mwanamke basi umeisaidia jamii nzima. Kwa sababu angenielewesha hapa ni wanawake kiasi gani ambao wamefaidika katika hawa wafanyabiashara binafsi, ili niweze kujua na mimi na kwa kushirikiana na yeye Mhe. Waziri kwa sababu mimi hapa nipo kwa tiketi ya wanawake, basi tujuwe suala hili kama linataka kutiliwa mkazo au vyenginevyo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kilimo katika kipengele kile cha 78 ukurasa ule wa 43 pale juu, labda ninukuu ili tuweze kufahamu sote Mhe. Spika, pale Mhe. Waziri aliposema,

Kifungu cha 78

> " Aidha ushajihishaji wa mafunzo ya kumwagilia kwa njia ya matone, yaani *drop irrigation* yametolewa kwa wakulima wenye uwezo".

Mimi nikasita hapa kidogo, nikasema kwa nini iwe wakulima wenye uwezo, hawa wasiokuwa na uwezo kwa nini wasiongezewe uwezo. Kutokana na hili na uwezo wenyewe ni katika kununua vifaa vya matumizi katika maeneo ambayo yeye ameyataja.

Mwelekeo siku zote Mhe. Spika, tunapoambiwa kwamba kunapelekwa nguvu ya aina yoyote kwa wananchi, basi pia na wale ambao hawana nguvu zile nao wapewe nguvu zile, ili waweze kufika sehemu. Lakini hawa kumbe nguvu wanazo na bado mafunzo wanaendelea kupatiwa hawa hawa ambao tayari uwezo wanao, sijui Mhe. Waziri hapa alilenga vipi, ningemuomba atakapokuja anieleweshe kwa nini wakawalenga hawa wenye uwezo na hakuwataja hawa ambao hawana uwezo. Kwa sababu kwa mtazamo wangu nadhani wangelengwa wote basi ili kuondosha dhana ya ubaguzi hapa kwamba kwa nini hawa na sio hawa. Lakini kwa sababu hawa tayari wana uwezo basi zaidi tungewatizama hawa wasiokuwa na uwezo ili nao wanyanyuliwe wawe katika kiwango kidogo cha kuridhisha.

Mhe. Spika, nitakwenda haraka haraka, nikitoka hapo katika kipengele hicho cha kilimo nitakwenda katika kipengele cha 118 cha masuala mtambuka. Nampongeza Mhe. Waziri sana tu kwamba ametambua kuwa wanawake wanaunda sehemu kubwa na muhimu kwa jamii yetu, nampongeza sana kwa hilo. Kwa sababu wanawake siku zote kilio chao kilikuwa ni nao kutambuliwa kuwa ni sehemu kubwa ya jamii.

Lakini nilipoendelea kusoma katika kipengele kile Mhe. Spika, nikabaki tena na maswali, sasa katika utambuzi huu, nafasi ambazo yeye Mhe. Waziri amezitaja kuanzia nafasi ya uwaziri mpaka unaibu katibu, kumbe bado wanawake ni wachache sana na kwa hesabu zangu mimi za haraka haraka nilizozifanya hapa ni asilimia 21 tu ya wanawake. Sasa nikajiuliza hivi hakuna wanawake wasomi ambao wanaweza kushika nafasi hizi au ni vigezo gani zaidi ambavyo wanavitumia katika kuwaweka wanawake katika vigezo hivi? Kwa sababu kama Mhe. Spika, wanatambua kwamba wanawake wanao uwezo na wanatambua kwamba wanawake wanaunda sehemu kubwa sana ya jamii na sote tunatambua kwamba wanawake ni asilimia kubwa ya wananchi wa visiwa vyetu.

Sasa kwa nini basi isifike hata ile asilimia 30 ambayo kipindi hiki tunakimalizia cha wanawake ambao tumekubaliana sisi wenyewe katika mikataba hiyo ya kimataifa ambayo tunaingia kwamba sasa tuwanyanyuwe basi wanawake waingie katika viwango hivi vya kazi au vya uamuzi? Katika kipindi kilichopita tulisema asilimia 30, lakini sasa hivi tunaelekea kwenye asilimia 50. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri aliangalie hili kwamba tukisema tunatambua basi tutambue kwa vitendo, tusiseme tu tunatambua lakini kumbe tukija kuchanganua yale mambo yalivyopangwa, tunakuta kumbe utambuzi wenyewe Mhe. Spika, haujaenda sambamba zaidi na makubaliano ambayo sisi wenyewe tunaingiliana nayo katika vyombo vya kimataifa.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye muelekeo wa mpango wa maendeleo kwa mwaka 2010/11. Katika kipengele kile cha 162 Mhe. Spika, mimi nilipokisoma hiki naona muelekeo wa bajeti yetu zaidi unakuwa ni tegemezi, kwa sababu zaidi ya asilimia 90 Mhe. Spika, tunategemea misaada kutoka nje katika shughuli zetu za maendeleo ndani ya nchi yetu. Angalau tungepishana kidogo basi katika mchango wetu sisi na mchango ambao tunaita wa washirika wetu wa maendeleo. Lakini tunapoweka asilimia kubwa kama hii kwamba itokana na washirika wa maendeleo zaidi ya asilimia 90 na mchango wetu sisi wenyewe ambao maendeleo yale yatatugusa sisi kwa faida yetu sisi tunasema tunachangia asilimia 8.5.

Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri aje atuambie ni vigezo gani na ni kwa nini ikawa hivi, kwamba hatuna uwezo kiasi hiki? Kwa sababu hawa nao

washirika wa maendeleo wanapokuja, wanakuja na masharti yao Mhe. Spika, na kipindi hiki ni cha uchaguzi, wasije wakaja hapa wakatushinikiza kufanya vile wanavyotaka wao katika uchaguzi, kwa sababu tayari wameshaona kumbe asilimia kubwa ya mapato yetu tunayotegemea kuyapata katika kipindi hiki ni lazima yatoke kwao. Mimi naogopa tena naogopa sana hapa Mhe. Spika, vinginevyo nitamuomba Mhe. Waziri aje anieleweshe ili nielewe, kulikoni ndio kweli hatuna pesa kiasi hiki au tumeshajizowesha kwamba katika masuala ya maendeleo lazima tuelekee kwa wahisani wa maendeleo, kwa sababu wanaitwa wahisani wa maendeleo.

Mimi nadhani tunao uwezo na hasa tukiangalia makusanyo yetu pamoja na kwamba kipindi hiki tunaingia kwenye uchaguzi, lakini bado tuna uwezo wa kukabili masuala yetu kwa kiasi tusitegemee sana wafadhili kwenye masuala yetu ya maendeleo. Kwa hivyo, nadhani atakapokuja hapa kunielewesha hapa Mhe. Waziri kuwa walilenga masuala gani au vigezo gani walivyotumia katika hili ili nikamuelewa basi nitashukuru sana.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limenigusa kuna mmoja wa waheshimiwa waliochangia hapa amelizungumzia ni suala hili la kaulimbiu za bajeti za serikali. Mimi ninajiuliza kwani hizi bajeti lazima ziwe na kaulimbiu na nimejiuliza kwa sababu, mwaka jana serikali ilikuja na bajeti yake hapa inasema kaulimbiu ni kuimarisha miundombinu ya kilimo na utalii. Nilichotegemea mwaka huu katika bajeti hii Mhe. Waziri angezungumza kwamba mwelekeo wa bajeti ile tumefanikiwa katika asilimia hii kilimo na katika asilimia hii utalii. Lakini kutokana na sababu moja, mbili, tatu na nne tunabadilisha mwelekeo tunaingia mwaka huu katika bajeti ya demokrasi na maendeleo. Vyenginevyo atuambie kwamba kule tumefanikiwa kwa asilimia 40 na asilimia 60 tunategemea kufanikisha katika kipindi hiki. Lakini akatuacha tu na bajeti ile ya mwaka jana ya kuimarisha miundo mbinu ya kilimo na utalii akaiwacha hewani na leo akatujia na kaulimbiu ya demokrasi na maendeleo.

Mhe. Spika, tunakuwa na wasi wasi, mimi tena nimekuwa na wasi wasi mkubwa sana. Maana yake kinachonijia mimi ni kwamba fedha zote tunazozikusanya katika kipindi hiki zinakwenda kwenye uchaguzi tu, labda na kura za maoni. Ndio maana napata dhana Mhe. Spika, kwamba ndio maana hapa masuala ya maendeleo yote tunataka hawa washirika wa maendeleo watuletee pesa, naogopa tutakwenda sivyo. Kwa sababu kuna hatari ya kuburuzwa na wahisani hawa kama sisi wenyewe hatukujipanga vilivyo.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri kwamba hebu hizi bajeti tusiweke kaulimbiu. Kwa sababu tunapoweka kaulimbiu tunategemea tuje tujipime basi tulifanya nini katika kaulimbiu ile tuliyojiwekea na ndio maana kaulimbiu hizo utasikia

siku ya mtoto duniani, kaulimbiu ya siku ya afya duniani. Kwa sababu tunaangalia yule mtoto tumemuwezesha kwa kiasi gani au katika afya tumepiga hatua kiasi gani, hiyo ndio maana yake. Lakini tunaposema tu kaulimbiu ndio hiyo halafu tena tunaiwacha tu kwenye hewa, kesho tunakwenda kwenye kaulimbiu nyengine.

Mhe. Spika, sitaki kusema kuwa Mhe. Waziri anatudanganya, sio kauli nzuri, lakini ningeomba aje anieleweshe kwa nini tukapinda haraka, maana yake tumepinda mpindo ule *U-turn*, huku hajatueleza chochote. Hiyo kilimo mbolea tulipata au hizo mbegu za ng'ombe zilikuaje, hakuna kitu zaidi ya kwamba atawawezesha wale wenye uwezo kwenye *drop irrigation*, lakini hakuna kitu Mhe. Spika. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri aje anieleweshe hili anitowe wasi wasi kwenye hili ili tuache kujiuliza haya maswali au tukenda huko tukiulizwa basi tujuwe na sisi tutalieleza vipi.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, nizungumzie umuhimu wa huu mfuko wa *CDF*. Mimi nauunga mkono kwa nguvu zote, kwa sababu kumekuwa na malalamiko mengi sana ndani ya Baraza lako, mifuko ya maendeleo ya wananchi, kuna mifuko ya maendeleo ya jamii, kuna mifuko ya maendeleo ya wanawake, kuna mifuko ya vijana na kuna mifuko mingi sana lakini utakuta inaelekezwa zaidi kwa wale ambao sijui wana mbinu gani kuipata ile mifuko au sijui labda kuna michakato ya kupita ndio wanapata na kufaidika na mifuko ile. Utakuta kuna maeneo ambayo kabisa mifuko ile haifiki Mhe. Spika.

Sasa kwa mtazamo wangu mimi hii *CDF* kwa sababu kila eneo litakuwa na mwakilishi ambaye ataingiziwa mfuko huu, basi watafaidika na pesa zile. Mimi ningeomba nimshauri Mhe. Waziri hapa kwamba miradi ile yote ielekezwe kwenye mfuko huu. Kwa sababu huko kuna wanawake, vijana, kuna hiyo jamii na wananchi, sasa hiyo mifuko yote ielekezwe huko. Lakini utaratibu wa kule nao uandaliwe vizuri. Kwa sababu kama alivyotangulia kusema Mhe. Mjumbe aliyekaa sasa hivi kama hakukuandaliwa utaratibu mzuri huko tutakuja hapa tuanze kujiuliza nani aulizwe kuhusu mifuko ile, kwa sababu waulizaji ndio sisi, kwa hivyo uandaliwe utaratibu mzuri, kama kwenye serikali za mitaa au itakavyoona serikali. Lakini mifuko hii ikishaelekezwa huko kwa utaratibu mzuri utakaopangwa, basi naamini Mhe. Spika, suala hili hapa Barazani hofu ya wawakilishi wako itapungua kwa kiasi kikubwa sana. Kwa sababu wao ndio watakuwa wana jukumu la kusimamia hiyo kwa njia moja au nyengine, kwa sababu wao ndio wanawawakilisha wananchi wao, lakini wao ndio watakuwa wanahakikisha pia kwamba lile lililokuwa limekusudiwa kwenye mifuko ile basi inafanya kazi iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, baada ya hayo nimuombe Mhe. Waziri aje anieleweshe tu kwa sababu ni ada inapoletwa hapa hotuba kama hizi na sisi tuweke michango yetu,

kwa hivyo anitowe wasi wasi niliokuwa nao, lakini pamoja na yote hayo naiunga mkono hotuba yake hii kwa asilimia mia moja mimi binafsi, lakini kwa niaba ya wanawake walioniingiza humu ndani ya Baraza lako tukufu wa Mkoa wa Mjini Magharibi. Nashukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Assaa Othman Hamad:** Nikushukuru Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Allah Subhanahu Wataallah kwa kutupa uzima na tunaendelea na shughuli zilizotuweka hapa za kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Spika, nadhani kazi kubwa imeshafanywa na wenzetu waliotangulia, nataka niamini hivyo. Lakini kwa sababu bajeti ni ya serikali na sisi tuko hapa kuwawakilisha wananchi wanaoisikiliza bajeti yao hiyo, napaswa kusema mawili au matatu.

Mhe. Spika, ulimwengu sasa umetandwa na mtikisiko mkubwa wa hali ya uchumi, hatuwezi kuepukana nayo hali hiyo na ni lazima tujipange, lakini tujiamini kutumia rasilimali zetu na utaalamu tulionao ili kuhakikisha kwamba uchumi wetu unakua kwa faida ya watu wetu na maslahi ya nchi hii. Tutafika mahali tutakuja kuwasuta wataalamu, mimi naanza kuwatetea leo, kumbe kosa tumelitenda sisi na serikali.

Mhe. Spika, mwaka jana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya mtikisiko mkubwa wa hali ya uchumi duniani, ilijipanga kwenye maeneo machache na hali ndio hii ambayo imetufikisha hapa tulipo sasa. Tuliimarisha miundombinu, lakini Mwenyezi Mungu anatupenda hali ya hewa nayo ikawa nzuri kwa ajili ya kilimo chetu, kilimo ambacho Mwenyezi Mungu anatujaalia zote rehema zake lakini sisi wenyewe hatujakuwa tayari.

Mhe. Spika, Zanzibar hii kwa jiografia yake hatutokuwa na kilimo zaidi ya haya maumbile ambayo tunayo, lakini kama maumbile haya tutayatumia vizuri basi watu wetu wataweza kula vizuri, watashiba na yumkini tutapata cha kusafirisha angalau basi kwenye haya mahusiano yetu ya kikanda. Lakini bado kilimo tumekipa mgongo, sipendi nilitumie hili neno lakini bahati mbaya leo nitalitumia tena. Zaidi tunakuwa na imla tunaandika lakini utekelezaji ndio hivyo ni tatizo letu. Naomba sana tubadilike hapa ili tufanane na wenzetu tunapitwa jamani.

Jengine Mhe. Spika, hebu tutumie hizi rasilimali na rasilimali kuu Mwenyezi Mungu ambayo katujaalia. Pale ambapo baba wa taifa aliposema ili tuendelee tunahitaji mambo manne, akataja watu na ardhi, Mwenyezi Mungu akatuambia hiyo hapo, ardhi hiyo ni hii huku juu na ile kule baharini. Sasa hii huku juu kwa hapa kwetu ni chache, lakini upeo wa bahari tumefanya nini ili kuhakikisha tunajitetea na hali hii ya maisha na kupambana na hali ya uchumi duniani.

Mhe. Spika, tulipaswa nguvu zetu tuzielekeze huko, serikali ielewe hivyo, lakini pia tuacheni woga. Kwenye bahari ile, kule kwenye bahari kuu ndiko tutakako mkomboa Mzanzibari na hali mbaya ya umaskini, huko kwenye bahari kuu ndio kwenye matarajio na hii huku meli 12. Mhe. Mohamed Ali Salim juzi aliniambia anataka apate ujumbe mdogo wa Baraza lako tukufu ili akawaoneshe jinsi mafuta yanavyo cheua, kama vile mtoto alivyoshiba maziwa ya mama yake huko Wambaa.

Lakini suala hili sitaki nilirudie sana leo, kwa sababu limeshatajwa humu. Tumekwama mpaka Naibu Waziri hapa wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kaja kutunyamazisha, hakupaswa afanye vile. Tulitaka Mhe. Waziri mwenye dhamana atuambie serikali imefikia wapi juu ya hili, Wazanzibari popote huko duniani walipo masikio yao walikuwa wanasikiliza hapa patasemwa nini kwenye vitabu vitatu hivi juu ya suala zima la mafuta, sio suala la kuja kujibiwa kwenye maswali na majibu ya asubuhi hata kidogo. Ilikuwa tulikute hapa ni mikakati, kama ni mikakati imepangwa vipi, ili na sisi tuwemo.

Mhe. Spika, hii kutaja Nigeria, Equatorial, Guine na Angola, kwani na wao si kama sisi tu, tofauti yetu sisi ni kisiwa nadhani tuna urahisi wetu zaidi kwa suala hili kulikamilisha. Tutaendelea kusafa na hali mbaya ili hali kitu tunacho wenyewe. Tena nimetishika sana Mhe. Spika, nadhani utakuja kunigaia muda kidogo. Nimeshituka niliposikia Mhe. Waziri anasema tumepata ruhusa sasa Zanzibar nayo kukopa. Nakuja kutizama maeneo ya kukopa bado tunahitaji mkongojo, kama hili ni mkongojo haya mafuta je tutahitaji kitu gani. Mhe. Waziri hapa nitaomba unipe majibu ili niridhike na sio mimi tu ninahitaji niridhike, lakini wanatuuliza huko nje Wazanzibari.

Mhe. Spika, umetajwa utalii, lakini tuutizame utalii na suala zima la mtikisiko wa uchumi duniani. Watalii wanakuja huku kama hali ni nzuri huko kwao, uchumi umetengamaa na usalama wa nchi zetu zinaridhisha, lakini hali ya uchumi ameshatuambia ni ngumu. Je watakuja watalii ama hawatakuja? Sasa tufanye nini ili kufunika pengo hilo la watalii? *Automatically* kama hali ndio hiyo, kampuni ziliopo hapa zinatakiwa zirudi kwao kwenda kufidia hiyo hali, mtalii hatokuja. Kipaumbele cha utalii kwa uchumi wa Zanzibar bado ni mtihani, nadhani turudi kule kule kwenye ile asilia ni kilimo na kilimo ni tanzu pana iko kwenye mifugo na hasa pale kwenye bahari.

Mhe. Spika, nadhani hujaniashiria lakini ninaheshimu sana kiti chako, nasubiri kauli yako kwa muda uliobaki, nina machache nimeyawacha.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa endelea.

**Mhe. Asaa Othman Hamad:** Samahani sana Mhe. Spika, nilikuwa naihesabu ile ni saa 7:00 kumbe ni saa 6:00 nakushukuru. Mhe. Spika, nakushukru sana nilikuwa naanza kutupa tupa.

Mhe. Spika, maeneo yetu kwanza ni baharini, baharini kuna mengi na yote ni mazuri. Sasa kinachotakiwa ni kujipanga, serikali ijipange vizuri, kutandika sera nzuri, kutandika sera za kuwavutia wenzetu wawekezaji. Hapa pia tuna mawili au matatu, tutaweza kupata lishe nzuri kutoka baharini. Jana wenzangu walikuwa wanazungumza tutaweza kula samaki kwa wali, kwa viazi na mambo mengine.

Lakini jengine ni ajira ya vijana wetu. Mhe. Spika, vijana tunawapoteza huko nje, na tunawapoteza pengine nasema hapa kwamba lawama isiwe kwa wataalamu iwe wanasiasa na serikali. Vijana tunawapoteza kwenye unga na mambo mengine. Hawana ajira, wanakaa vijiweni *frustration* zile zinawafanya kufanya mambo ya ajabuajabu. Tunawaondoa pale tunasema sijui tuwapeleke Tunguu tukawasomeshe, tufanye nini halafu wanarudi kule kule hatuna cha kuwafanyia. Bado, lakini kama tutapata watu watakaokuja kuwekeza kwenye eneo hili la baharini, hawa hapa Darajani mpaka anaosema Mhe. Mkuu wa Mkoa wote kama meli imewameza kwenda zao, huko miezi sita atakuja kujipanga wapi tena? Hana.

Na wale dada zetu wanaotajwa kwa haya mambo mengine, watakuwa kwenye hivi viwanda vidogo vidogo watafanya *packing* na mambo kama hayo watafaidika na ajira hii. Wataondokana na hii ndwele iliyotukabili sasa hivi. Ni nzito sana Mhe. Spika, naogopa kuitaja, lakini Waheshimiwa wanaijua.

Baada ya hilo nije katika eneo la uhusiano wetu wa hizi kanda za Afrika Mashariki na *SADC*. Huwa napata tabu sana na rafiki yangu mpenzi Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi jinsi ya ushirikishwaji wetu pale sisi Wazanzibari.

Mhe. Spika, mara moja nilikuwa na Mhe. Waziri wa Afrika Mashariki Mtanzania wetu. Nilipokuwa namuhoji juu ya nafasi yetu, akaniambia suala la upendeleo kwa nchi wanachama kwa lile wanaloliona wao kwao litakuwa ni kikwazo cha maendeleo yao kiuchumi, kijamii hata kiutamaduni lazima wa-*raise* hiyo hoja. Nafasi hiyo milango iko wazi.

Sasa nakumbuka hapa mara moja tulitajiwa kwamba tumepata nafasi kupitia huko Afrika Mashariki ya Uwanja wa Ndege wa Karume pale Pemba kama sikosei palitajwa na bandari. Lakini mara hii sikuyasikia tena humu kwenye vitabu. Labda nimuulize Mhe. Waziri, suala hili limefikia wapi?

Lakini kwa mbali kuna harufu kwamba ndugu zetu wa damu wamelikataa hili. Haidhuru wenzetu wengine Kenya na Uganda walikubali kwamba stahili yao Wazanzibari bandari huru iwepo Zanzibar. Wao kwa kujua historia yetu na umuhimu wa jiografia yetu ya visiwa vyetu walikubali hilo. Lakini sasa habari hii naitaka niisikie kutoka kwa kauli ya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, hapa hapa kwenye uwakilishwaji huwa tunasikia utata. Kuna nyakati wataalamu wetu hawaendi kwa sababu za hapa na pale. Halafu ukija ukienda huko unakuta tayari kuna *sign* zimewekwa kwamba Wazanzibari walikupo. Inaonekana kuna kutokuelewana hapa, kuna Afisi ya Mhe. Waziri Kiongozi inayoratibu mambo, kuna na Afisi ya Mhe. Rais na wao ambao kuna Idara ya Uhusiano wa Mambo ya Nje na Ushirikiano. Hawa hufika mahali ikawa hawana mawasiliano. Kwa hivyo, hawa waende au hawa wasiende matokeo yake kuna namna tu ya kwenda, lakini mwendo huu wanaokwenda ni kipi kinachopatikana kwetu?

Uhusiano wa Afrika Mashariki tulikuwa tuna wasi wasi tangu asubuhi. Zanzibar tutakosa mengi na yanatutisha Mhe. Spika, kwa sababu ikiwa leo bado yaliyopo ndani ya Muungano tunahesabu kero, yakishafika kwenye Afrika Mashariki tutaita jina gani? Mimi nina wasi wasi, kwa sababu yapo ya Zanzibar kama nchi na yapo ni ya Muungano wa Tanzania. Muungano najua yatakuwa chini ya mwavuli wa Muungano, hayo ya Zanzibar yatakuwa chini ya mwavuli upi? Huu ndio wasi wasi wangu unaponipata.

Lakini kama tunaingia ndani ya shirikisho bado kuna mwiku wa Muungano, tukiongeza na yale ya shirikisho hivi sisi tutakuwa na hali gani?

Mhe. Waziri haya ni maswali ninayohitaji majibu yako. Kwa sababu nimeulizwa huko na wananchi wangu na mimi leo nimeyaleta hapa wanahitaji kuyasikia.

Mhe. Spika, haraka haraka nije kwa wafanyabiashara kuwa wanatukimbia. Wanatukimbia kwa kukosa mashiko mazuri ya kuwaweka hatimaye tunawarundikia kodi za ajabu ajabu, tunayohisi kwamba labda ndio mafanikio ya kupata pato la uchumi wetu.

Mhe. Spika, wafanyabiashara wetu wanatusimanga tukifika hapo Bara. Nina ndugu yangu mmoja analipa kodi 2.5 bilioni kwa mwaka, yupo Dar es Salaam. Mmoja nimemkuta Mwanza tulipokwenda na kamati yangu ya Fedha na Uchumi, wenzangu walimuona. Sasa yote yale mimi najiuliza tungekuwanayo hapa kwanza wangetusaidia ajira. Wana kampuni, wana viwanda, hawawezi wao peke yao tu, wao familia nzima iko pale lakini bado wameajiri.

Mhe. Spika, niliposema kwamba twamba kiimla maana yangu ni hii. Lakini hata zile ambazo ni vyetu wenyewe magawio haya ya *BoT*, magawio yetu ya Afrika Mashariki, ya *East African Currency Board,* hili gawio sugu la 4.5 tutakwenda hivi hadi lini? Muda hautusubiri tunapitwa.

Nadhani Mhe. Waziri Kiongozi ndugu yangu, nilikusihi sana miaka miwili iliyopita kwenye ile kamati hebu tupa jicho na huu upande wa pili. Huku utapata watu wa kwenda kukinga kifua kwa sababu unazozijua wewe na mimi. Lakini hivi mnavyokwenda kwa *chain* ile ile Makamo wa Rais, Waziri Mkuu, ni mtihani na huku jopo lako kutoka Zanzibar hebu lichanganye. Mhe. Waziri Kiongozi lichanganye tukaona patafunguka ama patavunjika. Nadhani patafunguka, kwa sababu nia ni njema isipokuwa wenzetu hawajatuelewa nadhani watatuelewa.

Mhe. Spika, nije kidogo tu kwenye suala la nishati ya umeme ambalo litakuwa la mwisho. Mhe. Spika, kengele imeshalia kwamba twendako kuna hatari. Hali hii tuliikuta mwaka juzi kwenye kamati na mabadiliko ya siku ile ilikuwa haijafika 168, ilikuwa ni chini ya hapo. Tulipoihoji wenzetu kule wakatwambia hili halitawezekana mpaka pande mbili zikae. Kuliulizia kwa kasi kidogo wakasema Mheshimiwa, *EURA* ndio wamepanga hivyo.

Sisi ni wateja wa *TANESCO* hiyo *EURA*, sijui na nani nadhani ni ya huko huko. Hapa masuala ya kisiasa, Waziri Kiongozi alikwenda tukapata afuweni, lakini Waziri Kiongozi *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ampeleke juu zaidi ya hapo alipo tudumu na hilo la kisiasa siasa, vyenginevyo litakuja kiukweli ukweli. Barua inasema kama mmeridhika, hamjaridhika nendeni *EURA*, ndivyo alivyotwambia Mhe. Naibu hapa.
Hiyo kasema mwenyewe, barua yenyewe inakejeli kejeli hivi ndani. Hiyo ni watoto nyoka yuaja. Suala la kuwa na mbadala tegemezi kuliko hapa tulipo sasa. Sherehe tumeshereheka, tunapata umeme Pemba kutoka Tanga, lakini wenye sura hii deni imeshafikia shilingi 29 elfu sijui kama tutalipa, uwezo huo hatuna. Hili linaonekana kwa sababu liko huku kwetu, yetu sisi ya miaka 45 hayasemwi ng'o wala hayatajwi, wala hawataki kuyasikia. Tuna mpango gani wa hili?

Hapa ndipo ninapomshauri Mhe. Waziri Kiongozi swahiba wangu mpenzi katika safari yake hebu achukue kidogo japo wawili tu wanatosha kukusaidia. Kwa sababu uso umeumbwa na haya. Mhe. Spika, mimi nasema kwa nia safi kabisa najua hilo. Anaposimama Mhe. Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Mizengo Peter Pinda na Mhe. Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akakaa mbele yake kidogo tabu. Hawa watu wanakaribiana na mnasaba unafanana fanana. Nyuso zimeumbwa na haya Mhe. Spika.

Lakini Mhe. Mohammed Ali Salim hajawahi kukutana na Mhe. Waziri Mkuu kidogo ni mgeni naye, yale tutakayomtuma ataweza kuyasema kama tulivyomtuma yeye. Mheshimiwa yeye atazungumza ile lugha ya kule kule. Hapo ndipo nilipo mimi. Nakuomba Mhe. Waziri Kiongozi hebu, sijui muda utaruhusu uliobaki, kwa sababu mambo ndio hivyo. Lakini *Inshaallah* kwa hivyo nilivyosema pengine awamu ijayo ama upo hapo au uko zaidi, nadhani hili utalikumbuka tukatatue kero hasa.

Kwa sababu kero za Wazanzibari zilizotiwa saini juzi ni *very micro,* kuna *macro* ni hizi za uchumi. Tunahitaji hapa tukwamuke ili hizi nyimbo za kiuchumi ziwe zinasogea mbele si kurudi nyuma.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache sana, zumari zimeshasemwa sana zimeshapigwa, tarumbeta kaipiga vizuri Mhe. Abass Juma Muhunzi namshukuru, kanifilisi mengi niliyokuwanayo. Nakushukuru kwa kunipa hii nafasi ahsante sana.

**Mhe. Suleiman Hemed Khamis:** Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kunipatia nafasi japo kuwa fupi ya kuweza kuzungumza katika suala zima la bajeti.

Mhe. Spika, bajeti tunaijua sote kwamba huu ni mkusanyiko wa mapato ya ndani na vile vile ya nje, ambayo mapato haya tukishayapata tunazigaia wizara zetu na sekta nyengine katika matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

Lakini Mhe. Spika, tunaangalia kwamba bajeti ni lazima ichunguzwe. Hawezi mtu kujifanyia bajeti tu bila ya kuchunguzwa, halafu ni lazima iidhinishwe iwe ya halali kabisa kabla ya kugawiwa katika wizara mbali mbali. Sasa hatujui kama bajeit hii inachunguzwa au haichunguzwi inafanywa hivyo hivyo tu, kama inaidhinishwa au haiidhinishwi sawa sawa, au kwa tamko la mtu mmoja tu linatosha. Hatujui hayo hatujaelezwa.

Vile vile katika bajeti kuna suala zima muhimu ambalo lijumuishe mambo yote muhimu, ambayo haya yataweza kutoa kipaumbele. Lakini sasa katika mtiririko mzima wa bajeti hatuelewi kwamba kuna *priorities* zinatolewa, au kuna sehemu muhimi kunaangaliwa kwenye bajeti ile. Je, kipaumbele kwa mambo yaliyokuwa muhimu kinatolewa au inapangwa tu hii bajeti bila ya kuangalia vipaumbele vya bajeti ile?

Pamoja na hayo tunajua kwamba ni lazima bajeti ile iangalie sera, sera ambayo ni muhimu itaweza kutufikisha mahala pazuri. Sera ile bila shaka itakuwa inalenga kwenye malengo ambayo iliwekewa kwenye sera ile. Sasa hapa hatukuelezwa kwamba sera ile imekwenda sambamba na malengo ambayo yamepangwa.

Vile vile tunajua katika bajeti ni lazima isimamiwe, usimamizi lazima upatikane kuangalia yale matumizi ya katika bajeti je, yamesimamiwa vizuri? Je, usimamizi huu umekuwa thabiti kabisa? Hayo vile vile hatukuelezwa wala hatuyajui kama kweli inasimamiwa vizuri. Kwa sababu hili ni suala muhimu sana la kusimamia bajeti, usimamizi lazima uwepo kwa sababu hii ni *public expenditure.*

Kama hii ni *public expenditure* ni lazima usimamizi uwepo na kuoneshwa maelezo kwamba katika bajeti yetu hii usimamizi ulikuwa mzuri na hakuna kasoro zozote zilizojitokeza. Lakini kwa mazungumzo ya hapa ya katika Baraza imeonesha kwamba pia kuna wasi wasi wa kwamba usimamizi wa hii bajeti yetu haujawa mzuri sana.

Lakini Mhe. Spika, kuna mengine ambayo ni muhimu. Tulikuwa tunaifikiria hii bajeti yenyewe kwa jumla, kwamba itashughulikia rasilimali zilizomo ndani ya nchi yetu. Rasilimali hizi tunajua tuna rasilimali bahari ambayo ndani yake ni uvuvi. Tuna rasilimali ardhi ambayo ndani yake ni kilimo, tuna rasilimali watu ambao ndani yake ni wataalamu. Sasa tunaelewa kwamba katika uvuvi kitu kadhaa kinahitajika, katika kilimo kitu kadhaa kinahiutajika.

Lakini katika suala la mwisho la rasiliamli watu hili ni suala muhimu sana. sasa hatujui hapa katika bajeti hii nikiasi gani rasilimali watu wameweza kutumiwa vizuri hao watu. Kwa sababu bila ya kupata hawa rasilimali watu ambao ni wataalamu, hawa ndio wanaoweka mipango yote mizuri. Sasa sijui kama watu hawa rasilimali wataalamu wametumiliwa kiasi gani kwa suala hili.
Kwa sababu hawa wataalamu ni lazima wakubali kupokea changamoto zote na kuzifanyia kazi ambayo ni ngumu sana na kuweza kutoa ile *thinking power* yao. Hawa wataalamu ni watu muhimu sana. Sasa katika kujenga bajeti ni lazima tuwatumie hawa wataalamu na wakubali kuitumikia kila sehemu. Sasa hapa ni suala muhimu vile vile, hatuelewi wametumika kiasi gani.

Halafu kuna suala muhimu katika bajeti hii vile vile. Kuna suala ambalo tunatakiwa wananchi wajuilishwe jinsi fedha ilivyotumika kwenye rasilimali hizo. Hatukuelezwa wala hatukuambiwa kiasi gani watu wameelezwa katika masuala haya.

Pia kuna suala zima la utekelezaji. Katika utekelezaji ni lazima tueleze kwamba matumizi ya bajeti yetu katika rasilimali hizo zimekwenda vizuri na ubora wake utakuwa hivi, huduma zake zitakuwa hivi, *time bound* itakuwa hii katika kila rasilimali. Hayo vile vile hatukuambiwa.

Mhe. Spika, baada ya hayo niendelee katika masuala ambayo tunataka tujifunze kidogo kwamba tuna matatizo katika nchi hii ya suala zima la ajira. Ajira ni

matatizo makubwa sana katika nchi yetu pamoja na tathmini iliyotolewa, lakini kuna vijana wengi bado hawajapata kazi.

Mimi kwa fikra zangu ni kwamba, kama tutaangalia historia ya nyuma ya karne zilizopita katika sehemu za nchi za Europe. Utakuta katika karne za 18-19 kulikuwa na jitihada kubwa sana ya kutafuta rasilimali au mali ghafi kwa ajili ya viwanda. Tumeona nchi bila ya kuwa na kiwanda bado haijaweza kuwanufaisha wananchi wake na hili ni tatizo kubwa.

Huko Europe baada ya kupatikana viwanda kadhaa wa kadhaa, nchi mbali mbali ndio maendeleo ya nchi yalivyopatikana. Sasa sisi hapa kwetu Zanzibar suala la viwanda bado linapigwa chenga, halijawa na msimamo, halijawa na *seriousness* katika suala hii. Hii kama viwanda vitapatikana kwa wingi hapa Zanzibar vitaweza kutusaidia kutukomboa kwa vijana wetu kuweza kupata ajira. Hatuna namna ya kuwasaidia vijana hawa zaidi ya kuweka viwanda, viwanda ndivyo vitakavyoweza kutusaidia, lakini mpaka sasa hivi hivyo viwanda vilivyopo ni vidogo, havitoshelezi kwa hivyo vijana wetu wanakosa nafasi za kazi.

Kwa hivyo, hili ni suala ambalo linaonesha kuwa viwanda hapa petu bado mpaka sasa vimeshindikana havijapewa kipaumbele. Na sisi tulisema katika *priorities* viwanda ni lazima vipewe kipaumbele. Kwa hivyo, hapa wizara haikutoa kipaumbele kikubwa sana kwenye viwanda. Kwa sababu kama tutakuwa na viwanda bila shaka tutaongeza pato la nchi, litapatikana na uzalishaji utakaopatikana utaweza kusaidia ndani ya nchi na vile vile tutaweza kusafirisha nje ya nchi ili kuweza kupata dola au *foreign money.*

Kwa hivyo, kama hatuna viwanda hii *foreign money* tutaipata wapi na hatuna viwanda? Kwa hivyo, tutakapozalisha vizuri na mali yetu ikawa safi kabisa yenye ubora mzuri tutaweza kupata ile akiba ambayo tunaihitajia sisi kuwa nao kwa ajili ya kununua vingine ambavyo sisi hatuna.

Katika viwanda vyetu hatuna ubora wa usafirishaji wa vitu, vitu vyetu tunapeleka hapa hapa ambapo haitusaidii kuweza kuweza kuchuma hii pesa ya kigeni.

Mimi naona kubwa zaidi ambalo bado wizara inahitaji kuwa na msimamo mzuri katika masuala ya viwanda ni kwamba serikali ijaribu kutafuta wawekezaji wa ndani na wa nje waweze kusaidia, kama serikali haina uwezo wa kulitanua suala hili. Kwa hivyo, nafikiri wawekezaji wanaweza kutusaidia katika mambo haya na kuweka vitega uchumi kadhaa wa kadhaa.

Mhe. Spika, hapa katika suala hili kama tunataka tulifanikishe sawasawa ni lazima watu wetu ambao watajikubalisha kuweka viwanda wasaidiwe kupata mikopo, mikopo ambayo itawasaidia kuweza kutanua katika viwanda vyao. Lakini leo iko wapi mikopo, benki gani iko tayari kuwapa fedha kitita kilichokuwa kingi cha kuweza kufanya viwanda. Utakuta watu wetu wanashindwa kwa hayo. Benki zetu ni nyingi lakini ni *branch* tu, lakini hazina uwezo wa kutusaidia sisi kuweza kufanikisha masuala yetu ya kufungua viwanda.

Mhe. Spika, kwa masuala mengine ya kibishara tunaiona hali ya kibiashara Zanzibar ilivyo, na bado mimi nasema ni *competition* kubwa sana. Mimi nataka nilinganishe, baina ya biashara tuliyonayo hapa ambayo havizalishwi vitu katika viwanda vyetu, ni vitu ambavyo vinazalishwa nje vinaletwa Zanzibar.

Tukiangalia mwananchi anavyopata shida, yeye analima lakini kilimo anacholima kinamsaidia yeye tu kidogo. Lakini ni lazima awe na fedha kuweza kununua vitu ambavyo vinatengenezwa nje ya viwanda vyetu ambavyo vinaletwa hapa Zanzibar. Kwa hivyo, utakuta bado watu wetu kutokana na masuala mengine wanashindwa kununua vitu kwa sababu ya vitu hivi bado mfumko wa bei ni mkubwa sana, vitu wanaviona madukani, lakini uwezo wa kununua hawana wanashindwa.

Kwa sababu hapa yeye analeta vyakula vyake sokoni anauza kwa bei rahisi, lakini anatakiwa pewa ile ile akaitumie madukani ambapo uwezo wake wa kununua vitu vile ni mdogo. Kwa hivyo, hili ni suala la kuzingatia kwenye viwanda.

Biashara yetu ndio halikadhalika, inaonekana ni namna hiyo na wale wafanyabiashara wakubwa wakubwa utawaona na wao kutokana na hali ya biashara inavyozoofika hapa, watu wetu wengi wanaondoka wanakwenda sehemu nyengine.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka niligusie kwenye hizi *priorities* niingie katika uvuvi. Uvuvi ni moja katika shughuli zetu za hapa Zanzibar tukitaka, tusitake. Sisi kazi yetu kubwa ni ukulima, kazi yetu ya pili ni uvuvi. Lakini suala la wizara yetu kuweza kuyakiuka mambo mawili haya kilimo na uvuvi na ikawa haikupewa nyenzo na fedha za kutosha au wawekezaji wakaletwa hili ni suala ambalo linazoofisha nchi hii. Kwa hivyo, utakuta uvuvi ni kazi yetu, ni amali yetu na tumekubali kuachana na ile *traditional fishing* (uvuvi wa kale), uvuvi wa kutegemea mishipi au mdogo mdogo wa kusambaza sambaza pwani pwani kwenye *shell waters.*

Mhe. Spika, hili suala naona bado halijapewa kipaumbele, tunahitaji sasa hivi kuondoka katika uvuvi ule ambao uvuvi huu ulikuwa ni wa kipato kidogo, tunataka tuingie katika uvuvi ambao utakaotupa kipato kikubwa. Sasa tutafanya vipi hata tuingie katika kipato kikubwa kwa wananchi wetu? Nani atakayetupa? Tutapewa na nani misaada hiyo kama si wizara hii kuchachamaa kwa kuhakikisha kwamba wizara inajikita zaidi kwenye mambo ya uvuvi.

Nafikiri tunajua hapa kipindi kilichopita, tulikuwa na Mkurugenzi hapa, akatoa semina, akatoa maelekezo yake ya uvuvi, aielekeza ile bahari nzima tukaiona kama na sisi ni wavuvi. Akatueleza katika bahari hii kuna mambo mazuri sana katika bahari, kuna uvuvi na kuna mambo ya kuvutia ndani ya bahari. Idara yake imeshatoa maelezo kwamba, wavuvi wanatakiwa kuna maeneo maalum wasivue. Kuna nyavu maalum wasivulie ambazo zamani ndio walikuwa wakirambaza wakipata hivyo hivyo, mama kanipa mzima wanakuja nao wanauza.

Sasa kama hali itakuwa hiyo, kwa upande mmoja wa Idara ya Uvuvi inawaeleza wananchi kwamba haya yasitendeke ni nani mwengine atakaewasaidia hao wavuvi ili kuweza kuingia katika bahari kuu?

Mhe. Spika, suala la kuingia katika bahari kuu ama itakuwa ni wizara, itafute wawekezaji wakubwa, wazito watakaokubali kuingia katika bahari yetu wakazalisha, tukapata samaki wa kutosha kwa ajili ya chakula chetu. Vile vile tukapata samaki wa ziada kwa kuongeza kiwanda cha pili, badala ya vile viwanda vilivyoko katika ardhi  na viwanda vyengine vya baharini ambavyo ni vya kusindika samaki, haya yako wapi? Suala hili ni la muda mrefu sasa hivi tuko hapa ni miaka mingi bado tumeshindwa kuweka viwanda vya kusindikia samaki. Jambo ambalo tungeweza kupata *capital income* ya *foreign* ambayo ingeweza kutusaidia kununua vifaa vya majenzi nje, kwa sababu sisi hatuna mambo hayo. Kwa hivyo nafikiria katika masuala haya, wizara ingejikita zaidi kwenye mambo ya uvuvi na mambo ya kilimo. Hizi ni sekta mbili kubwa na ni muhimu na kipaumbele chote kingewekwa pale.

Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba mpaka hivi sasa inavyoonesha kwamba hiyo kilimo yenyewe inapewa asilimia 6 na huo uvuvi wenyewe haujapewa chochote. Sasa tunakwenda wapi? Tutanyanyua vipi uchumi wa nchi yetu? Watu wetu hali zao zitakuwa vipi ? Na  sasa hivi tunataka kuzifanya hali zao ziwe bora zaidi, *capital* hatuna! Basi tuwashawishi watu waweze kuja katika nchi yetu, ili waweze kutusaidia.

Mhe. Spika, niingie katika suala hili la kilimo sasa. Kwa kweli Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba kilimo ndio uti mgongo wa wa uchumi wa nchi yetu, kilimo ndio kinachotusaidia sisi angalau ku-*survive* katika nchi hii.

Mhe. Spika, vile vile kilimo ni sekta kuu ya nchi yetu hii na tunaitegemea kwa mambo yote ya uzalishaji na ni sekta muhimu, baada ya sekta hii ya kilimo na sekta ya utalii ambayo sisi sasa hivi tunaitegemea sana sekta hii ya utalii, na pengine kipaumbele chake kinakwenda zaidi kwenye utalii kuliko katika kilimo. Ndio wanasema kwamba katika mgao wa fedha inapewa asilimia 6 haitoshi, kweli tunaweza tukajikomboa kwa asilimia 6 ni ndogo sana.

Mimi katika mazungumzo yangu nilitaka waziri angetoa kitu kama *comparison* hivi, hali halisi tulivyokuwa katika kipindi kilichopita na hali halisi tulivyo hivi sasa, tuone ni kiasi gani kilimo kimepiga hatua, yaani tulinganishe kipindi kilichopita na kipindi hiki ambacho tunaingia hivi sasa. Tuone kama kipindi kile kilichopita tulikuwa na eka kadhaa tuliweza kuzifanikisha kutokana na idadi ya matrekta 45 tuliyopewa kwa ajili ya kilimo na tukaona je tukiongezewa hapo tutaweza kupiga hatua zaidi.

Vile vile ilikuwa tuone kama ikiwa vifaa vilivyoletwa kwa ajili ya kilimo je, vimeweza kufanya kazi kwa maeneo yote ambayo yako wazi ya kilimo. Kwa sababu hatujui mpaka sasa hivi pengine kuna maeneo ya wazi bado hayajatumiliwa, yako hivi hivi. Sasa haina maana kusema kwamba tuna matrekta 45 tuliyopewa kwa ajili ya kilimo. mengine yamegaiwa yamepelekwa Pemba na mengine yamebakia hapa. Lakini tuone ni kiasi gani matrekta yale yameweza kusaidia katika ukulima wa umwagiliaji maji, mbali ya vibonde Bubwi hivyo hatuvitii katika hesabu sana, ingawa vina asilimia lakini ni ndogo sana. Zaidi tunategemea uzalishaji mkubwa wa kilimo kwa njia ya trekta pamoja na udogo wa ardhi yetu tulionayo.

Lakini hapa Mhe. Waziri hakutueleza ni kwa kiasi gani matrekta hayo yameweza kufanyakazi ya kilimo kwenye maeneo kadhaa na kuna maeneo kadhaa bado yamebakia hayajafanyiwa kazi, hiyo taarifa hatuna. Kwa hivyo, hiyo nayo ilikuwa tupate taarifa ili tujuwe kuwa je, tuongeze matrekta zaidi au kuna matatizo wananchi bado hawajaitikia suala la kilimo na kama hawajaitikia suala la kilimo kuna lipi ambalo linaweza likasaidia serikali.

Vile vile katika kulima tumeweza kujua kwamba katika kulima unapata matatizo ya kilimo. Kuna hawa wadudu ambao wanaleta athari ya kilimo. Ilikuwa tuelezwe kwamba katika kipindi kilichopita bahati nzuri kilimo chetu kimekwenda vizuri wala athari haikupatikana, hatukuelezwa habari hizo. Au kama ilikuwa maradhi yalitokezea basi ilikuwa tuelezwe kwamba mipunga imeathirika kwa kiasi kadhaa.
Mhe. Spika, halafu nakumbuka kwamba katika kukifanya bora hiki kilimo chetu cha Unguja ni kwamba palitolewa mipunga ya aina mbali mbali, ambapo mipunga hiyo uzalishaji wake unakwenda juu sana, yaani unampa mkulima kipato kikubwa kuliko ule utamaduni wetu wa zamani wa ile aina ya mpunga

ambayo tulikuwa tukilima kale uzalishaji wake ulikuwa ni mdogo. Taarifa hizi hatuna, hatujaambiwa katika mbegu zaidi ya mia zilizoletwa na mafanikio yake yamepatikana na ukulima umekuwa hivi na hivi. Kwa hivyo, hayo ni mambo ambayo ilikuwa tuelezwe katika aina za mpunga.

Mhe. Spika, kama waziri kidogo angeweza kutueleza mafanikio ambayo yameweza kupatikana katika suala zima la kilimo, tukaweza kutoa tofauti kwamba kipindi kilichopita tulizalisha tani kadhaa na tumepunguza uagiziaji tani kadhaa. Kwa hivyo hili hatukuambiwa, kwamba kipindi kile uzalishaji ulikuwa hivi na uagiziaji ulikuwa hivi. Kwa hivyo, tume-*minimize* uagiziaji kutokana na uzalishaji ulivyokua mzuri, taarifa hii hatunayo. Sijui kama zipo lakini inawezekana mimi sijaziona au sikuzisoma.

Mhe. Spika, kama ikiwa hili suala zima la ukulima wetu wa Zanzibar halikupewa kipaumbele na ustawi ukawa mzuri sana wa kilimo, basi ndio yale yale tunayoyakimbia yanaweza yakaingia, nayo ni yapi, ni mfumko wa bei. Kwa nini ukaingia mfumko wa bei. Mfumko wa bei unakuja kutokana na hali duni za uzalishaji wa kilimo, matokeo yake vitu vilivyomo ndani ya maduka wanavipandisha juu kwa sababu wanajua huku hakuna kitu na watu wote wanaelemea kwenye maduka. Sasa hapa mfumko wa bei unakuja juu sana.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mkulima ambaye na yeye angefaidika, basi hapa hawezi kufaidika kwa sababu yeye hana kitu anacholeta au ni kidogo hakitoshelezi, kwa hivyo anategemea vile vilivyomo madukani na vilivyomo madukani ndio wameshajua kwamba hali ya kilimo ni dhaifu, kwa hivyo na wao wanapandisha vitu bei. Suala hili la kupandisha vitu bei vinapandishwa kiholela na watu wanapiga kelele kwamba bei ya vitu bado iko juu, ingawa huku inaelezwa kwamba mfumko wa bei unateremka chini. Mimi siamini kama unateremka chini, mimi naona unakwenda juu hasa, hawakubali wafanyabiashara. Kwa hivyo, kama yeye anataka kutueleza juu ya suala zima la mfumko wa bei, kwa kiasi fulani angeweza kutuambia *percentage wise.* Mfumko wa bei umepanda juu kwa asilimia fulani na umeteremka kwa asilimia fulani ili tukaweza kujua.

Halafu katika masuala mazima ya kilimo, hatukupata maelezo ya kuonesha nini fikra za wakulima wanaishauri nini serikali iendelee, isiendelee au kuna matatizo fulani wanahitaji wakulima ili uzalishaji uwe mzuri zaidi. Kwa hivyo, ningemwambia Mhe. Waziri kwamba aje atueleze kidogo hapa kwamba kweli amepata ushauri wa wakulima na wametoa mawazo yao na fikra zao.

Vile vile tulitaka kujua kuwa hiki kilimo kama kiliendeshwa vizuri, hiki kipato cha huyu mkulima kimeongezeka kwa kiasi gani, ili tuweze kujua kama kweli hapa imepatikama *improvement* ya kilimo. Kwa hivyo, tuweze kujua pale yule

mkulima amenyanyuka juu kwa kiasi fulani. Mimi nafikiri kwa ufupi tu kwenye suala hili, mgao huu mimi sikuridhiana nao katika kilimo, kama ni sekta muhimu basi ilikuwa hii ipate fedha nyingi zaidi ya kuweza kuendeleza mambo yake.

Mhe. Spika, ninalotaka kuzungumza sasa hivi ni suala zima la (*CDF)* yaani *Constituency Development Fund.* Mhe. Spika, hili ni suala muhimu sana na mimi namshukuru Mhe. Waziri kuwa hili suala tayari amekwishalitamka na tuna mategemeo nalo kwamba litaweza kutusaidia. Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, sasa huu Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ni mzuri sana. Bila shaka nchi katika kuangalia maendeleo, unaweza kuona nchi za jirani zinafanya nini basi na wewe ukaweza kuiga, kwa sababu hakuna ubaya kuiga kitu kizuri. Kwa hivyo, tumeona hapa kwetu Tanzania na tumeona kwa jirani zetu wa Kenya. Kwa kweli kwa miaka yao yote ya maendeleo ya nchi ya Kenya, haikuwa namna ya kuwasaidia wananchi wake zaidi ya mafanikio ya *CDF*, hii imewasaidia pakubwa sana na maendeleo wao wanashukuru kwa kipindi ambacho wameweka mfuko huu basi wamejisikia wananchi kwamba sasa serikali inatusaidia.

Kwa hivyo, na mimi natilia mkazo kwamba kweli kama wizara hii ina nia ya kuweka huu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii katika Majimbo, *it is only thing* hakuna namna nyengine. Kwa sababu na sisi wawakilishi tunabanwa mpaka koo, niamini mimi. Siku unayoteremka tu pale watu wamekukusanyikia kweli, huyu ana shida hizi na huyu ana shida hizi. Kwa hivyo, mimi nafikiri mfuko huu ni muhimu sana kama tutaupata basi tutasaidia kupunguza baadhi ya matatizo na bila shaka kama kutakuwa na kamati ya maendeleo ya jimbo basi itaweza kutusaidia ili kuweza kufanikisha masuala yetu.

Mhe. Spika, la mwisho kama wakati upo, au muda umekwisha.

**Mhe. Spika:** Malizia la mwisho.

**Mhe. Suleiman Hemed Khamis:** Ahsante sana. Mhe. Spika, baada ya hiyo *CDF*, nimalizie kwa suala la mwisho, ni kuhusu *income* ya nchi hii, ambapo *income* ya nchi hii *traditional* ni suala la karafuu. Lakini mimi ni jambo ambalo linanisikitisha kwamba hii *traditional* karafuu ndio zao la asili la kale la nchi hii ambalo hili ndio lililokuwa likitusaidia Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nakumbuka katika kila senti mia moja za mapato basi senti themanini zilikuwa zinatoka katika karafuu. Mimi nastaajabu kuwa leo zao lile limetupwa, hakuna *initiative* yoyote inayofanywa, watu wanajifanyia kiholela, hakuna utaratibu wowote wala hakuna msisimko wa suala lile. Tangu tulikuwa tukizalisha matani kwa matani mpaka sasa hivi tunazalisha tani tatu mpaka tani

tatu na nusu. Ni aibu kwa nchi hii kuambiwa kwamba nchi ya Unguja au visiwa vya Unguja vinazalisha tani tatu za karafuu.

Kwa hivyo, zao hili tukitaka tusitake kama wizara haijatilia mkazo kwenye suala hili basi pia tunakosa yale mapato ambayo ni pesa za kigeni. Tunauza karafuu nje tunapata pesa za kigeni, basi pesa za kigeni zile tutakazo zipata tunaweza tukaagizia vitu ambavyo ndani ya nchi yetu hakuna. Lakini leo lile zao tumelitupa na matokeo yake *graph* ya karafuu inazidi kuteremka chini zaidi.

Kwa hivyo, ningemshauri Mhe. Waziri pamoja na yote kuweza kutilia mkazo kwa siku za mbele, kuweza kusimamiwa vizuri katika utekelezaji wake ili mikarafuu ikapandwa kwa wingi na uzalishaji ukawa mzuri *Alhamdullilah.*

Sasa jengine lililobakia ninasikitika kulizungumza ni suala la mwani. Suala la mwani bila shaka linasaidia nchi hii. Lakini suala hili bado kutokana na taarifa ya Mkurugenzi wa Uvuvi, tayari amekwisha kuwawekea kizuizi hawa wakulima, kwa sababu zamani hawa wakuliwa walikuwa wanalima mwani wao kwenye maji ambayo ni haba ndio wanazalisha ule mwani wao. Lakini sasa hivi kwa mujibu wa mazungumzo ya Mkurugenzi ni kwamba suala hili sasa hivi haliwezi likafanyika hapo, mpaka waende wakafanye shughuli za kilimo katika *deep sea*. Jamani mimi hapa sijui waziri atakuja kuzungumza vipi kwenye suala hili.

Kwa sababu mwani unatusaidia kupata fedha za kigeni vile vile tunauza nje tunapata fedha na tunaingiza ndani na fedha ile ile inatusaidia. Sasa ikiwa leo wale wakulima kwa sababu za kuhifadhi mazingira. Kwa sababu wanasema huu mwani unaolimwa pwani unachafua mazingira ya pwani. Kwa hivyo, kama inachafua mazingira ya pwani ya pale mwanzo kwenye *costal area* wapelekwe huko kwenye maji mengi. Je, huu utaratibu una maandalizi yake yakoje au hao wanawake kweli wataweza kwenda kulima huo mwani katika *deep sea*.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kutoa maelezo yangu kuhusu suala hili.

**Muhyddin Moh'd Muhyddin:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili kuzungumza machache sana kwenye bajeti hii kuu ya serikali. Mhe. Spika, mengi yameshazungumzwa na wajumbe waliotangulia kuhusiana na kuiboresha au kuifanya bora bajeti hii ya serikali kwa manufaa ya watu wetu.

Mhe. Spika, mimi nitaanza na ujenzi wa barabara sita za Kusini. Naomba nichukuwe nafasi hii kwanza Mhe. Spika, kuishukuru sana serikali kwa kuwezesha ujenzi wa barabara hizi kuweza kuendelea. Kwa sababu ilikuwa

uwezekano wa kujengwa kwa barabara hizi ulikuwa umeshatoweka kabisa, baada ya zile fedha ambazo zilitengwa na kuhamishiwa kwenye mradi wa umeme. Lakini serikali ilikwenda mbio mpaka ikaweza kufanikiwa kupata fedha nyengine kutoka kwa hawa hawa wafadhili ili ujenzi wa barabara hizi sita uweze kuendelea.

Kwa bahati nzuri sana Mhe. Spika, ujenzi wa barabara hizi umeanza katika Jimbo la Mtambile. Ilianza barabara ya Mtambile Mwambe na baadae ikafuatia barabara ya Mtambile Kangani.

Mhe. Spika, lakini katika ujenzi wa barabara hizi, sasa hivi kunatumika utaalamu mpya katika ujenzi wa barabara hasa hii ya mwanzo niliyoitaja ya Mtambile Mwambe. Miongoni mwa vifaa vinavyotumika ni saruji na mambo mengine. Kwa hivyo, nilikuwa nina hamu sana ya kupata hii nafasi, kwa sababu sijui kwenye wizara ya mawasiliano kama nitakuja kupata nafasi ili nimwambie Mhe. Waziri kwamba katika matumizi ya vifaa hivi vinavyotumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii ya Mtambile Mwambe, kuna ubadhirifu mkubwa wa vifaa. Hasa vifaa hivi vya saruji pamoja na *diesel*, maana yake mambo yanafanywa wazi wazi mpaka wananchi wenyewe wanaona. Wananchi wamepatwa na wasi wasi kwamba huwenda ama barabara ile isikamilike kwa sababu vifaa itakuwa vimekwisha au itakamilika lakini katika kiwango cha chini kabisa. Kwa hivyo, ninamuomba sana Mhe. Waziri suala hili alifuatilie ili kuinusuru hilo.

Jengine Mhe. Spika, katika ujenzi wa barabara hizi, tunashukuru kwamba na wananchi wanapata ajira japo ya muda mfupi lakini inawasaidia. Halafu popote pale panapofanywa kitendo cha maendeleo hutokea matatizo, kwa sababu katika utayarishaji wa ujenzi wa barabara hizi kuna vipando vya wananchi vilivyo athirika. Sasa wananchi wa maeneo hayo wanataka kujua ni nini hatima ya vipando vyao vile vilivyo haribiwa. Je, watafidiwa na kama watafidiwa basi fidia hiyo italipwa lini? Suala hili wamenisisitiza nimuulize Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kuhusiana na fidia ya vipando vyao vilivyoathirika katika utayarishaji wa ujenzi wa barabara hizi.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumzia katika bajeti hii ni mikopo kwa sekta binafsi kwenye kitabu hiki imeelezwa katika kifungu cha 59 na kwenye kitabu kile cha mpango kimeelezwa katika kifungu cha 5(2) ukurasa wa 27. Mhe. Spika, tunashukuru kwamba mikopo imeongezeka kwa sekta binafsi lakini masikitiko yetu ni kwamba ili kuweza kukuza uchumi ni budi kuzalisha, ili uzalishe kwa matumizi ya ndani na halikadhalika kwa kusafirisha nje. Kwanza ukisafirisha nje utaweza kupunguza lile lililomtisha Mhe. Thuwaybah la nakisi ya urari wa biashara, kwa sababu kila ukisafirisha zaidi na ukiagiza kidogo ile nakisi inapungua. Sasa tumeona kuwa nakisi ya urari wa

biashara kila mwaka inaongezeka ili kwa sababu usafirishaji wetu ni mdogo kuliko uagizishaji kutoka nje ama Tanzania Bara au nje ya Tanzania.

Kwa hivyo, ili tuweze kusafirisha ni lazima tuwawezeshe wazalishaji katika sekta ya kilimo na katika sekta ya viwanda. Sasa katika sekta ya kilimo kuna mambo mawili Mhe. Spika, kuna kilimo hiki cha juu na kuna kilimo cha baharini. Sasa wazalishaji katika kilimo cha juu halikadhalika na cha baharini, kwa sababu baharini kuna uzalishaji wa aina mbili. Kwanza kuna hili alilomalizia Mhe. Suleiman Hemed la mwani. Sasa wazalishaji wa mwani sikuona kwamba wamewezeshwa katika mikopo hii iliyotolewa na hayo mabenki. Halikadhalika na wavuvi nao hawakuwezeshwa kuweza kufanya shughuli zao za uvuvi katika bahari kuu. Hao waliowezeshwa kwa kupewa hayo maboti pamoja na nyavu ni wavuvi wa dagaa, sasa dagaa litatusaidia kwa kula hapa hapa ndani hatuwezi kusafirisha dagaa, ili tuweze kusafirisha ni lazima tupate minofu ya samaki na minofu ya samaki Mhe. Spika, yanapatikana hapo tutakapokwenda kwenye bahari kuu. Sasa sijui Mhe. Waziri atatueleza nini kuhusiana na kuwezeshwa hao wavuvi wanaoingia katika bahari kuuu, halikadhalika na waoteshaji wa mwani.

Jengine Mhe. Spika, kwenye kilimo tuna zao letu kubwa la biashara nalo ni karafuu. Kwa kweli Mhe. Spika, naweza kusema kwamba serikali imelipuuza zao hili la karafuu kwa sababu kutenga milioni 80 kusaidia katika uendelezaji wa mikarafuu ni dhihaka tupu. Kwa sababu mikarafuu Mhe. Spika, imo katika visiwa vyote viwili vya Unguja na Pemba. Sasa na hali ya karafuu kama tulivyoona, uzalishaji wake umeanguka sana kutoka miaka ya 1960 tani 16,000 mpaka sasa hivi tunazalisha tani 2,500 mpaka tani 3,000 kwa mwaka.

Sasa hali hii kwa kweli Mhe. Spika, ni mbaya mno na serikali ilikuwa ikae kitako ilifikirie ili iweze kuwawezesha wazalishaji karafuu, ili kuyaendeleza mashamba yao ya karafuu kwa ajili ya kupata uzazi wa karafuu ulio bora ambao utaweza kuongeza uzalishaji wa karafuu na kwa hivyo kuweza kusafirisha nje zaidi. Pamoja na kwamba bei ya soko la karafuu katika soko la ulimwengu imeteremka, lakini ukisafirisha kwa wingi kile kipato kinaongezeka vile vile Mhe. Spika. Sasa kama huwezi kusafirisha kwa wingi, ili tuweze kusafirisha kwa wingi ni budi kuona kwamba tunazalisha karafuu kwa wingi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, Mhe. Waziri ilikuwa kuna haja kubwa zaidi kuliangalia suala hili la kuwawezesha wazalishaji katika kilimo hiki cha juu pamoja na kilimo cha baharini. Halikadhalika Mhe. Spika, sikuona vile vile katika mikopo hiyo iliyotolewa kuwawezesha wawekezaji wa viwanda, kwa sababu na kwenye viwanda nako kunazalishwa kwa ajili ya matumizi ya ndani, halikadhalika na ziada ya kuweza kusafirishwa nje.

Mhe. Spika, ni bahati mbaya sana kwamba suala hili la viwanda katika nchi yetu lina matatizo makubwa, kwa sababu viwanda vinaanzishwa lakini baada ya muda mfupi viwanda vile vinalala havizaliswi tena. Nakumbuka hapa kulikuwa kuna viwanda vidogo vidogo Sebleni vilikuwa vikifanya kazi nzuri sana Mhe. Spika, lakini viwanda vile leo havipo. Kulikuwa kuna kiwanda cha nguo lakini sasa kiwanda kile hakipo na viwanda vingine. Sasa sijui kuna haja ya wataalamu kufanya utafiti ni sababu zipi zinazopelekea viwanda vyetu vikawa haviendelei na vinaanguka katikati. Ilikuwa kuna haja hiyo ufanywe huo utatifi na kuweza kupatikana mbinu za kuweza kuviimarisha viwanda hivi na kuanzisha vingine kwa ajili ya kukuza uchumi wetu.

Kwa sababu tukizalisha kwenye viwanda vyetu na vile ambavyo huwa tunaagiza kutoka nje basi itakuwa hatuagizi tena na ziada tunaweza tukaisafirisha. Kwa sababu viwanda vidogo vidogo vilivyokuwepo Sebleni, vilikuwa vinatosheleza soko la ndani na halikadhalika vilikuwa vina safirisha. Kwa hivyo, viwanda havipo. Kiwanda cha Sigara cha Tabia Njema hata hakijulikani tena, kuna majengo tu magofu yaliyobakia. Sasa Mhe. Spika, nadhani na hapa wataalamu wetu wa kiuchumi na wengineo kuna haja ya kuyaangalia hayo na kuweza kutuletea ufumbuzi.

Mhe. Spika, jengine lililoelezwa kwenye bajeti hii na Mhe. Waziri ni kuboresha takwimu. Nadhani hili Mhe. Spika, ni suala muhimu sana, kwa sababu hao wachumi wetu wanaweza kutufanyia hii mipango kwa kutumia takwimu. Sasa takwimu kama haziko sahihi na mipango vile vile hatimaye itakuwa haiko sahihi. Ili waweze kutengeneza mipango mizuri wataalamu wetu wa kiuchumi hapana budi kupata takwimu zilizosahihi. Kwa hivyo, hili namuomba Mhe. Waziri kwa sababu kalitaja kwenye bajeti yake basi alipe kila msukumo na takwimu sahihi ziweze kupatikana kwa ajili ya matumizi ya wachumi wetu kututayarishia mipango iliyo bora.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusiana na wafanyakazi. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katueleza kwenye kitabu chake kwamba hivi sasa tuna wafanyakazi 45,551. miongoni mwa wafanyakazi hao, wafanyakazi 31,378 wako katika sekta ya umma na wafanyakazi 10,230 wako katika sekta binafsi. Sasa ukijumlisha wafanyakazi hao katika sekta mbili hizo unapata wafanyakazi 41,608. Sasa ukitoa kwenye ile idadi kubwa aliyotupa Mhe. Waziri unabakiwa na wafanyakazi 5,943.

Naomba kumuuliza Mhe. Waziri wafanyakazi hawa ambao kawajumlisha katika ile idadi ya ajira wako wapi, au wanafanyakazi ya siri hawa ndio hataki wajulikane walipo. Kwa sababu 31,000 wako katika sekta ya umma, 10,000 wako katika sekta binafsi. Sasa hawa wafanyakazi 5,943 wako wapi au hawa ndio wafanyakazi hewa ambao wanachukua pesa zetu halafu sisi tukakosa

kutumia fedha hizo kwa ajili ya mipango ya kuwaendeleza watu wetu. Naomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa aje atupe jibu ambalo litaturidhisha.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nataka nilizungumze kwa kumalizia muda wako ni suala la deni la mafao ya wastaafu. Amefanyakazi kubwa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kuweza kutatua tatizo hili la deni la wastaafu, lakini bado kuna bakaa iliyobakia ambayo wastaafu hawajalipwa. Je, namuuliza Mhe. Waziri hili deni lililobakia litachukua muda gani kulipwa kwa wastaafu hao waliobakia.

Halikadhalika kwa hawa hawa wastaafu kama walivyosema waliotangulia, Mhe. Waziri kakusudia kuongeza ile pencheni yao kutoka Shs.15,000 wanayoipata sasa mpaka kufikia Shs. 25,000. Si haba hiyo kuongezwa, kwa sababu Mtume (SAW) anasema usiposhukuru kwa kidogo ulichopata basi hata ukipewa kingi huwezi kushukuru. Kwa hivyo, na hili tunashukuru kwa kufuata kauli hiyo ya bwana Mtume (SAW), nadhani mwaka utakaofuatia watawaweza kupata hao wastaafu Shs. 60,000 au zaidi ya hapo. Kwa hivyo, tunashukuru sana kwa hilo.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, ni kwamba Mhe. Waziri katika mipango yake kuna milango miwili ya kupatia fedha kwa ajili ya kuendeleza mipango yetu. Kwanza fedha za ndani na fedha kutoka kwa wafadhili. Sasa Mhe. Spika, mwaka jana alipanga hivyo hivyo, lakini fedha zilizopatikana kutoka kwa wafadhili hazikufikia hata asilimia 50 na cha kushangaza ni kwamba mara hii kaongeza zaidi ya zile fedha anazotegemea kupata kutoka kwa wahisani. Sasa sijui ana mikakati gani ya kuweza kuonesha kwamba hizo fedha ataweza kuzipata. Au Mhe. Waziri anafanya kama ile hadithi aliyoikuta bwana Mtume (SAW) katika safari yake ya Miraji. Kwa sababu katika safari yake ya Miraji alipita pahala akamkuta mzee mmoja ana mzigo wa kuni anataka kuunyanyua kichwani, akaunyanyua mpaka ukafika mabegani haukufika kichwani, akaushusha akaongeza tena kumi.

**Mhe. Spika:** Malizia.

**Muhyddin Moh'd Muhyddin:** Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Hiyo hadithi waheshimiwa wameshaitambua, kwa hivyo wanakushukuru kwa hadithi hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe tutaendelea jioni ambapo katika orodha yangu kuna wachangiaji watatu ambao ni Mhe. Ali Haji Ali, Mhe. Machano Othman Said Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Mhe. Asha Moh'd Hilal. Makusudio ni kwamba uchangiaji tumalize jioni leo na kesho

tumuombe Mhe. Waziri atufanyie majumuisho kwa maswali mengi ambayo mmeyauliza.

Jioni kwa sababu nitakuwa na dharura kidogo Mhe. Mwenyekiti wetu Thuwaybah Edington Kisasi ataendelea na kikao. Baada ya hayo naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

*(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadilino yanaendelea)*

**Mhe. Zahra Ali Hamad:** Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa fursa alaasili ya leo na mimi kuchangia moja mpaka mawili ambayo nahisi niyazungumze. Mhe. Mwenyekiti hapa tulielezwa kwamba kuna mwanamke mzalendo ambae amegundua dawa ya wadudu wanaoingia katika matunda, sasa mimi nilitaka nijue kama mzalendo huyu serikali imechukua hatua gani ya kuhakikisha kuwa inamsaidia?

Hichi ambacho kakivumbua kama tayari kimefanyiwa utafiti na kuonyesha kwamba kweli inafaa sasa ni msaada gani ambao tumempa? Kwa sababu haya maradhi hivi sasa imeshakuwa ni kikwazo, kwanza yalikuwa ndani ya embe sasa hivi tunda lolote yamo. Kwa hivyo nataka nijue hatua ambayo serikali imechukua kwanza kuhakikisha utafiti kwamba kweli hao wadudu wanakufa isijekuwa maana yake , Mhe. Mwenyekiti kungumanga tunaijua kazi zake, karafuu pia tunajua kazi yake ile inalegeza, hii inakazanisha sasa vitu viwili hivi vinapokutana nahisi ni mtihani kidogo, lakini nadhani watafiti wenyewe watakuwa tayari huyu mzalendo amefikia pahala kaona kwamba ni dawa.

Mhe. Mwenyekiti jengine juu ya tatizo hili la wadudu wanaoingia kwenye matunda serikali imechukua hatua gani ya kuhakikisha kama matunda hayaingii ndani ya nchi yetu, kwa sababu nina hakika haya maradhi yameingia kutoka katika nchi ambazo zinatuzunguruka, lakini wakati huu tunatibu na kutafuta dawa hatuyapunguzi tunayazidisha kwa sababu njia ya kupitia matunda ziko wazi. Kwa hivyo nahisi wakati tunatafuta dawa basi tuweke na udhibiti wa kuhakikisha hakuingii matunda ovyo ovyo ndani ya nchi yetu, wenzetu wanathamini sana na wanaweka karantini kwa kila jambo ambalo wanaona lina dhara.

Mhe. Mwenyekiti katika safari zangu siku moja niko Hong Kong tukayakuta matunda tukanunua komamanga moja zuri sana nikafikiria nilichukue ili nipate mbegu nakuja nayo nyumbani lakini wakati huo nilikuwa naingia China sasa

tumeingia katika treni usiku kumbe mle katika treni kiti kilichoko mbele yako kimewekwa tangazo kwamba si ruhusa kuingiza tunda la aina yoyote, nimeingia nimejichokea na nimelala baada ya masaa matatu niko China kufika uhamiaji zahma, salama yangu kilichonisaidia ni ile kuwa na *diplomatic passport* na wachina ni rafiki na watanzania. Lakini kinyume cha hivyo mungelinisikia redioni tu. Sasa tuone namna gani wenzetu wana udhibiti ndani ya nchi yao ya kuweka vitu kama hivyo au kuzuia vitu kama hivi, kwa hivyo naishauri serikali kuna haja ya kushauri jambo hilo na kulichukulia hatua ambazo zinafaa.

Mhe. Mwenyekiti, nimevipitia kwa kiasi fulani vitabu hivi ambavyo tumepewa na nikaona mikopo ambayo wamepewa baadhi ya watu ambao wamebahatika, lakini katika kipindi kama hiki ambacho tunakwenda nacho cha msuko suko wa uchumi duniani mimi nadhani tungewashauri wananchi wetu, lakini pia tungeyashauri mabenki ambayo yanatoa mikopo kuelekeza mikopo hii kwenye kilimo.

Mhe. Mwenyekiti sisi hapa tupo kwenye visiwa hatuna ardhi kubwa lakini hii ardhi ndogo ambayo tunayo laiti kama tunawawezesha wananchi wetu wakaondokana na hiki kijembe kongoroka mpini, wakaweza angalau kulima kilimo ambacho ukivuna unaweza kutumia kwa mwezi mmoja au angalau ukapata pesa ya kusaidia watoto ingeweza kutusaidia. Lakini kwa namna hii tunayokwenda hizo pesa mbili tatu wanazosaidiwa watu wanazopewa mikopo zitakwenda na umasikini utabakia, si hasha ikawa ni ufukara ukatufunika badala ya umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona kwenye hotuba Mhe. Waziri kajaribu kutoa misamaha kwa vifaa vya kulimia lakini vitu ambavyo katoa Mhe. Waziri sivyo ambavyo kwetu vinalimiwa, wanaolimia ni hao wenye mashamba makubwa matajiri si hawa asilimia sabiini ya wanawake ambao ndio wakulima wa nchi hii hawana uwezo wa hizo zana ambazo zimetajwa hapa kwamba zinatolewa msamaha, tungekwenda kwenye pembejeo Mhe. Mwenyekiti, madawa hapa tungeweza kweli kusaidia tofauti na wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti juzi nilimuona Mhe. Prof. Sarungi kwenye jimbo lake anatoa matrekta arubaini na tano, kenda kukabidhiwa tu sio yeye katoa lakini ni wananchi wenyewe wameji- *organize* , ilikuwa kuna shamba la serikali linataka kukodishwa akasema hapana hili tukodisheni sisi wakakodishwa wakaji- *organize* wakanunua matrekta na vifaa vya kuvunia na kila kitu. Sasa sehemu kama hiyo ndio ingefaa lakini sisi wakulima wa kuwapa afueni hiyo wakowapi? Hakuna Mhe. Mwenyekiti, wetu sisi uwapunguzie pembejeo hapo itakuwa ni kweli wamekusudia kuwasaidia wakulima.

Mhe. Mwenyekiti jengine ambalo nataka kulizungumza na ambalo itakuwa limezungumzwa na wenzangu lakini na mimi sina budi kulizungumza. Hili utaona mara hii kila anayesimama analigusia ni kweli kwa sababu ilikuwa hatujajua kiundani bahari yetu iko vipi ndio maana kila anayesimama unasikia bahari, bahari, yale mafunzo ambayo tumekuja kupewa hapa nadhani ndio yaliyotushtua tukaona kumbe uchumi tunao lakini tumeukalia. Bahari yetu bado haijatiwa mkono meli kumi na mbili tu kutoka ufukweni ndio wavuvi wetu wamejaribu kufikia fikia haijaguswa wanasema bikra, sasa tunatafuta mambo mengine tunaacha hili ambalo liko mbele yetu na linaweza kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti lazima tukubali tumeambiwa ukipewa kilema ujue na mwendo wa kutembea, hizi ni nchi za visiwa na uchumi wake unakuwa wa visiwa na wenzetu kila siku wanapanda ndege na kuteremka lakini kwa nini hili hawalioni na wala hawajifunzi huko wanakokwenda wakaja kutufunza na sisi. Bahari inaweza kutuendesha kuna samaki tokea walipozaliwa mpaka leo hawana asili ya ndevu lakini wameshaota ndevu kwa upevu, lakini kwa mwananchi wa kawaida atafikaje huko bila ya serikali kutia mkazo? Bila ya serikali kuwezesha vijana wetu hawana kazi. Kazi zao ni kukaa barazani na kula unga nguvu kazi inatoweka, hii sio kwamba wanafanya kwa kutaka au kupenda unapokuwa huna la kufanya.

Mhe. Mwenyekiti kichwa kinavurugika lolote unaweza kufanya ukaja kujuta baadae lakini umeshafanya tuwasaidie vijana wetu kwa kutafuta boti za kisasa ambazo zitafika huko ambako wavuvi wa kawaida hawajafika, watavua tutapata kitoeleo cha kutosha ndani ya nchi lakini pia tunaweza ikawa ni biashara tutafuteni meli jamani japo mbili mpaka tatu tuanzie tuelekezeni huko ikiwa huku mambo sio mazuri basi tutizame kwengine na hatuwezi kwenda kama nchi kwa kutizama njia moja tu.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tumekamata utalii karafuu tumeisahau wakati ingekuwa utalii tunao na mikarafuu yetu tunaimarisha lakini hivi sasa mikarafuu inakufa, lakini wakati tunakwenda na haya pia tunatizama uvuvi huku tunapata kidogo na huku kidogo ndio mfuko wenyewe unavyotuna, serikali ifikirie kutafuta meli za uvuvi za kisasa ambazo zitatupa ajira kwa vijana wetu. Nafikiri Mhe. Abass Juma Mhunzi kazungumza hapa asubuhi yeye kasema kufuga kwa hali tuliyokuwa nayo hatuna hata haja ya kufuga. Wale wenzetu ambao wanafuga ni kwa sababu wamepungukiwa na wameitumia sana bahati, sasa inabidi wafuge lakini sio mbaya hata hiyo mifugo pia tunaweza kuwasaidia. Kwa sababu pweza wa kufuga Mhe. Mwenyekiti nimeona wiki tatu tu anavuliwa na nipweza wa kukatana shoka.

Kwa hivyo tutizame utanona ni vitu vidogo vidogo lakini hebu tizama bei ya pweza bei ambayo inanunuliwa, tutizame kamba huli hapa mpaka uwe na homa

au uwe umetamani kutokana na bei, lakini kama tunawawezesha vijana wetu wakaweza kufuga tutaweza kutumia wenyewe ndani ya nchi lakini pia tutaweza kusafirisha. Tusijidanganye tukasema kwamba huo msuko suko wa uchumi duniani sisi hauwezi kutufikia tunao kwa sababu tumo humu humu na sisi duniani na tunatarajia hao walioko duniani sisi ndio tunakoponea ili kunyanyua miradi yetu, sasa ikiwa wao hawana na uchumi kwao unaporomoka sisi tunatarajia nini?

Mhe. Mwenyekiti watafiti wanasema hasa utafiti unaonyesha kwamba huu mmong'onyoko wa uchumi duniani una uhusiano wa karibu na upandaji wa bei duniani sasa sisi hatuna ambacho tunazalisha, hatuna viwanda isipokuwa vya maji tunategemea chochote tukipate kutoka nje, mfumko wa bei athari zake zinaonekana dunia nzima leo utasema sisi hatuwezi kuathirika waheshimiwa itakuwa tunajidanganya lakini nadhani hatujachelewa sana tutafute njia muwafaka wa kuweza kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti la mwisho ambalo nilitaka kuzungumza nilikuwa natizama hii bajeti lanini naona imemsahau mwanamke, mbali ya yale mambo ambayo ni ya pamoja pamoja, kwasababu ukisema nikijenga barabara itamsaidia mwanamke, ukipeleka umeme vijijini umemsaidia mwanamke lakini yale mambo ya kijinsi ambayo kama mimi Zahara nnayo lakini Mhe. Dk. Mwinyi hana sioni imemtizamaje mwanamke wakati tunajua wanawake ni asilimia hamsini na moja kwa nguvu kazi wanasaidia sana katika nchi, kuna mahitaji ya lazima ya wanawake kama afya. Nilitarajia badala ya kelele zetu zile za mwaka jana Mhe. Waziri aje atwambie kama hii ambayo anatozwa mwanamke kwa upereshen katika bajeti hii imeondoka, lakini naona hakuna hilo neno wala hakujazungumzwa chochote kuhusu hilo.

Mhe. Mwenyekiti, hili nadhani ni jambo ambalo kama wanawake linatuuma na sisi wajumbe wako wa baraza lako hili linatuuma zaidi kwa sababu tusiozaa tunazaliwa, kutwa tupo hospitali kwa sababu wanatwambia nyinyi ndio ambao tumewapeleka katika Baraza la Wawakilishi na hamututetei kwa hivyo hizi zitatoka katika mgongo wenu arubaini elfu. Kwa nini tunashadidia hili jambo ambalo tuna mambo chungu nzima ambayo tunayatolea misamaha. Kuna wafanya biashara ambao tunawasamehe tuna makodi ambayo tunayasamehe sasa kuna lazima gani kushikiria mpaka leo kuweka iwe hivi? Kuna kodi gani ambayo ni kubwa ambayo serikali haiwezi kusamehe? Jamani waoneni wanawake kama ni wazee ambao wamewazaa, iwapo hutomhurumia mama utamhurumia nani?

*Lailaha ilallwa Muhamada Rasullullah* mfunguzi nifungue ili nijifungue nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia bajeti hii ya mwaka 2010/2011 kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na afya.

Lakini pia nikushukuru wewe mwenyekiti kwa kukalia kiti chako cha enzi kizuri na kuendeleza mjadala huu ni fursa nzuri na pengine kukalia kiti chako hapa inapingana na ile kauli ya wengine kwamba wanawake wanatengwa baada ya kuondoka Mhe. Spika, sasa umefuatia wewe kwa hivyo nafikiri huo ni usawa kijinsia.

Lakini pia nitoe pongezi na shukurani kwa waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi ambao wamepata fursa ya kuichangia bajeti hii. Pongezi nyengine pia niwape Wawakilishi wa CUF ambao tayari wamemaliza mchakato wa kura za maoni kwa chama chao, *ishaalla* na sisi tutamaliza salama ili tuje kuungana nao.

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi yeye pamoja na timu yake yote Katibu Mkuu, Makamishna na Wakurugenzi, Manaibu Makatibu Wakuu kwa hakika watu hawa wamefanya kazi kubwa sana na wao ndio wachumi wetu wa kutuchumia hiki ambacho tunakitumia sisi ambao tunatumia tunaweza kusema hakikukolea chumvi na hakikukolea mafuta lakini ukweli wanajitahdi sana na wako katika hali ngumu na wanastahiki kusifiwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, mtiririko wa kibajeti unategemeana haiwezekani bajeti ya mwaka mmoja ukaitenganisha na bajeti iliyopita au ijayo, kwa kipindi kirefu kidogo watendaji wa Wizara ya Fedha na Uchimi na viongozi wao Mhe. Waziri na katika hali ya kipekee Mhe. Rais wetu namshukuru sana wamejenga uwezo mkubwa wa kifedha katika Wizara ya Fedha lakini pia wamejenga nidhamu ya matumizi ya fedha. Maana unaweza kuwa na fedha nyingi lakini bila ya nidhamu ya matumizi hali inawa kuwa mbaya.

Sasa na mimi nipate fursa hii kumpongeza Mhe. Rais kwa kuisimamia sekta hii ya fedha na kujiimarisha vizuri na kwa kipindi cha miaka kumi hakujawahi kutokezea tatizo kubwa ambalo limeishinda serikali kuitatua, kweli tumepitia katika hali ngumu wakati mwengine dunia imetetereka kiuchumi sisi wenyewe ndani tumepata matatizo ya kiuchumi lakini shughuli za kiserikali na shughuli za kijamii zinaenda na sote tunapata huduma kama ilivyopangwa.

Mhe. Mwenyekiti kuanzia mwaka 2008 mpaka 2009 hata mataifa makubwa ambayo uchumi wao ni mzuri waliyumba sana na sisi huku ambao ni watu wadogo wadogo, kwanza tulikuwa tukihangaika kiakili itakuwaje kwetu tutaishi je kwa sababu hakuna mtu ambae anataka kukopesha na

anayekukopesha anakuuliza utamlipa lini ili na yeye aweze kusonga mbele, wafanya biashara wameacha kulipa madeni kwa sababu na wao walikuwa wanasema hatuna cha kulipa na kama mtu umemkopesha hana cha kulipa utamfanya nini itabidi ustahamili kwanza mzungumze sasa hii hali haikuwa nzuri kwa dunia na hali hii Zanzibar haikujitenga kwamba haikukumbana nayo, lakini kutokana na maarifa ya watu wa fedha tukifanya nao vikao walikuwa makini na kutufikisha hapa leo alhamdullillah.

Lakini sio hilo tu kabla hili halijamalizika tukapata tatizo la umeme nchini nalo likatuathiri sana tukawa na simanzi kubwa sana, lakini hawa watu wa Wizara ya Fedha na Uchumi na watu wetu wa mipango na uchumi ambao waliandaa programu nzuri katika miezi yote mitatu kunako tatizo la umeme, tuliweza kupata maji ingawa kwa mgao kwa kutumia majanareta shughuli za kiserikali ziliendelea sisi ambao tuko serikali tunasaidia shughuli hizi tuliathirika kidogo lakini sio kwa kiwango cha kutisha kwa sababu ya mpango mzuri wa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Sisi ni watumizi wakubwa wa fedha za serikali wizara yetu lakini kwa kipindi chote tuliweza kupata fedha na hazikukatwa hata mara moja Wizara ya Miundo mbinu msifanye kwa sababu hali iko mbaya tunawashukuru na kuwapongeza sana sisi na wenzetu wa kilimo, umeme na Waziri wa elimu sote tuliendelea kupata huduma hizi. Hili ni jambo ambalo liliwezekana kwa sababu ingelikuwa hawakujiandaa kwa muda mrefu kupanga mipango ya kiuchumi isingeliwezekana miezi ile mitatu kuhimili uchumi tungeliweza kuparaganyika na kuanza kuyumba katika suala la uchumi, lakini waliweza na bahati nzuri sote tukashikamana bila ya kujali misingi ya vyama na tukaweza kuishi vizuri kwa kustahamili na baadae hali imejirekebisha. Kwa hivyo nasema hawa watu wa Wizara ya Fedha na Uchumi wanastahili pongezi sana.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii ya mwaka 2010/2011 na kwa kuwa mambo mengi yako tayari nchini ninatoa fursa kubwa kwa Wazanzibari kuwekeza katika nchi yao, lakini hata kwa wageni ambao kuwa wana nia njema kuwekeza katika nchi yetu. Sasa ni fursa kwa Wizara ya Fedha kutusaidia tuweze kufikia malengo ili kile kilio cha Waheshimiwa walichokizungumza hapa cha kuwa na sisi ni wazalishaji kiweze kufikia malengo.

Sasa hivi kuna utaratibu kwa wananchi wetu wengi kuwa na SACOs. Mimi ningewashawishi Waheshimiwa Wawakilishi na sisi tungelijikusanya kikundi angalau cha watu 10 tukipata kiinua chetu mgongo tuweze kufanya jambo letu moja la maana cha ushirika, sisi tunaaminiana ni watu wazima nafikiri tunaweza tukachukua pesa zetu zile, tukakopa na Benki kidogo tukafanya jambo kubwa ambalo litatupa maslahi ya baadaye katika maisha yetu.

Nitoe changamoto kwa Waheshimiwa Wawakilishi bila ya kujali msingi wa chama wala jinsia. Humu ndani kuna wajasiri amali wakubwa, wazuri wanaweza kutuongoza ili kutusaidia tuweze kufikia na sisi tuwe kama wao. Lakini tukienda mmoja mmoja nafikiri itakuwa sio rahisi kwamba kila mmoja humu anaweza kufanya jambo la maana, lakini mkiwa watu kumi basi mnaweza mkapata fedha mkafanya jambo la maana. Wapo waheshimiwa humu wanao uwezo wa kutusaidia kama Mhe. Mazrui na wengine hebu basi ingieni humo mtushawishi tuingie katika ujasiri amali na sisi tuweze kuisaidia nchi yetu. Maana tukiwa katika hali bora sisi ina maana ni hali bora ya wananchi na hali bora ya nchi yetu kiuchumi. Bajeti hii ni ya maendeleo na demokrasia na sisi waheshimiwa tukaeni tufanyeni jambo ambalo litatusaidia na sisi kuondokana katika hali ngumu ya utegemezi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niishukuru sana Wizara ya Fedha kwa kipindi kirefu wameendeleza hili jambo ambalo halijaweza kuyumba tena na ulipaji wa viinua mgongo tangu alipoingia awamu ya sita Mhe. Amani Abeid Karume. Nafikiri jambo hili limekwenda vizuri na nafikiri halikurudi nyuma. Mwanzo tulikuwa tunahofu kwamba pengine baadaye itarudia hali ile ile lakini haikurudi tena. Hata sisi ambao tunafanya kazi kwa miaka mitano kulipwa kiinua mgongo tulivyoingia Barazani mara ya kwanza tukaambiwa tutalipwa, tuliwakuta waheshimiwa wenzetu waliondoka mtu anakuja anapewa laki tano anaondoka, anapewa laki tatu  tena kwa uwenyeji. Lakini sote Mwenyezi Mungu alijaalia 2005 tulilipwa kwa pamoja kwa kiwango ambacho tumepangiwa hakuna mtu aliyeondoka anadai na tunatarajia 2010 tutaondoka hivyo hivyo hakuna mtu ambaye atadai serikali kwa suala la kiinua chake mgongo. Haya ni mambo ya kuyashukuru na kuwapongeza wenzetu ambao tumewachia jukumu la kushughulikia suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la CDF na mimi nimponge Mhe. Waziri na timu yake kwa kuona kwamba kuna umuhimu na sisi kuanzisha CDF. Ushauri wangu kwamba ingekuwa ni vyema tutakapoandaa sheria kwanza tufanye mawasiliano na wenzetu ikiwezekana tuzungumze na SMT kwamba sisi huku Zanzibar tuna viongozi wawili sawa. Tutakapokuwa na mifuko miwili kwenye jimbo moja badala ya kutuunganisha inazidi kutuweka mbali. Kama ingeliwezekana maarifa yakawepo kukawa na mfuko mmoja ukawa na wenyeviti wenza nafikiri haya mambo kidogo yangekuwa mazuri na yangepunguza hili joto la kuwa watu wawili mpo jimbo moja lakini kila mtu na mfuko. Sasa itakuwa wa mfuko huu anafanya hivi na wa mfuko huu anafanya hivi. Hili nafikiri ni jambo jema na hizi fedha sio kwa ajili ya Mhe. Mbunge kuzitumia kama zake na pia sio za mwakilishi kuzitumia kama zake, hizi fedha wenyewe ni wananchi basi ni vyema ingelikuwa njia moja ikapitia fedha hizi ili zitumike kwa maendeleo ya wananchi na tungeliimarisha hata watoaji wa maamuzi yakawa hayapo kwa waheshimiwa hawa waliochaguliwa, yakawa

kwa wananchi wa eneo lile kwamba fedha zao waziamue wenyewe wanazifanyia nini kwa ajili ya maendeleo yao ili kupunguza tatizo ambalo linaweza kutokezea kama sisi tutakabidhiwa tutoe maamuzi ya utumiaji wa fedha hizo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo sasa kwa ufupi naomba nizungumzie yale ambayo waheshimiwa wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi walizungumzia kwa Sekta ya Miundo Mbinu na Uchukuzi. Kwanza Mhe. Saidi Khelef alizungumzia kuhusu Baraza ya Bumbwini, alisema dalili anaziona kama barabara inajengwa lakini isiwe kuwekwa vifaa tu.

Nimshukuru Mhe. Said kwamba anajitahidi sana kuhakikisha kwamba barabara ile inajengwa na ninazo taarifa za uhakika kwamba yeye na Mhe. DC walikwenda kuzungumza na wananchi kuhusu upatikanaji wa kifusi na baadaye Mhe. DC tuliwasiliana na tukazungumza na tukakulibaliana baadhi ya mambo. Jambo ambalo Mhe. Said umelizungumza kwamba wananchi walitaka kwamba vipando vyao viking'olewa wapewe wenyewe hili nafikiri halina mashaka na sisi ombi hili tunaweza tukalikubali kwa sababu sisi tunataka kusafisha ili tufanye shughuli nyengine, kama mtu kuna mnazi wake anataka kuchukua mwenyewe itakuwa ni juu yake wala sisi tutakuwa hatuna matatizo naye.

Isipokuwa tunawaomba wananchi wa Bumbwini waendelee kutuunga mkono, barabara inajengwa kwa ajili ya maendeleo yao na maendeleo ya nchi kwa hivyo watupe mashirikiano. Jambo ambalo tunalifanya hivi sasa na linatukwaza kidogo ni uondoaji wa miundo mbinu katika barabara, tuna tatizo moja kubwa ambalo linatukabili. Sisi tukijenga barabara wenzetu wa miundo mbinu mengine na wao wanakuja kujenga na wao humo humo watu wa maji wanasogea karibu ya barabara waweke mabomba yao watu wa umeme na wao wanaweka nguzo zao. Siku tukitaka kutanua barabara yetu inabidi wao tuwalipe. Sasa gharama za mwanzo za uondoaji wa mambo ya maji kwa barabara ya Bumbwini zilikuwa karibu milioni 360 ni fedha nyingi sana. Tunazungumza nao ili kutafuta jinsi ya kupunguza gharama, kwa sababu fedha zenye hizo ndio za ujenzi, hapo hatujalipa nyumba wala hatujalipa vipando vya watu. Tunataka tuanzishe fomula mpya, tukijenga barabara wenye mabomba ya maji wasisogee karibu ya barabara na wenye nguzo za umeme na wao wasogee mbali kidogo ili tukifanya utanuzi wa barabara hizo gharama nyengine ziepukike.

Halafu weheshimiwa wengine walizungumzia zaidi Mhe. Muhunzi leo asubuhi alizungumzia uimarishaji wa Bandari ni muhimu. Na mimi nakubaliana naye na hivi sasa Shirika letu la Bandari limeshaagizia vifaa, vikija tutavigawa pia na Pemba ili Bandari ya Mkoani nayo ipate vifaa vya kupakia na kupakuliwa mizigo. Pia alizungumzia barabara ya Kenya/Chambani. Waheshimiwa

barabara hii ipo katika mradi wa ujenzi wa barabara sita (6) za Kusini Pemba, ikiwemo barabara ya Mtambile/Kengeja ambao ujenzi wake upo katika hatua nzuri Mungu akipenda tunatarajia mwezi wa nane au wa tisa kikosi kazi cha pale kitaondoka na kuhamia barabara ya Mizingani/Wambaa. Halafu tumeanza ujenzi wa barabara ya Mtambile/Kangani, hatua za usafishaji zimeshakwenda vizuri, tumeshapita mpaka mbele ya Mhe. Muhiddini tumeshafika mbele ya nyumba yake kwa mbele pale kalvat nyengine zimeshaanza kujengwa kwa hivyo nayo kazi inakwenda vizuri. Kikosi hichi kikimaliza ndio kitaingia Kenya Chambani.

Ushauri wa Mhe. Muhunzi ni mzuri lakini kwa barabara ile ilivyo tunahofu kwamba tukiyang'oa yale mawe na hali ya mabonde ya ile barabara pembeni inawezekana tukaondoa tatizo moja tukapeleke tatizo jengine la pili. Sasa hivi hakuna tope lakini unakwenda taratibu kwa sababu ya mawe kidogo yapo juu sana, sawa sawa na barabara ya Chanjamjawiri Tundauwa nayo ni ya mawe, ukiyang'oa yale kabla ya kujenga barabara unaweza ukapata tatizo jengine la kuwa na tope na utelezi.

Juzi nilikuwa Wambaa, ukweli kuna sehemu Wazani kwendea bondeni barabara ni mbovu imeharibika sana. Tumekubaliana kwamba tungojee kidogo barabara ikauke kidogo, twende tukaifanyie matengenezo ya dharura kabla ujenzi rasmi wa barabara ya Mizingani/Wambaa kuanza.

Waheshimiwa tutakapojenga lazima kuna wengine wawe na subira, kwa sababu huwezi kujenga msingi ukataka ukaezeke na paa kabisa, lazima tuende taratibu, tujenge msingi, tuweke matofali na baadaye tuende kwenye paa. Zile barabara ni sita zina awamu tatu, ya kwanza tumeanza tutakwenda ya pili, tutakwenda ya tatu, zote Mungu akipenda lengo letu tuzimalize ili wananchi wa Kusini Pemba waondokane na tatizo la barabara.

Kuhusu wizi wa vifaa, Mhe. Muhiddin tumekusikia lakini tunaomba na wewe kama mwakilishi wa wananchi na zile barabara ni za wananchi anayeibiwa pale sio serikali, tusaidieni sio lazima wewe mwenyewe umkamate mtu lakini tupatieni taarifa ambazo sisi zitatusaidia kama wafanyakazi wetu tuweze kuwakamata na kama wananchi basi tutajua tutumie vyombo gani vitaweza kutusaidia. Kwa sababu kama kweli unavyosema tukiibiwa kila kitu hasara ni yetu sote, serikali, wananchi, viongozi, kila mmoja atakuwa na hasara yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla bajeti hii imezungumza mambo mazuri na kuna moja la barabara ya Kiongole jana Mhe. Haji alizungumza namshukuru kwa maoni yake. Ni kweli kwamba tulichelewa kuianza lakini tayari tumeshatoa baadhi ya kazi na tulikubaliana kwanza tuanze na ujenzi wa madaraja na kalvat katika barabara ile kwa sababu sio wengi ambao wameshawahi kufika

Kiongele. Pale Kiongele/Mkwajuni ni eneo linye vimto vingi katikati, maana eneo la kutoka Mkwajuni mpaka Donge kati kati kuna sehemu zenye mito mingi sana. Lazima kwanza basi tuanze na vidaraja hivi na baadaye tuweze kujenga barabara. Nimemuahidi kwamba tutakwenda kuangalia barabara hii nafikiri kabla ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano kusomwa mwanzoni mwa mwezi wa saba (7) hapa katika Baraza lako.

Mhe. Naomba nimalizie kwa mambo mawili kwa juhudi kubwa ambayo imechukuliwa na Wizara hii ya Fedha kwa bajeti hizi nzuri basi tumeweza kufanya matengenezo makubwa ya *runway* yetu na Mungu akipenda hadi mwezi wa saba itakuwa imekamilika kila kitu mpaka taa za uwanja zitakuwa tayari. Hizi ni habari za faraja na tayari tunatarajia ujenzi wa jengo la abiria utaanza hivi karibuni kampuni ya Kichina watajenga jengo hilo.

Mhe, Mwenyekiti, Mhe. Waziri anayeshughulikia Fedha nichukue fursa hii kwa niaba ya wafanyakazi wa mawasiliano kukushukuru sana kwa juhudi zako na watendaji wenzako, lakini shukurani za pekee zimuendee Mhe. Rais wetu, amekuwa akisimamia utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka 10 kwa umahiri na kwa ufanisi mkubwa na leo tofauti na bajeti ya miaka 9 zote zilizopita. Bajeti hii watu wanazungumza kwa furaha sana kwa pande zote mbili . Nina hakika kwamba pande zote mbili tutaiunga mkono bajeti hii na kuweka historia mpya ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Chumbuni ambao nawawakilisha hapa kwamba tunaiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia.

**Mhe. Aziza Nabahan Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie kidogo. Awali ya yote tumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili nikupongeze kwa ulivyopendeza hapo kwenye kiti alau sasa hivi Baraza linapendeza kapatikana na mwanamke anaonesha kwamba na mwanamke anaweza na *Alhamdulillah* kaanza kutuongoza vizuri.

Tatu nizungumze kidogo kuhusu Bajeti ya Demokrasia na Maendeleo. Bajeti yetu tumeletewa hapa tumeambiwa ya demokrasia na maendeleo. Sisi sote tunajua nini demokrasia na nini maendeleo. *Inshallah* Mwenyezi Mungu aijaalie hii bajeti iwe kweli ya demokrasia na iwe ya maendeleo. Ili na sisi katika nchi hii tuwe huru na amani na utulivu na maendeleo yapatikane yaje katika nchi hii ili wananchi wetu wafaidike.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naanza kidogo kuhusu uchumi wetu. Sote tunajua kama uchumi wetu ni mdogo hautoshelezi kwa nchi yetu. Nchi yetu sisi ni visiwa lakini ni visiwa vyenye utajiri mimi nasema sisi si masikini hapa. Sisi ni

matajiri sana na tuna vitu mbali mbali ambavyo vinaweza kutuendeshea nchi yetu kabla hata ya hayo mafuta hayajachimbwa wala hayajaja.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tuna karafuu, kilimo, bahari imetuzunguka nchi zote mbili, bahari yenyewe inatoa samaki kwa wingi. Sisi tuna mambo mengi hapa, ingawa hatuna migodi ya dhahabu lakini migodi mengine Mungu ametuteremshia na tunayo.

Kwanza tuzungumze kuhusu mazingira yetu, uchumi wetu unategemea na mazingira yetu yalivyo. Lakini mazingira yanatakiwa yawe vipi, mazingira yatunzwe ndio utakapoweza kupata uchumi ndani yake. Lakini sisi mazingira yetu bado Mhe. Mwenyekiti, hatuyatunzi, tunakwenda nayo tu kihivyo hivyo halafu tunalaumu, tunawambia watu wanaharibu mazingira kumbe mazingira tunayaharibu sisi wenyewe.

Niseme kama ule ukanda wa Micheweni, nimekwenda wakati wa ziara yangu ya Kamati tumekwenda kuuona ukanda wa maeneo huru. Jana hapa sijui nani alisema huru huru, huru kweli. Tunawalaumu wananchi wanakata matofali wafanye nini na eneo lipo wazi na wao wana njaa, watakwenda wakakate matofali, wauze wapate waendeshe maisha yao. Lakini sisi ingelikuwa yale maeneo tumeyatumia kama tulivyokuwa tumekusudia yasingefika kukatwa matofali lakini tumewaachia wananchi wetu wenakwenda pale wanakata matofali, wanauziana, wanajengea na wanafanya kila kitu, wakati huo huo maeneo yale yanaharibika. Hata huyo muwekezaji akija akiiyona ile hali ilivyo kule sifikiri kama atatamani kuwekeza. Hatotamani kuwekeza kwa hali ya mazingira, hatotamani kuwekeza kwa hali ya njia iliyokuwepo kule.

Kwa hivyo tukiwalaumu watu kwamba wanaharibu mazingira hawaharibu watu ila wanasababishwa wayaharibu. Serikali ijitahidi yale mambo ambayo tunayaamua kufanya *must be serious* tusifanye kitu tunakiamua halafu tunakiacha, kuna mambo mengi kama haya ya kukuza uchumi wetu ya kutuendeleza lakini hayaendelezwi yataamuliwa, yatapangiwa kamati, yatafanyiwa kila kitu yataambiwa hayo hapo utaona kama sasa unapata mapesa tele lakini *at the result* unakuta mambo yamekwenda hata hujui yamemalizikia vipi.

Mfano mmoja mkubwa sijapata kuusikia tokea nimeingia katika Baraza hili kutajwa hapa palikatwa msitu, ikakatwa miti, pakapandwa mipira ndani ya nchi hii Unguja na Pemba lakini hata siku moja. Miye tokea nimeingia katika Baraza hili sijasikia kwamba mipira ile imeleta tija gani kwa nchi yetu, mipira ile imevunwa kiasi gani na imetia faida kiasi gani au imetia hasara vipi. Kama haina faida kwa nini tunaiwacha tuiondoeni imekaa tu utafikiri watu waje kutembea waje watizame mipira wende zao haina maana. Lakini kama inatia

tija kwa nini hatuambiwi na kwa nini haiendelezwi. Kuna sehemu nyengine imekatwa mikarafuu, sehemu nyengine imekatwa minazi kwa kupandwa mipira ili uchumi uongezeke. Lakini ile mipira ndio mipira imeshabakia vile vile hatujui kitu chochote kinachoendelea na kinachopatikana katika mipira ile.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeliwashauri serikali tutafute chumi mbali mbali ili tuendeleze nchi yetu, lakini tutafute kwa dhana kwamba tunatafuta halafu tunaendeleza. Tusitafute tukaiweka ikawa haitufaidishi kitu chochote au wanafaidika wale wanaopewa mashamba ya mipira kwa sababu nasikia kuna mengine yanakodishwa, wanakodi watu wanavuna. Sasa je, nyie mnaokodisha mnapata faida ndani yake kama inapatikana basi tuelezeni na siye tujue kwa sababu tukiulizwa huko tupate kujua la kujibu na tutakuwa mstari wa mbele kuitetea mipira ile. Toka ilipopandwa mipira ile na kuvunwa nafikiri ingelikuwa tayari tushajenga kiwanda cha kutengenezea mipira, kwa sababu utomvu tunao wenyewe hapa na tunaupata kwa wingi kwa nini tusiweze kuweka kiwanda cha mipira tukaweza kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu wanawake, maana mimi ni mwanamke na walionileta hapa hususan ni wanawake. Wanawake naona kama wanyonge, tunahitaji msaada mkubwa kutoka serikalini, kutusaidia ili tuweze kujiendeleza. Wanawake ni asilimia 70 ni wakulima na ukiwakuta hizo hali zao huko mashambani utawaonea imani na wao ndio wanaosaidia kilimo tukapata chakula tukaja kula siye tunaokaa mjini. Bila ya wao kule hakuna kinachoendelea. Serikali imewasaidia vipi ili waendelee pale walipo, wanalima lakini hawapati faida.

Kwa sababu wanalima mgomba lakini ni mgomba ule ule wa zamani anakwenda mtu na kijembe chake atachimba shimo atatia mgomba wake utazaa mizao miwili mgomba unang'oka, matoto yale ya chini yake yanayokuja yanang'oka, hapati faida kwa sababu hana taaluma. Tuwasaidieni wanawake sio kwa kuwapa pesa, tuwasaidieni wanawake kwa kuwapa taaluma ya namna gani waendeleze kilimo, namna gani walime mpunga, walime migomba, walime mihogo. Kuna baadhi ya nchi zao lao kubwa ni mihogo, kwa nini na sisi tusiweze kuwafundisha watu wetu au wanawake wenzetu au wanawake wa visiwa hivi wakaweza kulima vizuri na wakapata mazao mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi Unguja hapa tuna hatari, ndizi nyingi zinatoka Pemba, bado wenzetu Pemba wanalima vizuri kuliko hapa. Hapa tunalima migomba, lakini siku mbili tatu unakuta migomba ishawiva imekuwa rangi ya manjano, pengine haiwahi hata kuzaa. Sasa yale yote sio makosa ya wanaolima ni makosa kwamba hawana taaluma. Tunamabwana shamba waliojaa katika maeneo yetu, lakini mabwana shamba hao sijui wanafanya nini. Kwa sababu

haiwezekani kwamba mabwana shamba wapo wasione yale makosa yanayotendeka ili wakayarekebisha na wakaweza kuwaelimisha wale watu.

Mimi naiomba serikali sana iwasaidie wanawake, iwasaidia kuwapa taaluma, kuwapa nyenzo, sio lazima ukamnunulie mwanamke trekta la milioni ngapi ukamletea hivyo hivyo kidogo wengine wanalima kwa trekta la ng'ombe lakini wana taaluma nayo. Lakini hapa hatuna kwa hivyo tuwasaidie wale wanawake waweze kulima tupate manufaa kwa sote na tuwapunguzie mzigo na ukali wa maisha. Jamani mama ana kazi kubwa haidhuru nimekwenda kwenye mafunzo nimeambiwa kwamba mwanamme ana kazi maana yake ndio baba analipa anafanyaje, hamna. Mwanamke ana kazi ndani ya nyumba ya kuelea mtoto anapokuwa na njaa hakwambii baba nna njaa anakuja kwa mama, mama naona njaa nataka kula. Mama wakati mwengine unakung'uta mifuko unamwambia miye sina kitu, wewe fanya maarifa. Kazi yote na jukumu lote linarudi kwa mama.

Tumsaidie mama yule ajiweze tusijione sisi wengine ambao tunao uwezo ndani ya makazi, mabaraza, manini, waume zetu wanapesa wanakuja wanatuhudumia. Lakini kuna watu huko mlo mitatu hawaiwezi, mmoja unawashinda sasa namna gani jinsi ya kuwaepusha na yale ni kumsaidia huyu mama, baba zaidi ukipata pesa nyingi sana utakwenda kuowa tu. Lakini mama pesa yake atakavyoipata anajua kula na watoto wake, wanajua kusomesha watoto wake. Kwa hivyo tumsaidie mwanamke, miye nitasema sana kuhusu mwanamke kwa sababu najua nini jukumu la mama ndani ya nyumba.

Waheshimiwa Wanawake wanajaribu kila jambo kufanya, wanawake ndio wanaofanya visheti wakenda wakauza ili apate buku la mtoto, mwanamke anakaanga samaki apate pesa akanunue japo nusu kilo ya chakula amsaidie baba. Baba mwengine anasema miye si nishaleta mchele wewe tafuta bizari, sasa mama kama hajasaidiwa akapata maendeleo atapata wapi hiyo bizari.

Mhe. Mwenyekiti, hii bajeti kidogo naona mnaufinyu wa hali ya kutizamwa wanawake. nimemtizama mwanamke kwenye afya kwa sababu ni bajeti ya pamoja baba yumo, mama yumo na mtoto yumo. Ukenda kuna mtoto zaidi kuliko mama lakini elimu ile ni lazima aisimamie mama ndani ya nyumba baba kutwa hayupo, yeye yupo na pirika zake mama ndio anayetaka amlazimishe mtoto akamate buku asome. Sasa kama mama atakuwa hana utulivu na mtoto hasomi kabisa atashuhulika na mambo mengine na michezo na yeye kashuhulika masikini anahangaisha na maisha ili apate rizki ya kwenda kula na watoto wake. Wengine wanao waume wa kuwasaidia, wengine hawana jamani. Tuwasaidieni wanawake.

Juzi nilisikiliza kwenye mawiyo nilisikia neno ambalo limenisikisha sana nimeona niliseme labda serikali itashtuka kidogo. Kuna watu nafikiri wameruhusiwa kuvua, wamepewa *lisence* ya kuvua wenye meli. Lakini wanachokifanya sasa hivi ni sehemu ya Jambiani, sijui Mhe. Nyonje yupo hapa. Wanasema kuna meli zinakuja zinavua haya maji madogo. Sasa hawa wenye vidau jamaa zangu miye watavua wapi, wanawake wanapiga kelele mpaka mwani wao unakokotwa na zile meli ndivyo tulivyoruhusu serikali. Baada ya kuwapa ruhusa huko maji makubwa kwenda kuvua tunawaachia wanakuja mpaka ndani, watu wetu watakula nini. Kama pande za Kusini, sehemu za Jambiani uvuvi ndio chakula chao, uvuvi ndio matumizi yao.

Sasa leo ukiwa wewe mwenye meli kubwa unakuja kuvua kwenye maji madogo unamwambia huyu anayevua kwa kingalawa na kijahazi afanye nini. Wanapiga kelele watu wale ndani ya radio wanasema tumeshapeleka habari lakini sisi tumekaa tunatizama tu serikali itafanya nini. Kwa hivyo tuwasaidieni watu wetu tusizidi kuwaumiza. Kwa sababu kuwaachia meli kubwa zikaja zikavua maji madogo ni kuwaumiza wao halafu kuwaachia wanatubururia na mwani wetu wanawake ambao tunategemea pale tupate pesa za kujiendesha. Waheshimiwa kuna mambo lazima tuyatizame na tuyachukulie hatua.

Waheshimiwa nije kwenye afya na mama hapa nimeona kwenye ukurasa wa 46 tumeambiwa mambo mengi, kuhusu matone, kuhusu chanjo, kuhusu nini. Mwanangu Zahara kasema hapa lakini lile la elfu arubaini hatujaliona na tulilipigania hapa Baraza zima tukilisema hii elfu arubaini iondoshwe kama haikuondoshwa kabisa basi hata haipunguzwi, ili wanawake wakenda kule wasipate tabu. Jamani kuzaa kazi hivyo, mimi ningeliomba serikali kwa sababu nchi za wenzetu unapokwenda kujifungua baba na yeye anaitwa, anaambiwa kaa pale umtizame mkeo mpaka amalize kuzaa. Sasa ningeomba na hapa serikali tukajaribu kidogo. Kina baba mkaona namna gani kina mama wanavyopata tabu, seuze yule ambaye anashindwa kuzaa mwenyewe anahitaji kufanyiwa operesheni.

Anakaa pale roho yake iko mikononi anamuomba Mwenyezi Mungu amsitiri, alau unamwambia toa shilingi arubaini elfu kama hukutoa sikufanyii operesheni, si tunawaua kwa makusudi tena itakuwa tumewasaidia hivyo kuwaambia tunafanya hifadhi ya mama na mtoto. Anaweza kufa mama na mtoto wake au anaweza akafa mama mtoto akabakia na akibaki mtoto unamuonea kwa sababu anabaki yatima atalelewa na nani? Tusaidieni jamani. Hizi shilingi 40 elfu haziko kwenye njia nzuri, tutafutieni sehemu yoyote mtutilie.

Watu wanalewa sana hapa wapigieni kwenye ponbe, wanavuta sigara, wanakunywa soda, itieni hii kidogo iende kwenye pombe ichangie kwenye

uzazi. Kwanza tutapata thawabu nyingi kwa sababu unapokwenda kujifungua wakati ule Mwenyezi Mungu anatwambia mbingu zote zinakuwa ziko wazi, makaburi saba yawazi, yanakusubiri wewe mama, sasa ikisha uingizwe na kichwani shilingi 40 elfu za kulipia operesheni. Jamani mnatuonea.

Mhe. Mwenyekiti, pia nizungumzie kidogo kuhusu malaria. Malaria imepungua Zanzibar, haikwisha. Sisi tusijiamini tukasema malaria imekwisha kabisa Unguja, kwa sababu kuna siku hapa hapa nilisema nikaambiwa ukiwa na mgonjwa wa malaria sisi kule Kivunge tunanunua. Sikutaka kushindana, lakini malaria bado haijesha isipokuwa imepungua. Kwa hivyo, tuifanye hii malaria isizidi. Kwa sababu sasa hivi malaria inarudi kwa kasi kubwa sana.

Mimi nimepoteza mwanangu hivi karibuni kwa sababu ya malaria tu. Kakaa hospitali miezi mitatu hapo Mnazi Mmoja, alipimwa malaria mara moja tu akakutikana nayo akatibiwa akapewa ruhusa akarudi nyumbani. Lakini alirudi hospitali miezi mitatu tumemuweka pale, kila siku anapimwa kila aina ya vipimo hajapimwa tena malaria.

Mwisho nikawaambia jamani huyu mtoto mbona anakauka kwa sababu alikonda akakaa kama mgonjwa wa UKIMWI, nikawaambia nipimieni na UKIMWI tena msipime hapa tu, nipimieni kama hospitali mbili au tatu isijekuwa ana UKIMWI. Alipimwa UKIMWI hana, lakini haikuwajia kabisa kurudia tena kumpima malaria. Kafika kutiwa damu mara tatu, akitiwa damu kama leo keshokutwa damu hana imeshakauka, kumbe wadudu wa malaria wameshakuwa wengi wanakula ile damu.

Mhe. Mwenyekiti, nikamchukua nikawaambia basi twendeni Dar es Salaam, tumekwenda huko kufika kitu cha mwanzo alipimwa malaria na akakutikana ndani ya mwili wake hana *red blood cell* wamekwisha wote wameshaliwa na wadudu wa malaria. Waliotawala mule ni wadudu wa malaria, haikufika hata siku tatu yule mwanangu akafariki.

Kwa hivyo, hii malaria bado ipo na inarudi kwa kasi kubwa sana, tusiidharau kabisa. Tutizame na tuwapime watu wetu na kujua nini kinachotusababisha. Mimi nafikiri sasa hivi kungekuwa kuna mkakati mtu akienda hospitali kitu cha mwanzo apimwa malaria ili ijulikane maeneo mengi yana mbu wengi wa malaria pafanyiwe tiba. Hizi dawa za majumbani *Alhamdulillah* mimi leo kwangu imepigwa dawa. Lakini tuzidishe kasi.

Wakati wa zamani mimi mdogo dawa za malaria *WHO* walipokuwa wakipiga mpaka migombani, ndani ya migomba shamba wanapiga, vibanda hata ikiwa cha punda kinapigwa dawa. Kwa sababu ya wale wadudu wasibaki, hawana

wazimu wale waliokuwa wakifanya vile, migomba iliyokuwa karibu na nyumba yote inapigwa dawa hasa siku za mvua.

Kwa hivyo, waheshimiwa tunahitaji sana kuwa na tahadhari ya baadhi ya maradhi ambayo tunayahisi si maradhi makubwa, lakini ni makubwa na yanatuathiri.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kidogo kwanza, nimpe pole si Wizara ya Fedha na Uchumi tu au Mhe. Waziri, bali tujipe pole serikali na wananchi wote.

Juzi kumetokea kitu cha kusikitisha Pemba, jengo lililokuwa linajengwa jipya la Wizara ya Fedha lililogharimu pesa nyingi sana za wavuja jasho. Sijui hata kumetokea nini yule mkandarasi alikuwa anasinzia sijui alipokuwa anajenga au alipotoa *plan* yake, au kaona gharama kubwa kufanya pale. Akaona atuondoshe njiani kwamba hata nendeni huko hamna lolote nyie. Leo jengo limeanguka Pemba.

Sisi tumekwenda kwenye kamati na tuliwaambia sisi tunakwenda zetu Unguja lakini hili halifiki hata mwezi litaanguka. Wakasema halianguki wameliwekea munda, akaa! Banda la mgongo hilo na lile dude zito. Leo limeanguka hasara ngapi iliyoingia serikali. Nafikiri yule aliyepewa ile kazi atatulipa pesa zetu la si hivyo tutamshitaki. Hatuwezi kuvumilia kuona pesa kama zile zinapotea bure kitu ambacho Pemba walikuwa wanakililia, serikali imekubali kufanya halafu tunakuta kinakwenda ovyo. Hii ni ovyo, pale ni pahala penye maji.

*ZSSF* imejengwa pale pale ubavuni kwake, lakini huyo aliyekwenda kujenga *ZSSF* alipaona kama pana tope akafanya kuliko vile alivyokusudia na wenyewe *ZSSF* walikubali nasikia. Baada ya hiyo estimate aliyofanya aliwaambia hapa tunataka tupate mifuko 200 ya saruji tuanze kwanza chini msingi ili tuweze kunyanyua.

Lakini wenzetu waliojenga hili hawakulitizama hilo, *as a result* wametutia hasara tena hasara kubwa. Pesa zile mngetugaia hospitali wodi ya kina mama tukaifanyia kazi basi ingekuwa zile shilingi 40 elfu hatuchangishwi.

Mhe. Mwenyekiti, niwape pongezi kidogo watu wa Wizara ya Fedha, sio sana maana yake mgema akisifiwa tembo hutia maji. Niwaambie wamejitahidi, mwaka 1995 mishahara ilikuwa hupati baada ya miezi mitatu, lakini kuanzia Awamu ya Sita mishahara tunapata. Watu wanashukuru wanapata mishahara inakwenda vizuri, wamejitahidi, wameweka mambo yao vizuri. Vijana wamekaa, mwanangu Omar Kingi kule ana chumba chake cha mahesabu hicho kina kila kitu. Kwa hivyo, mambo yamekuwa mazuri *Alhamdulillah*.

Lakini tujitahidi yawe mazuri zaidi. Kwa sababu wananchi wetu wanalalamika hali ya maisha katika nchi hii ni ngumu. Maisha yamepanda marudufu na wengine hawana kitu chengine. Wengine ni wafanyabiashara, wengine wakulima, lakini kuna wafanyakazi serikalini, wanatakiwa kutwa waweko serikalini, mshahara mdogo. Mshahara kuanzia laki moja ukiifanyia hesabu kwa kutwa unatumia kiasi gani? Labda shilingi elfu tatu kwa siku ambapo upate laki moja kwa mwezi.

Sasa ikiwa ni hivyo, mtu yule kweli ana watoto ndani ya nyumba wanne mpaka watano na sisi Waswahili unajua tunavyozaa, watoto kumi unao ndani ya nyumba timu ya mpira. Una wa ndugu, jamaa na rafiki. Kweli zitamsaidia hizo, basi angalau mzivute vute mpaka laki na hamsini. Imewavunja moyo wafanyakazi sana kusikia mshahara haukuongezwa pameongezwa pencheni na hiyo pencheni yenyewe akitoka Makunduchi shilingi elifu kumi iliyoongezwa akaenda akirudi elfu sita imekatika, hajapata hata zawadi ya kununua akarudi nayo.

Kwa hivyo tujitahidini jamani, kila panapoonekana pana nafasi tupenyeze kidogo na wale wafanyakazi wetu wabaki watulie kazini. Kwa sababu kuna mtindo unakwenda kazini hukuti watu, mtu akishafanya hesabu ya shilingi elfu tatu ya kutwa haimtoshi anakimbia sasa, anakwenda kutafuta kuuza tungule huko sokoni au akatafute kitu chengine afanye ili ile *income* iongezeke. Sasa tukiwasaidia wataacha kukimbia na watabaki kazini watafanya kazi na taifa letu litapata kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, ukosefu wa umeme tuliambiwa hapa kwamba tulijipanga tukawa hatukupata hasara, tumejua tumefanya nini, si kweli. Ukosefu wa umeme miezi mitatu tulipata hasara kubwa sana. Sisi tulikwenda kutembelea Shirika la Uvuvi wakatwambia hii miezi mitatu kwenye asilimia mia moja tumetupa asilimia 70 kwa sababu ya ukosefu wa umeme. Silaumu kwa sababu jambo Mwenyezi Mungu akiliandika linakuwa tu hatuna vya kufanya, lakini tunaambiwa *tahadhar kabla-l-athar*.

Kweli juzi tuliambiwa hapa kuna majenereta yameshaletwa lakini yana *mega watt 25* sijui nini mnajua wataalamu. Sasa sijui ndugu zetu wa damu wakija wakinuna wakituzimia umeme kwa wiki moja kama litatutosha hilo. Leo bado tumekwenda kuunga tena kule kule Tanga-Pemba. Vizuri, lakini tuweke na akiba, akiba iliyowekwa ni ndogo, tena akiba hiyo isiwekwe Unguja tu bali iwekwe Unguja na Pemba.

Majenereta kama yananunuliwa yaongezwe, pakipatikana nafasi tuongezeni majenereta kwa sababu wakati wa kuzimwa umeme mwenye samaki wake kaoza friza halifanyi kazi. mwenye kuuza malai umeme hakuna, ilimradi

mambo madogo madogo mengi, ambayo yanachangia uchumi wa nchi hii, yalirudi chini kwa sababu tumekosa umeme. Yote yale kwa sababu hatukufikiri, mwanzo tuliona tutakaa siku zote, bila kutokea kitu kama hichi, lakini sasa tumeona na ukupigao ndio ukufunzao.

Sisi tumeshapata tatizo lile tumuombe Mwenyezi Mungu lisitutokee tena ili tukapata hasara tuliyokwisha kuipata. Mwenyezi Mungu *Inshaallah* atakuwa pamoja na sisi atatujaalia kwa amani hii tuliyonayo na imani tulizoziweka kwamba sote sasa hivi ni kitu kimoja. *Inshaallah* halitatokea jambo baya na tutakuwa pamoja na tutashauriana kama hivi tunavyoshauriana.

Kushauriana ni jambo muhimu na kuambiazana na mwenzako ukikaa kitako ukimsikiliza akikubali ushauri wako basi ameshapata thawabu kwanza kukubali ushauri. Lakini pia ameshatengeneza hataharibu tena. Kwa hivyo, nakuombeni tushirikiane tuwe kitu kimoja tujenge nchi yetu, tuacheni yote yaliyobakia. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atakuwa pamoja na sisi na nchi yetu itakuwa tajiri kuliko nchi tajiri. Kwa sababu sisi ni matajiri. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Asha Moh'd Hilal:** Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kupata nafasi hii na mimi kuichangia hii bajeti. Kwanza hongera kwa kupendeza na kiti chako.

Nitaanzia na bajeti. Bajeti ni nzuri, lakini bajeti sanifu au bajeti nzuri zaidi ni ile iliyoanzia michango kwa wananchi wa chini. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri mara nyengine tukiifanya bajeti yetu tuwahusishe na wananchi wa chini, wawe ndio waanzilishi wa hii bajeti. La msingi tuwaelimishe kwa kipindi hiki kabla, maana ya bajeti na hiyo bajeti yenyewe inatakiwa iwe vipi na inachangiwa vipi. Kwa hivyo, tutoe elimu hasa kwa makusudi mazima kuwafahamisha wananchi wa chini hii bajeti nao inawahusu na inabidi waichangie ili tupate kuwa na bajeti sanifu.

Nikija katika ukurasa wa 56 kwenye vizazi na vifo, kwa kweli Mhe. Waziri ametwambia zimeenea kompyuta za kuhifadhia hivi vizazi na vifo. Lakini hali halisi ilivyo hizi kompyuta nyingi ni mbovu. Mimi mwenyewe binafsi nimetembelea kule lakini hali si nzuri. Kuna mabuku yamenyambuka yote na bado tunayatumia, tunatafuta watu walipotelewa na tarjisi zao lakini hali ya mabuku yale ni mbaya kabisa. Magamba yote yametoka na baadhi ya kurasa zimepotea. Narudia kusema hii ni mara ya pili, nilikwenda kama mwezi mmoja nyuma hali bado iko vile vile. Nilisema bajeti iliyopita lakini na hii naisemea tena.

Ukienda ukiangalia ukurasa wa kwanza, wa pili, wa tatu haumo, wale watu wanakuwa hai lakini tayari tumeshawauwa kwa sababu mle hamna *data* zao zozote zinazoelezea zimepotea kabisa zile karatasi. Mhe. Mwenyekiti,

namuomba Mhe. Waziri pamoja na hizo kompyuta ambazo nyingi ni mbovu, lakini tungetafuta mabuku ya usajili tukafanya vizuri kwa kuweka zile *data* zetu mpaka tutapoweza kupata kompyuta za kutosha tukawatoa mule na kuwaingiza huko kwenye kompyuta.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa 76 malalamiko ya wafanyabiashara kutozwa kodi mara mbili Tanganyika. Hili tumeambiwa liko katika hali ya mazungumzo na ina mwelekeo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, namwambia Mhe. Waziri ukiacha kutozwa kodi kuna jengine jipya tena ni zito kuliko hilo la mwanzo. Kwa kawaida mapato yetu mengi tunapata kwa wafanyabiashara na mfanyabiashara jamani anachoka. Anatoka nje huko pengine keshapita *transit* nchi tatu au mbili, ametoka huko usiku wa jana, na usiku mwengine mpaka asubuhi au mchana ndio anafika Tanganyika. Kwa kweli hali ya kuchoka inakuwa kubwa sana.

Sasa ukifika pale mote dunia nzima ule mzigo wako ukitiwa *tag* una *land* kule unakokwenda isipokuwa hapa kwetu. Utatoka huko na *Emirate* au *Qattar* kwa sababu hizo ndizo zinazounganisha nchi za mbali, hizi za kawaida zinakuwa zinaishia hapa hapa karibu. Utatoka kucha mbili umefika pale mzigo umetiwa *tag* ya Zanzibar.

*Emirate* wao wamekubali kuunganisha. Kwa hivyo, ule mzigo pale hauhalisi kushuka kwa sababu una *tag* yake ya Zanzibar. Pale uingizwe kwenye *Precision* madhali alikubali uje kushuka huku. Sasa kilichokuwepo, wafanyabiashara kuna kitu kinaitwa kadi, kuna *green card* ina kilo 10, kuna *silver card* kilo 20 na *gold card* una *excess* ya kilo 30 mbali ya zile 50 zinakuwa 80. Kwa hivyo, ukifika Tanganyika mzigo ule unashushwa haidhuru una *tag* ya Zanzibar.

Pale kinachofanyika kilo 27 tu ndio wao wanachukua zilizobakia zote unalipa shilingi 3,500 kwa kila kilo moja. Mimi niligoma kulipa sikufichi Mhe. Mwenyekiti, na nikatikisa kweli kweli nikachukua mizigo yangu nikaondoka. Lakini kwa kweli wananchi wanapata tabu sana wafanyabiashara na ndio ambao tunawategemea kuingiza mapato yetu kwa asilimia fulani, sio kubwa sana lakini ni asilimia kubwa. Biashara imeshakufa Zanzibar na sasa hivi inazidi kuangamia kwa mfumo huu. Kweli hivi tutafika?

Mhe. Waziri kama hayupo Naibu Waziri ananisikia, unasinzia naibu waziri unanisikia. Kwa hili inabidi Mhe. Waziri akae na hawa *Emirate* pamoja na *Precision* kulizungumza hili, watatukimbia watu wote tutamalizika. Tumekwisha na sasa tutamalizika kwa hili. Kwa sababu hiki ndicho kilio kikubwa sana na ukimsikia mtu anayo *hand luggage* hiyo ndio inanusuru

angalau anapata *ticket* kulipa, *visa* na mambo mengine ya kuweza kujisaidia. Kwa sababu mzigo una mwezi hapo ndio unafika baada ya *packing* na kuja kufika kontena unautoaje.

Kwa hivyo, kwa hili lazima tulitizame kwa kina kuwanusuru wafanyabiashara wetu hao watatu wanne waliobakia.

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo. Mhe. Waziri nampongeza sana kwa kutuingizia na sisi huu Mfuko. Kwa sababu baadhi ya Wabunge walitaka kutesa kwenye majimbo kuwafanyia *competition* Wawakilishi, lakini madhali huu Mfuko upo na sisi *Alhamdulillah* japo mdogo lakini ndio upo. Tunakushukuru kwa hili.

Nije kwenye umeme. Kwa kweli tuna kilio kikubwa sisi Zanzibar kwa suala la umeme. Sijui Mhe. Waziri Kiongozi suala hili amefikia wapi. Nikiwa na kamati yangu nina masikitiko makubwa kwa wananchi wote wa Zanzibar, ikiwa Mhe. Rais tayari ameshatoa agizo watu wote wapewe *level* moja ya kulipa umeme sisi inakuwaje kuwekewa asilimia na zaidi mpaka kufikia pahala tunadaiwa shilingi 29.5 bilioni. Hii kweli ni haki?

Ukizingatia hii *TANESCO* ni yetu, wananchi wananisikia nawaeleza hakika kwamba hii *TANESCO* ni yetu, sisi mle tuna ubia na ndio waanzilishi. Leo hii wao wana-*join* sehemu tafauti, wanaingiza pesa sisi hawatujali chochote bila ya kutuambia au kutuarifu kama wame-*join* na sehemu nyengine au wameingiza pesa wanajichukulia na still sisi wanatuongezea, tukiuliza tunaambiwa *EURA*. Sisi huyo *EURA* ndiye tuliyetiliana naye mkataba? Mwisho tunatoka hapa sisi kwa *appointment* tunamfuata huyo Mhe. Ngeleja, tunafika anatukimbia anasema tuonane na Mulima. Sisi hatuna shida ya Mulima.

Mhe. Mwenyekiti, tuligoma kwa sababu hatukuwa na haja ya Mulima, sisi tulikuwa na haja ya Mhe. Ngeleja atueleze yote tuliyoyakusudia na yaliyomo mle kila siku yanayoandikwa kwenye barua hayafikii upeo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba hili utufafanulie na wananchi wajue mwelekeo wetu kuhusu huu umeme.

Nikiendelea nije kwenye ardhi. Mhe. Mwenyekiti, migogoro ya ardhi ni mingi na wanaofanyisha matatizo makubwa ya kugonganisha watu vichwa ni baadhi ya masheha, madiwani pamoja na hii Halmashauri. Hawa watu hawaeleweki wanacheza mchezo wa bingo, hawa wanakubaliana wanauza sehemu, wakishauza wakati huo huo wananchi tayari wameshapewa kibali wananchi walio chni kama vile wauza samaki. Wale ni watu wanaopata tabu sana, kila siku wanafukuzwa kutoka hapa kwenda hapa.

Mimi mwenyewe nafsi yangu ninao pale palipoandikwa bango kubwa la *Tigo* Viwanda vidogo vidogo. Wale walikuwa wanahangaika sana kila siku usumbufu, wakienda Halmashauri wakaomba wakapewa *document* na kila kitu, wakatitaza pale na mimi nikawasaidia, wakakaa vizuri katika hali ya salama, sasa hivi pamevamiwa panajengwa maduka. Maduka yale ukiuliza unaambiwa ya Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Nilimkabili mwenyewe kumuuliza Mhe. Waziri wa Maji, hivi Mhe. Waziri pahala kama pale palikuwa na mavi matupu wewe unapataka pale? Kwa sababu mimi nikipewa sipataki. Akanambia aah, hao wananizulia tu mimi simo. Nikafuatilia kwa Mkuu wa Mkoa tukamuuliza mpimaji akasema kapima kaambiwa wapewe wananchi. Kapigiwa Lupindo simu akasema hayo maduka ya Halmashauri tunajenga hapo na wao watabaki hapo hapo. Je, pale panajengwa magorofa wafanyabiashara wale wa samaki wataishia vipi?

Kwa sababu pahali penyewe si pakubwa na panajengwa majumba ya gorofa na pako kwenye korosi. Je, masikini ya Mungu kama wale pale palikuwa na maji pachafu, hapataki mtu, wamepashughulikia mimi mwenyewe nikawasaidia, wamepata pahala wamekaa wamestirika, wanachezeshwa mpira wa *Olympic* huku wanapigwa buti huku wanapigwa mpira, wataelekea wapi wale watu jamani na pale ndio wanapata riziki yao? Mbona tunawanyanyasa na hati wamepewa na kila kitu pale. Imekuwa pakishakuwa pazuri wanyonge wanaondoshwa wanatafutiwa sehemu nyengine, na wala hawajatafutiwa. Kwa kweli hivi tutakuwa hatufiki.

Ukilinganisha na hali halisi ya hivi sasa tunayokwendea sio vizuri, maisha magumu. Kwa hivyo, hapa nitamuomba Mhe. Waziri anifafanulie pale wale watu wangu mimi watapata stara ipi na watakuwa wapi. Wenyewe sasa hivi wananisikia kwa sababu niliwaambia nitasema, mimi pia wananichezesha mpira nikienda huku, huku, sielewi kitu.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumze kuhusu wazazi. Jamani uzazi mgumu, tena sana. Tumepiga kelele sote kwa pamoja wanawake na wanaume kikao kilichopita, ile ada ya wazazi iondoshwe kwa sababu dunia nzima uzazi na mzazi ni mali.

Uingereza anapewa *priority* kwanza mzazi na mtoto wake, watoto wote wanakuwa wa malkia sio wapofu wale. Wameupa kipaumbele uzazi kwa sababu una thamani na kinachozaliwa kinakuwa cha jamii. Kwa hivyo, na mimi naungana mkono na wenzangu hii asilimia kule jamani kwa masikitiko makubwa sana tunaomba iondoshwe. Mzazi anakuwa hana kitu mambo yote yanaturejea sisi.

Wewe ukitaka usitake na ukijua hali halisi ya mzazi hata kama saa saba utatoka ukamlipie mzazi ili apelekwe operesheni. Usipokwenda kule atakufa na mwanawe na yeye hatajua vipi, ataona ni wewe uliyekataa kwenda kule kumlipia. Jamani tujitahidi, Mhe. Waziri tunakuomba hii bora tuiondoe kabisa malalamiko yamezidi. Hivyo sote sisi tunasema ndio tunampigia gita mbuzi, huku anakula majani.

Kwa sababu mbuzi ukimpigia gita anakuwa hana habari kabisa anakula majani. Lakini tunakuomba Mhe. Waziri kwa hili hawa wazazi tuwasaidie. Kwa sababu kilio chao chote kinarudia kwetu na saa nyengine unakuwa hupo, hajalipa mtu yule anawekewa vikwazo na uzazi hauna muda na kila mtu na alivyojaaliwa huyu amaze vipi na huyu amaze vipi, kashindwa kuzaa kwa njia ya kawaida na operesheni hana vifaa ndio anafariki huyo.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo yangu machache. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Asha Moh'd Hilal kwa mchango wako huo. Sasa tumpishe Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa sababu ana shughuli nyengine anataka kwenda kuzifanya halafu Mhe. Ame Ussi Juma utakuja kuchangia baadaye.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii nikushukuru sana na kukupongeza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti. kwa sababu sijawahi kukuona kukaa hapo ndio kwanza leo. Sio kwamba nimekuwa mtoro sana, lakini majukumu yamekuwa mengi. Lakini nakupongeza sana kwa kazi jinsi unavyoiendesha.

Nimesema nikuombe nafasi hii ili niweze kuchangia kidogo kwa sababu kuna masuala fulani muhimu ambayo itabidi tukayafanye. Lakini nilikuwa nina wajibu kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi kwa namna alivyowasilisha bajeti. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Makunduchi natanguliza kuiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna alivyosimamia uendeshaji wa shughuli zote za kifedha pamoja na uendeshaji wa nchi.

Niwashukuru sana watendaji wote wa Wizara ya Fedha ambao wamekuwa wakitusaidia sana na kutekeleza wajibu wao mpaka yale mambo ambayo

yanahusu maendeleo  hasa ndio ambayo yamepewa kipaumbele zaidi. Nawashukuru sana. Hata jimboni nashukuru *Alhamdulillah* mambo si mabaya.

Nataka nichangie masuala mawili ambayo yamejitokeza hapa. Moja linalozungumzia suala la *quality* na *quantity of education*. Lakini la pili ni suala ambalo lilizungumzwa na Mhe. Ame Mati Wadi hasa suala la *ZATU* (Chama cha Waalimu). Naona bora nianze na hili la Chama cha Waalimu.

Mhe. Mwenyekiti, Chama cha Walimu tunakitambua, kimesajiliwa kihalali, kinafanya kazi nzuri, na kwa kweli tumekuwa na mashirikiano ya karibu kinyume na hayo ambayo nimeyasikia au niliyoyaona kwenye karatasi hiyo waliyotupa kwa kamati ya huduma za jamii.

Chama hiki mara kadhaa wametaka *appointment* ya kuja kuniona na kadiri walivyotaka *appointment* hizo nimeonana nao. Walikuja na kilio cha kwanza wakasema Mhe. Mwenyekiti tushirikishwe kwenye Sera ya Elimu, tulipokuwa tunaandaa Sera ya Elimu. Kwa hivyo, Mwenyekiti wa Chaka cha Walimu Ndugu Rabia tukamchagua miongoni mwa Wajumbe wa Sera ya Elimu akawemo. Kama vile haitoshi wakaniomba tena hii sheria ambayo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inataka kuipeleka basi na sisi tushirikishwe tutoe mchango wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikaagiza tukatoa *copy* tukawapa *document* ile tukawaambia katika wiki moja muweze kuirejesha. Nashukuru waliirejesha baada ya wiki nne au tano. Lakini baada ya kurejeshwa kuna mambo mawili au matatu ambayo waliyaongeza, ile sheria ilikuwa imeshafika katika vikao vya juu serikalini, ikabidi basi tuongeze na vile vipengele ambavyo walipendekeza. Yote hayo ni katika kujenga maelewano mazuri.

Suala moja ambalo lilikuwa gumu ambalo walilitaka na haliwezekani Mhe. Mwenyekiti, walitaka tuwashirikishe kwenye vikao vya kamati tendaji ya wizara. Wale wanaoshiriki kwenye kamati tendaji ya wizara ni wateule wa Rais, ZATU sio wateule wa Rais wanateuana wenyewe. Sasa hatuwezi kuwaingiza kwenye vikao vile na hatujui kwa nini wanatafuta nini? Kwa sababu kule hatukisemi ZATU, wala hatuzungumzi habari ya ZATU, tunazungumza maendeleo ya jumla ya elimu.

Mhe. Mwenyekiti, katika malalamiko yao mengi wamesema bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekuwa kama ni ripoti sio bajeti hasa. Sasa kwa bahati nzuri mimi sijawasilisha bajeti hiyo, mimi nitawapa *challenge* nitakaa nao wakiwa tayari waiandae bajeti waniletee nikae nao halafu tutizame ipi itakuwa ripoti ile yangu mimi au yao wao. Kwa sababu ripoti ya Wizara ya Elimu nadhani ni *one quarter* tu tunapata ile *text* yenyewe, *three quarter* ya

bajeti ni *statistics*. Sasa kama wanashindwa kuzisoma zile *statistics is not my problem,* kwa sababu zile ni takwimu za kitaalamu na zinahitaji kufafanuliwa kitaalamu na mimi niko tayari kusaidiana nao kama wakipenda hivyo.

Lakini tatizo moja walilolizungumza ni suala la marekebisho ya mishahara. Hiki ni kilio cha siku nyingi Mhe. Mwenyekiti, tumehangaika. Walikuja wakasema ni lini utawapa posho la asilimia 25, walipokuja ndio kipindi ambacho hakuna umeme. Sasa jamani kipaumbele tutowe asilimia 25 kwa walimu, au kipaumbele tutafute uwezekano wa kuwatafutia umeme wananchi wetu. Nikawaambia stahamilini mpaka umeme utakapowaka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri ZATU ni walimu ambao wengine wako kazini mpaka sasa hivi wanasomesha. Mwalimu mmoja akaniuliza unatupa tarehe maalum ya kutoa posho la asilimia 25. Nikasema hii kazi, nikamwambia hatuko mahakamani hapa. Lakini nakuhakikishieni kwamba umeme ukiwaka muda hautokuwa mrefu tutatoa.

Ninashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwaka umeme tu mwezi Machi basi mwezi Aprili asilimia 25 ikarejeshwa. Kama hilo basi halitoshi walimu wote ambao wamefanyakazi kwa zaidi ya miaka kumi, kumi na tano au ishirini na thelathini ambao nyongeza zao zilisimama tumewarejeshea. Walimu waliokuwa na uzoefu sasa hivi *they are been paid much better* kuliko wale walimu wapya.

Mhe. Mwenyekiti, yote haya tumeyafanya kwa maslahi ya walimu na mimi mwenyewe ni mwalimu na wengi humu tuliokuwemo ni walimu na tabu ya ualimu tunaijua. Serikali imejitahidi. Mimi nilitegemea ZATU wangeipongeza sana serikali, zaidi wanasema mshahara hautoshi. Kwani nani mshahara unamtosha? Kila siku tunaomba sisi tuzidishiwe mishahara hapa na pale. Hata wahudumu nyumbani wengine wanakuambia kila siku Shs. 20,000/= nifanyie Shs. 30,000/=. Ukimfanyia Shs. 30,000/= anakuambia nifanyie Shs. 40,000/= na mambo yanakwenda hivyo hivyo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hiki waliofanyiwa marekebisho haya ni walimu tu, kada nyengine zote zimeachwa. Katika kipindi hiki cha Mhe. Aman Karume marekebisho ya mishahara ya walimu yamefanywa mara mbili, ukiacha ya jumla yale ya kitaifa ya serikali. Walimu peke yake 2003 yalifanywa marekebisho ya mishahara ya walimu na leo mwaka 2010 tunapozungumza yamefanywa tena ya walimu. Lengo ni kuzidi kuwapa *incentive* walimu ili waweze kufanya kazi kwa moyo wao.

Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru nimefanya ziara mbali mbali, kila nilikokwenda basi walimu walipongeza. Tatizo lililojitokeza hapa, kabla ya

kutoa hizi asilimia 25 uliandaliwa waraka wa kutaka kusambazwa kwa walimu wote, kwamba watie saini ili kuishinikiza serikali kwamba wadai ilipe asilimia 25. Nilishangaa sana, ZATU ina wanachama wasiozidi 3,000, walimu wote tuliokuwa nao ni 14,000. Kwa hivyo, walitaka hata wale walimu wasiokuwa wanachama nao watie saini *that was unfair*. Tukasema sisi mwalimu yeyote ambaye sio mwanachama wa ZATU hatoruhusiwa kutia saini kitu hicho. Kama kuna malalamiko basi yafuate taratibu za kawaida, tuandikiane barua ili tuweze kutatua. Hawakulipenda.

Mhe. Mwenyekiti, tayari serikali miaka miwili iliyopita Rais Aman Karume alikuwa keshatoa tamko kwamba atarejesha asilimia 25, lakini ZATU wakasisitiza kwamba lazima litekelezwe. Pamoja na hayo yote serikali ilikuwa haijasema kama haitotekeleza, lakini tukaweza kulitekeleza hilo.

Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli asilimia kubwa ya walimu wameridhika. Hata kwenye risala zao unapokwenda huko unawasikia wakishukuru kwamba wanapongeza kwa hatua iliyochukua serikali. Mimi naomba nichukuwe nafasi hii kwa dhati kabisa katika hali hii, kwamba tulikosa umeme miezi mitatu na matumizi makubwa ya bilioni ya fedha na bado Wizara ya Fedha na Uchumi ikaweza kufanya utaratibu, kwa kushirikiana na Idara ya Utumishi wakaruhusu walimu walipwe asilimia 25 yao pamoja na nyongeza zao ambazo walistahiki kulipwa kutokana na uzoefu wao. Nawashukuruni sana Wizara ya Fedha pamoja na Waziri wa Fedha na Uchumi kwa kazi hiyo nzuri mliotufanyia.

Jengine ambalo tumesingiziwa. Mhe. Mwenyekiti, ni lazima niseme kuwa tumesingiziwa na hii ni *acquisition* kubwa sana ambayo imo kwenye hii ripoti yao, ambayo Makamu Mwenyekiti wa Huduma za Jamii amenipa. Inasema "michango ya wanafunzi skuli inachukuliwa na wizara kwa kupitia milango ya nyuma".

Mhe. Mwenyekiti, hii ni *acquisition* kubwa sana na tusingependa liishie hivi hivi, kwa sababu hizi ni tuhuma nzito. Wakati Baraza hili hili na kama sikosei Mhe. Aziza Nabahan au mwengine ni miaka miwili iliyopita, simkumbuki vizuri ni mheshimiwa gani. Alisema jamani Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali hata hii asilimia 10 hamuwaonei huruma walimu mkawaachia. Nikatangaza siku ile na kwenye bajeti yangu nilipofanya majumuisho, kwamba si ruhusa kwa idara au taasisi yoyote ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuchukua sehemu yoyote ya mapato yanayopatikana skuli kule. Kwa hivyo, hakuna hata shilingi moja ambayo inaingia kwenye mfuko mkuu wa wizara. Pesa hizi zote ambazo zimetajwa zinakusanywa na walimu wenyewe wanatumia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu wote wa Unguja na Pemba pamoja na kamati za skuli. Hayo madarasa ambayo yanajengwa huko ni kutokana na michango kama hii ambayo inachangiwa. Kwa hivyo, naomba niwapongeze na kuwatakia heri *inshaallah* katika uchaguzi unaokuja.

Mhe. Mwenyekiti, wamechukulia wanafunzi tuliokuwa nao wote. Mfano wote ni wanafunzi 200,000 na wote wanachangia. *Primary*, *Secondary* tuna wanafunzi 150,000 wote wanachangia. Kwa hivyo zimekuja *data* kama ndio tunakusanya pesa hizo. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, wazee na wananchi hawana uwezo wa kuchangia. Pesa ambazo zinapatikana ni chini ya asilimia 30, hata hicho ambacho kinakisiwa kitumike ni wananunua chaki na kusaidia mambo ya ununuzi wa saruji na mambo mengine Mhe. Mwenyekiti, kwa skuli zao. Kwa hivyo, hisi takwimu ukiziona zinapendaza, na tutaonekana tunakusanya pesa nyingi sana, lakini ukweli sio hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ambayo bahati nzuri nimesimama mimi kwa miaka kumi, tumejitahidi sana kudhibiti masuala yote ya fedha katika wizara hii. Ndio maana yake tukasema hapana, wananchi wenyewe wanachanga pesa na wazee wanachanga pesa basi pesa hizi zibakie skuli. Kwa hivyo, hatuchukuwi hata shilingi moja. Isipokuwa katika siku ya walimu duniani, walimu wanatakiwa wachangie Shs. 1,000/= na hizo ndizo ambazo zinachukuliwa na baadae pesa hizo hizo wanarejeshewa wenyewe wale wafanyakazi bora au walimu bora. Sasa hili ni jambo la hiyari na nina sikitika sana kwamba hizi *data* ambazo zimetolewa zilikuwa zina *acquisition* ambayo kwa kweli sio nzuri. Lakini sisi ni viongozi tunatakiwa tuwe na vifua vya kustahamili na tutayastahamilia *Inshaallah.*

Jengine ambalo ningependa kulizungumza, rafiki yangu Sheikh Rashid Seif Suleiman hayupo, anapiga rakaa mbili kule na faradhi. Alizungumza suala la kwamba bado tunakwenda kwenye *quantity.* Katika mazingira ya nchi kama yetu isingekuwa jambo la busara kwamba tukawaacha watoto kukosa elimu kwa sababu ya kuhofia labda tutakosa *quality*. Kwa hivyo, ni kweli tumekuwa tukichukua watoto wote waliokuwa wametimia umri wa kwenda skuli, tunajitahidi kuwachukua, tunaendelea kuwachuku na tutaendelea kuawachukuwa kwa sababu wacha waingie darasani watapata elimu.

Mhe. Mwenyekiti, hatuja-*loose* pamoja na kwamba magazeti yalituandika kwamba tumefanya vibaya. Mimi nashangaa sijui tumefanya vibaya kwa kiasi gani? Mwaka jana tulifanya vizuri sana, sikuona gazeti likitupongeza, lakini haina tatizo. Angalau hili la mwaka huu kuna skuli binafsi mbili zimefanya vibaya na moja ya serikali katika mitihani ya *form six.* Mhe. Mwenyekiti,

unaweza kuwa na vizuri 20 ukaambiwa hebu chagua kidogo kilichokuwa kibaya katika hivi vizuri 20 utapata, na katika vibaya 20 basi unaweza ukatafuta kizuri kimoja ukakipata au viwili.

Mhe. Mwenyekiti, nina hakika kwamba matokeo yetu ya mwaka huu yalikuwa ni mazuri na ndio maana idadi ya wanafunzi walioingia *form five*, ukitizama mwaka 2000 walikuwa chini ya wanafunzi 600. Leo hii wanafunzi walioingia *form five* wamefika 1965. Miaka ya 1970 hadi 1980 Mhe. Mwenyekiti, *form five* ilikuwa tunakusanyana darasa moja halitimii, si Castro wala si Lumumba. Wakakopeshwa wanafunzi hapa *credit* moja badala ya tatu, basi wakakopeshwa ili waingie *form five* basi darasa lilikuwa halijai. Leo tumefungua *form five* katika skuli 13 kwa sababu wanafunzi wanafaulu vizuri sana, tena ni za vijijini na mijini.

Sasa pamoja na kwamba kweli kuna suala la *quantity*, lakini sio kuwa tumeliwacha suala la *quality*. Limezungumzwa suala la *training* ya walimu na hata ZATU wamelizungumza. Kama wanafuatilia kwa makini tunatoa taarifa na Mkurugenzi wangu wa Mafunzo ya Ualimu Maalim Shaaban, mimi nampongeza sana tokea amekua Mkurugenzi pale amefanya kazi nzuri sana, programu alizoziandaa za ualimu. Hivi sasa kuna programu za walimu wa sayansi kila mwaka kwa ajili ya kuwaandaa walimu wa darasa la tano na sita, ili waweze kusomesha kwa kutumia lugha ya Kiingereza, walimu 500 tunawaandaa.

Mhe. Mwenyekiti, tumewapeleka walimu nje ya nchi kwenda kupata mafunzo. Walimu wakuu wamekwenda nje ya nchi karibu 20 tuliwapeleka India, kuna walimu ambao wamepata mafunzo ya nchi wamekwenda Dar es Salaam na wengine wamekwenda nje ya nchi kwa mafunzo mbali mbali, wanaochukua digrii ya kwanza, ya pili na ya tatu. Sasa serikali inajitahidi sana na ninawaomba ZATU wawe karibu na sisi ili tuwape hizo takwimu waweze kuzijua. Sasa kwenye bajeti yangu wakitizama hizo takwimu za walimu wote waliopatiwa mafunzo wataziona, wasitizame ile *text, text is nothing* kwa sababu sisi tunaendeshwa na takwimu zile ndizo zinazofanya kazi, hatuwezi kutoa *text* tupu bila ya kutoa takwimu.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani katika historia ya wajumbe waliokuwemo katika Baraza hili wanajua kwamba bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ukitizama sehemu ya *text* inakuwa ndogo na takwimu zinakuwa nyingi. Kwa sababu hata idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo inaonekana ndani yake.

Kwa hivyo, naomba kusisitiza kwa ndugu zetu wa ZATU na maalim wangu Mhe. Rashid Seif Suleiman, wasione kwamba tunachukua *quantity* tu, lakini vile vile tunajitahidi kuangalia *quality* ndio maana tumetafuta vitabu na

tumevisambaza. Juzi tu *Alhamdullilah* tumesaini na ndugu zetu wa Marekani *MOU* pale watatupatika karibu *20 millions dollars.* Ni kama wiki moja na nusu iliyopita tu nadhani au siku kumi, kwa ajili ya kutayarisha vitabu vipya ya *primary* darasa la kwanza hadi la nne. Mitaala tayari imeshatayarishwa, skuli zote za Unguja na Pemba zitaunganishwa na *internet.* Mazungumzo yangu na Balozi sasa hivi tunakoelekea ni kwamba kila mwanafunzi mmoja wa Zanzibar basi awe na kompyuta yake, ambayo ataweza kuitumia pale darasani na kuweza kuichukua nyumbani kwa ajili ya mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hapo ndipo tunapoendeleza hiyo *quality* yenyewe. *Library* zetu tunaziimarisha. Juzi nilikuwa Oman tumepata misaada ya ma-*carton* ya vitabu vinafika 43 ni zaidi ya vitabu karibu 12,000 Mhe. Mwenyekiti, yote haya tunahangaika huku na huko kutafuta juhudi za kuweza kuwaendeleza vijana wetu.

Kwa hivyo, pale pakushukuriwa basi tushukuriwe na pale pakuelekezwa basi tuelekezwe kwa utaratibu ambao unafaa. Mimi sikatai *criticism* na kila ukini-*criticize* basi kwangu mimi ni *challenge* na inaweza kunisaidia kutekeleza majukumu yangu ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niiunge mkono tena hii hoja na nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya upendeleo na uendelee kunipa nafasi ya upendeleo. Ahsante sana.

**Mhe. Ame Ussi Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa jioni hii kupata fursa ya kuweza kuchangia bajeti ya serikali. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote, wakiwemo Wakurugenzi, Makatibu Wakuu na maafisa kwa juhudi ambazo wamepoteza muda wako kwa kuweza kutafuta mbinu ili zituwezesha katika Serikali yetu ya Mapinduzi. Kwa dhati kabisa nawapongeza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaelekea katika kitabu kwenye utekelezaji halisi wa mwelekeo wa sera za CCM za mwaka 2000/10. Katika kipindi chote hicho kuna takwimu ambazo zimeelezwa humu asilimia zilizopatikana kwa utekelezaji wa Chama cha Mapinduzi, mimi napongeza.

Pia katika utekelezaji huo lazima Mhe. Mwenyekiti, tukubali kwamba na kasoro zitakuwepo, hasa za mfumko wa bei ndani ya kipindi hicho cha utekelezaji wa sera, hayo yametokezea utekelezaji wa sera hizo katika maendeleo ya watu. Pia imekuwa ni changamoto kubwa sana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tuelewe kwamba mfumko wa bei ndio ulioathiri serikali watu au jamii nzima, sana ukilinganisha na kipato cha yule mtu wa chini ambacho anakua anakipata siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, katika bei za bidhaa ambazo zimeongezeka au zinapanda mara kwa mara ni sawa sawa na madawa, mafuta, vyakula na kadhalika. Hivyo basi serikali iangalie kwa makini zaidi katika kujipanga na kuona kwamba je, kasoro hizo kwa mara hii au kwa bajeti hii na hapa tunapoendelea hazitatokea.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imefanikiwa kusambaza umeme katika vijiji 141 kama ilivyo katika kitabu hiki. Hiyo ni faida kubwa sana na ni mafanikio. Umeme huo upo kwa Unguja na Pemba hili nalipongeza. Lakini bado kuna taarifa za tathmini ambayo labda serikali inaelewa au haielewi, hasa ukizingatia kwa upande wa huduma zaidi kwenye mazingira, afya na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili la kuangalia mazingira na afya kwa pande zote, suala hili katika mchanganuo linamgusa mwanamke na mwanamme. Kwa hivyo, nafikiri na hapa serikali zaidi ingetowa uwezeshaji wa maelekezo, wapi ambapo usimamizi wa karibu utafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, katika takwimu mimi napongeza kwamba utafiti wa mapato umefanyika kwa matumzi ya kaya sensa ya kilimo, sensa ya uzalishaji viwanda na utafiti wa hali ya uchumi zimefanyika. Mhe. Mwenyekiti, basi tungeona kwamba katika hoja hizi kuna tofauti zote zilizozingatia kufanya tathmini ya uchambuzi, ni kwamba masuala ambayo yanahusu jinsi basi nayo ingebidi kupewa kipaumbele, ikaonekana kwamba jinsia kama walivyozungumza wenzangu wengi hasa kwa upande wa kina mama tukaona mwanamama anawezeshwa ili kumudu yale matatizo ambayo anayakabili nyumbani. Ni kweli wanaume tunapangusa mifuko tukiambiwa hatuna. Sasa basi pangewekwa na mkazo katika suala hili kwamba ili kuondoa zile biashara ndogo ndogo wakapewa kina mama katika ile mifuko ya uwezeshaji.

Vile vile tukiangalia takwimu zingemlenga zaidi yule mtu wa kijijini. Maana mtu wa kijijini na mtu wa mjini ni tofauti sana matumizi yao. Yule mtu wa kijijini ambaye ndiye anayetafuta matumizi wakati mwengine au anayetafuta kipato, hasa kwenye kilimo kuweza kuuza kule mjini. Sasa yeye yule huwa anahangaika sana.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu ingekuwa tumetilia mkazo suala la kilimo katika bajeti hii, basi napo tungeona kwamba maeneo gani yanaweza yakafanikiwa katika ukulima wa mpunga na maeneo gani yanaweza kufanikiwa katika ukulima wa vitu vile vinavyohusika na maweni kama mbaazi, mahindi, mtama na viazi vikuu. Kwa hivyo, ingekuwemo humu nayo ili kutilia mkazo zaidi ya vilivyo hivi ili tukajua kwamba kweli takwimu zetu zimezingatia mpaka kule vijijini. Kwa sababu vijijini pia kuna sekta mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamesema kwamba kuna uvuvi. Hasa kule Kaskazini Mhe. Juma Duni alisema jana kwamba yeye kwao Mkwajuni, anaweza akashindana na Mhe. Haji Omar Kheir kwa kuvua. Lakini ukiangalia na kule Nungwi ni hivyo hivyo, kutokana na vijiji vya Nungwi, Tazari, Kilimani na Kigunda navyo vimezungukwa na bahari, ukija huku urejua na uchejua vile vile bahari imewazunguka. Kwa hivyo, basi tungeona zile zana za bahari zikapewa kipaumbele zaidi, ili kuwapa uwezo wale kwa sababu hivi sasa bado wanaweza wakatumia zile zile zana ambazo zimekatazwa. Kwa kweli kama unamkataza mtu kitu kwamba kinaharibu mazingira basi mpe kile ambacho anaweza akatumia kisiharibu mazingira.

Kwa mfano hivi sasa wavuvi hawana vifaa kama boti zile zinazokwenda bahari kuu kuvua, isipokuwa wana uvuvi ule ule tu wa kizamani. Nafikiri na serikali nayo ingetupia macho kwa masuala haya ya uvuvi hasa kwa kanda zile.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Aziza Nabahan alizungumza hapa kwamba kuna meli zimepewa vibali. Mimi nakubaliana naye kwamba kweli kuna meli zinakuja na zinavua katika sehemu zile za mnemba na karibu ya Pemba kule, kwa sababu wavuvi wetu wengi wanakwenda kule na wanakutana nao hao. Sasa na wale wetu basi wapewe vyombo vikubwa ili waweze kufika kule wanakovua wale na wao waweze kupata yale mapato yao waweze kuja kuuza na serikali ndio inakusanya humo humo katika madiko. Kwa hivyo, na hili ingekuwa limetiliwa mkazo basi wale wa vijijini wangejua kwamba tayari na sisi tumeonekana kuwa tunaweza tukafanya kazi hizo pasi na pingamizi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine serikali ingeweza kutafuta soko la mwani, kwa sababu soko la mwani bado linasumbua sana. Wakulima wetu wa mwani bado bei ya mwani ni ndogo hairidhishi kabisa. Mhe. Mwenyekiti, mwani una kazi sana unapanda na unapovuna kwa viroba, Bara wanaita viroba na sisi tunaita vipolo. Kwa hivyo, inabidi wewe utowe kwenye maji kule mpaka juu uanike. Siku moja unaweza pengine ukabeba vipolo kumi au kumi na tano, ukifika nyumbani wewe mwanamke ni kulala tu tena, huwezi kugeuka kulia wala kushoto. Kwa hivyo, hili nalo lingeonekana ni lazima suala hili serikali iangalie na takwimu zifanyike kwa uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba mimi kwenye kitabu hiki kwa sababu wengi wamechangia mengi sana. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nungwi naunga mkono mia juu ya mia ahsante sana.

**Mhe. Najma Khalfan Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi jioni hii kupata nafasi ya kuchangia japo kidogo bajeti hii ya serikali. Mimi nimesoma ndani ya kitabu, kwa hivyo nimeweka mambo yangu yote kwa jumla jumla tu.

Mhe. Mwenyekiti, naanza kuchangia bajeti hii kwa kuwatazama wafanyakazi. Ninavyoelewa mimi kuwa bajeti kuu ya serikali inaposomwa dunia nzima, basi wafanyakazi wote masikio yao huwa juu kusikiliza vyombo vya habari, leo serikali itatufanyia nini? Jambo moja ambalo wanalisikiliza wafanyakazi ni kuongezwa kima cha mshahara. Hata bajeti za wenzetu majirani zetu Tanzania Bara, majirani zetu wengine Kenya na Uganda, basi wafanyakazi wote wamefanyiwa vizuri, isipokuwa wafanyakazi wa Zanzibar tu wao wako pale pale na laki yao moja kama wengine wameshapata hiyo laki moja sijui.

Kwa hivyo, wafanyakazi wana kilio wanaona serikali yao haikuwatazama, kwa nini wasiwaongeze pesa kidogo angalau wakafikia Shs. 200,000/= kutokana na hali ya maisha ilivyo. Kama haiwezekani Shs. 200,000/= basi japo Shs. 150,000/= kutokana na hali ilivyo. Kwa hivyo, suala hili serikali ilitizame japo kwa kuwaongezea kimya kimya bila ya kutangaza, maana kutangaza nako saa nyengine kuna matatizo yake. Lakini wafanyakazi waongezewe japo kimya kimya.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili la mshahara mdogo linatuumiza kwa kweli hapa Zanzibar, kwa sababu na wasomi nao wanatukimbia. Sasa bajeti hii sijaisikia itawabakisha vipi wasomi hapa Zanzibar wasitukimbie kutokana na mshahara mdogo. Utakuja kuniambia pengine waliokuwa wameondoka hawana uzalendo, sio kweli. Kuna watu hapa wamefanyakazi sio chini ya miaka 20 lakini baadae kutokana na maslahi wanavyoyaona kidogo wameondoka, wakiwaona wenzao wenye daraja lile lile au chini yao wanapata mshahara mzuri. Binadamu wanafanyakazi kwa sababu wapate maslahi, sote tunafanyakazi kwa sababu ya kutafuta maslahi, bila ya maslahi huwezi kufanyakazi vizuri.

Kwa hivyo, sikuisikia bajeti itafanya nini juu ya kuwazuia wasomi wetu wasitukimbie. Sisi tunasomesha sana. Lakini inasikitisha sana kwamba wasomi wa Zanzibar wameenea dunia nzima hivi sasa, tumekuwa jivuli la mvumo, tunafunika walio mbali tuliokaribu tunapigwa na jua. Sasa hili si jambo zuri kwa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwa wafanyabiashara. Wafanyabiashara Mhe. Mwenyekiti, wako wa aina nyingi hapa Zanzibar na dunia nzima ndivyo walivyo. Kuna wafanyabiashara wadogo wadogo na kuna wafanyabiashara wa kati, kuna wafanyabiashara wale wa chini wanaouza tungule, mboga mboga na samaki. Lakini hawa wote kwa pamoja wanachangia pato la taifa. Sasa wafanyabiashara wakubwa wao wanasafiri wanakwenda nje kuchukua biashara, halafu wanazileta hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, miezi ya kutumia sisi Wazanzibari mara nyingi inakuwa ni huu mwezi wa Rajab, Shaaban na Ramadhani kwa sababu mbele kuna skukuu.

SACOS wote na wacheza upatu wote huko, kina mama siye maana tuna mambo yetu ya kupata pesa, watu wa mwani wote, watu wa mboga mboga na mamantilie wote pesa zao zinakuja kutumika katika miezi hii mitatu, kwa sababu ya kuwatengenezea watoto sikukuu. lakini ushuru unakuwa mkubwa mtu anakwenda dukani anaiuliza nguo mara tatu, anaitaka kwa ajili mwanawe ampendezeshe, inamshinda kutokana na bei, ukiwaliza wafanya biashara mbona hivi? Wanakwambia sisi hatuna tatizo tukipunguziwa ushuru sasa hivi basi kila kitu kitakuwa murua hapa.

Sasa tunaiomba serikali katika miezi hii narudia tena mwaka jana nilisema na mwaka huu nimesema, tukiingia katika miezi hii tuanze kupunguza kidogo ushuru ili wananchi wetu wamudu kununua nguo pamoja na kununua futari. Tunashindwa wakati wa Ramadhani unajua tena futari za Kizanzibar mtu kama hajapata muhogo na samaki mwingi, akapata vitobwesha maneno ya Mhe. Zakia hapa au vipopoo, makoroni ndio utamaduni mpya mradi janvi likachafuliwa na tuna tabia ya kufutarisha tunashindwa kwa sababu kila kitu kinapanda bei. Lakini kinapanda bei ukiwauliza wanakwambia na serikalini bei juu! Kwa hivyo hapa serikali tunataka ituwekee wazi miezi ikifika mpaka Ramadhani teremsheni ushuru ndogo ndogo nyingi kuliko kubwa moja.

Hapa ukipata ushuru ukipata hapa kidogo na hapa kidogo zinakuwa nyingi hebu tuwafanye wafanya biashara walipe wenyewe kwa hiari zao tusiwafanye walipe kwa maguvu, kwa sababu kwa hiari ni kufanya ushuru kuwa mdogo kwa hivyo mfanya biashara mwenyewe atakuwa na hamu ya kulipa. Sasa tutapata nyingi kwa kuzikusanya kidogo kidogo tutapata nyingi lakini tukisema tunataka kikubwa kwa pamoja tumchinje bata siku hiyo hiyo tupate mayai ya zahabu yote yaliyomo ndani ya tumbo lake tutashindwa hatuyapati. Hebu na tuwe na siasa za kihindi, wao shilingi tu ni kubwa kwake anafanya shilingi na shilingi zinaongezeka , lakini sasa sisi tunataka tupate mamilioni kwa wakati mmoja hapa tunashindwa watu wetu hawana kipato kikubwa kiasi hicho.

Halafu kuna hawa wenzangu mimi wa biashara ndogo ndogo hawa wauza sokoni, wauza samaki na mboga mboga. Jamani hawa kila wanapokaa sisi tunawatimua tunataka wakapate wapi rizki zao? Na ndio wengi, hawa ni Wazanzibar wenzetu hawana pa kwenda isipokuwa Zanzibar ndio pao, leo wapo soko la mboga wameshatimuliwa! Walijaa tele hapa Mhe. Mwenyekiti wauza mboga mboga walikuja Baraza la Wawakilishi. Wanajua hawana pengine pakwenda kwa ajili ya kulia isipokuwa waje Baraza la Wawakilishi watoe kilio chao ili wasikilikane tumeshawafukuza pale, tumeshatia uzio wa mabati soko la mboga na sehemu ya kuku kule tumeshatia uzio akina mama ntilie na wengine wapo miaka mingi sana hatukuwapa pahala pengine pa kwenda. Sasa tunataka weende wapi hawa? Wakaibe! Wakiiba wapelekwe

Madema wakafungwe! Watu na watoto wao na wengine hawajui mila za kuiba.

Sasa hawa wote tunawafanya nini na maisha yao tunayapeleka wapi? Tusiwatizame wafanya biashara wakubwa tu, tusiwatizame wawekezaji kutoka nje na tuwatizame na hawa wetu tunawapeleka wapi hawa leo, hawa hawa huwa tunapita tukakusanya kodi japo pesa mbili mbili lakini wanachangia katika serikali. Sasa leo tumeshawatimua hawa niambie hiyo shilingi mia utaipata wapi na umeshawatimua sasa hawa kama wameondoshwa pale panataka kufanywa maendeleo si vibaya basi na watafutiwe pahala lakini pakimaliza pale wajengewe vibaraza vyao, huyo atakayejenga awajengee na vibaraza vyao pakusanywe kodi ya serikali kama pameuzwa pajulikane lakini hawa warudishwe kwa sababu hawana pengine pa kwenda, ili waweze kuuza biashara zao serikali ipate na wao wapate.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwa hawa wasafirishaji wakubwa wanaokwenda nje kununua nguo hawa, hawa wakishapanda ndege kama *Ethiopia Air Line*, *Emirate, Kenya AirWays* wakati mwengine tabu inayowafika wafanya biashara wetu wanatulia Dar es Salaam, wakitua pale tu sio wafanya biashara wote wanaopata mizigo yao vibaya kutaja mashirika ya watu ni kuua biashaa lakini itabidi tuseme. Shirika kama *Ethiopia Air Line* mwaka jana karibu na Ramadhani ndege ilitua pale wafanyabiashara mpaka kufika Zanzibar mizigo yao haimo sio mmoja wala wawili wala sio watatu mpaka leo hawajapata kulipwa katika shirika hili. Tunaomba waziri anayehusika ashughulikie hili kwa sababu hawa ni walipa kodi wetu, sasa biashara zao zikishachukuliwa huko Dar es Salaam hazikuonekana tena watapata wapi kodi ya kuilipa serikali hawa na wamepewa tiketi wamesafiri na wamekwenda na kurudi huu ni mwaka sasa *Ethiopia Air Line* bado haijawalipa jamani wasaidieni wafanya biashara hawa waliobakia wawili watatu wasitukimbie.

Mhe. Mwenyekiti wakulima bado jamani, wakulima wa Zanzibar hatujajua kulimia hizo *glass* na vifaa vyengine, ukulima wetu ndio huu huu vijembe kongoroka tia mpini lakini hawa wanatakiwa wabadilike katika kulima. Mimi nilifundishwa skuli ukitaka kupanda mgomba tatu kwa tatu, tatu kupanda tatu kwenda chini utie mbolea hivi na hivi halafu ndio upande mgomba. Mimi najua lakini mkulima mdogo huko kwetu hajui kwa sababu hakwenda hata skuli pengine, sasa kama hakwenda kusimamiza na huyu bwana shamba atajuaje?

Sasa leo Mhe. Waziri anatuletea sijui matrekta ya kuvunia liko wapi hilo eneo la kufanya yote hayo, wakulima sasa hivi wanatakiwa kubalika kutoka kilimo cha zamani waingie cha kisasa tuwaleteeni basi japo matrekta madogo madogo yale ya mikono ili wamudu hata katika mtaa kama wenyewe watachangishana wataweza kununua na serikali itawasaidia. Vile vile katika ukulimi huu wa

kutegemea mvua umeshapitwa na wakati ingawa ndio tunaotegemea hiyo mvua yenyewe ndio inayoleta maji huko chini, lakini kilimo cha umwagiliaji kipewe msukumo nimeona humu ni Bubwisudi sijui na wapi ndio wana kilimo hasa cha umwagiliaji, maji mabonde mengine yaliyobakia hawana kilimo cha umwagiliaji maji tunawapeleka wapi hawa kweli tutakomboka kwa namna hii, kwa nini serikali hivi sasa kwa kuwasaidia wanawake kwa sababu ndio wengi wakulima haifanyi mipango ya kututilia mifereji katika mashamba.

Hakuna kitu kinachonichukiza kama kuchukua tungule bara kuja hapa. Mhe. Ame Mati halimi tena tungule ana utalii na utalii na yeye, sasa hivi tungule zote zinatoka bara zinaingia hapa hao wakulima wetu wanafaidika vipi na huo utalii ukitizama hakuna wanachofaidika. Lakini tuna mabonde mazuri kule kwetu kuna mabonde ya Ole, kuna mabonde ya Chambani, kuna mabonde ya Pujini lakini na hapa Unguja yapo kuna Kilombero na sehemu nyengine sasa wanataka maji hawa. Kwasababu ukipita humo kwenye mabonde walioinamisha migongo wanapalia na kulinda ndege ni wanawake watupu, mmoja mmoja katika wanawake kumi au kumi na tano mpaka ishirini ndio utakuta mwanamme mmoja na huyo pengine kenda kumpelekea mkewe chai ndio kaambiwa nikamatie mara moja, lakini wanawake wote ndio wakulima.

Sasa huu mpango wa kulima kwa nguvu nyingi tumeshachoka sie kutumia nguvu nyingi bila ya tij,a tutilieni mifereji humo mashambani tumwagilie tumeshachoka kulima kilimo tusichopata, kulima nnakwisha kuvuna panatosha hicho ni Kiswahili cha kwetu. Maana yeke ni kwamba nalima *pankwisha* maana yake nalima hapa mpaka pale, navuna pantosha maana yake huna kitu. Kwa hivyo tufanyie kilimo cha kisasa cha zana ndogo ndogo ambacho tutakimudu.

Vile vile tubunini mazao mengine ya biashara jamaa zangu wa Kipemba meli ikija pale siku zote huna hata siku moja meli isiyojaa ndizi hakuna. Sasa tuzifanye hizi ndizi kwa Zanzibar tumeona inawezekana basi tufanye kilimo cha ndizi kiwe cha biashara hebu tufanyeni kwa makusudi kabisa. Wizara ya Fedha na Uchumi ikishirikiana na Wizara ya Kilimo Mifugo na Mazingira zao jipya la biashara ndizi tuweze kuzisafirisha nje, wenzetu kule wana ndizi za mtwike na kiguruwe tu tunafikiri ndio wanazokula hebu tuzifanye ziwe ndio zao la biashara, tuzipeleke nje tuziuze tupate pesa.

Mhe. Mwenyekiti halafu kuna huu mkarafuu unaonekana haukupewa haki yake inaonekana kama serikali hautaki taki hivi umeupuuza puuza. Wakati mmoja karafuu zilipopanda bei na mimi ni Mpemba ninayo mikarafuu mabondeni huko tulikuwa tukiona watu wakipishana panga mkononi watu wanataka kugawana mikarafuu, hata wale walioipuuza wakasema hatutaki urithi basi kwa kuwa mikarafuu yenyewe haina tija. Wakati karafuu zilipopanda bei basi

ilikuwa panga mkononi tukagawane wanawake wamekazana kama nini na mimi nataka yangu japo kumi, ilipoteremka na wao wakaa kitako.

Sasa ikiwa hizi karafuu hazina bei tena jamani hebu tuwaachie wenyewe wakulima basi wailime wenyewe, wavune wenyewe na wauze wenyewe na serikali isimamie kodi yake na mkulima asidhulumiwe haki yake basi tuone huyu mkulima ataishughulikia mikarafuu yake au hatoishughulikia, kuliko kuiacha mikarafuu tukawa sisi na utalii na utalia. Utalii wenyewe kukichakarika tu kidogo watalii hawaji tena, kwao kumeporomoka kiuchumi hawaji tena kama inavyotakiwa, sasa sisi tusitegemee watu huu unawakuwa wakutegemea watu una hasara yake tutizame na hizi rasilimali alizotupa mwenyezi Mungu tuone zitatupeleka vipi kiuchumi katika nchi yetu hii ndogo.

Mhe. Spika, sasa nakuja kwenye ufugaji sijasikia huku kama kuna chochocte kilichosemwa katika ufugaji, ufugaji wa kuku Zanzibar umekufa kabisa sasa hivi nashukuru ule mradi wa kilimo SSPL sijui kama hivi ule kidogo unawatizama wafugaji wa kuku hususan wanawake, lakini kwa kufuga kuku wa kienyeji hili ni zuri sana. Hapa serikali kidogi imejitahidi sijui hapa Unguja lakini Pemba naona wafugaji wanawake wanajitahidi sana katika kilimo hiki na wako mbele sana, kwa sababu hivi karibuni Mhe. Ali Juma Shamhuna alipeleka watu kutoka katika jimbo lake waende wakajifunze namna gani kule Pemba wanavyoutumia mradi huu, yeye mwenyewe alitoa seti kwamba kweli kule Pemba watu wamefanya vizuri katika mradi huu wa ufugaji kwa kutaka na Unguja nao waige mradi huu wa kilimo unavyowasaidia wakulima hususan wakulima wanawake, kufuga kuku pamoja na kulima kwa kupitia haya haya mbolea ya mavi ya kuku. Lakini ufugaji mwengine wowote hapa haukutiliwa mkazo ni wenyewe wenyewe tu wanajitahidi tahidi.

Mgodi mwengine tuliokuwa nao uvuvi ndio yale yale hayaji mapya nao jamani tumeutupa hatuushughulikii kabisa, pale Mwenyezi Mungu anapotujaalia kuvua samaki wengi basi hatujui hata vile vya kuwafanya, ngona nikwambie mimi nakaa Mkoroshoni Pemba siku linaloanguka dagaa kule sisi tunaita toeya alfajiri kubwa sana saa 12.30 tayari linapita sio kwa masusu tu mpaka kwa magari linakuwa jingi mpaka linamwagwa, mwana yake watu huenea mpaka jengine linamwagwa. Tungelikuwa na uvuvi wa kisasa tukawa na kiwanda basi hili dagaa lisingelipotea lakini leo linapotea kwa sababu tulipeleka wapi hatunapo, hatuna ufugaji wa kisasa kama tutawauzia wale wenye viwanda vya kufuga hatuna. Kwa hivyo utakuta dagaa hili linapotea bure sasa hebu huu uvuvi tuupeni haki yake.

Mhe. Mwenyekiti nikikaa kwangu hapa Mji Mkongwe nikitizama baharini naona vibatari vile vya kuvulia vibua ni kusema kwamba wao wanavua hapa na pale mimi nisingewaona kama wanavua mbali, hawaendi mbali hawa

kwasababu hawana zana za kuvulia kwa hivyo piga ua au garagaza maneno ya vijana hawa wavuvi tuwatizame kwa sababu ndio wengi, wavuzi na wakulima ndio waliopo nchi hii wafanyakazi ni wachache tu. Nasema haraka haraka ili na wenzangu wapate kuchangia.

Lakini jambo jengine tuwekeze kwenye elimu hii elimu tumeipa pesa ndogo, tukiekeza kwenye elimu basi inaweza kutunyanyua kiuwezo hii elimu, kwa sababu ukishamsomesha mtu si lazima umpe pesa wewe umempa elimu atajua nini yeye afanye na kuweza kujitegemea yeye mwenyewe, kwa hivyo tuwekeze kwenye elimu ya kujitegemea. Elimu ya kusoma akajua kufanya hesabu na mambo mengine ni vizuri sana tukapata wataalam wazuri lakini pia tuwekeze ili mtu akitoka pale kwenye ufundi ajue mwenyewe anafanya nini, wengine watakapokuwa wamesoma elimu za juu watatumika katika serikali, wengine katika viwanda lakini waliokuwa hawakupata elimu hizo watazweza kujiendeleza wenyewe.

Kwa hivyo lile tatizo la kutegemea serikali sote ituajiri  na ajira zenyewe hazipo basi litaondoka tuwekeze kwenye elimu, watu wasome sana ili tuweze kupata wataalam wengi sana, tukipata wataalam wengi sana tutaweza kuwatumia ndani na wengine tutauza.

Mhe. Mwenyekiti jambo jengine ambalo sikuliona kwenye bajeti wala kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijapata kufanya, Wazanzibar tunao wengi sana sasa hivi huko nje na wengi wanawaletea wazee wao fedha hapa kwa ajili ya kuendesha maisha, hivi hatujazitia kwenye bajeti vijana hawa wanasaidia uchumi wa Zanzibar kiasi gani nchi nyengine wanazitia kwenye bajeti hizi pesa. Sasa tufanye maarifa kaa tutaweza kuwajua ni wangapi waliopo nje na wanazilete vipi hizi pesa tukaweza kuzijua, kwa nini wengine wabajeti katika nchi zao kwa vijana walioko nje.

Misri wanatia katika bajeti yao ya serikali kwa vijana wao walioko nje tuulize basi wanafanya fanya vipi hawa mpaka vijana wao walioko nje wakawatika katika bajeti ya serikali? Wanachangia kiasi gani uchumi wa nchi yao? Na sisi tuweze kujua hawa vijana ingawa wako nje lakini bado wanaisaidia vipi nchi yao ya Zanzibar japo kwa kuwaletea watu wao fedha ndani kutumia, lakini pia kwa wale waliokwishapata pesa nzuri huko nje tuwashawishi basi waje kuwekeza humu ndani ili nchi yetu iweze kunyanyuka kwa sababu na wao wanakuja na wezee wao wako hapa na wengine watoto wao wako hapa. Kwa hivyo lazima wawekeze ili tuweze kunyanyuka kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti  tuna chuo hapa cha Afya, tunatoa madaktari pale sijui hili ninalolisema kama ndivyo naomba nifafanuliwe, pale Afya najua wanafunzi wanaingia kwa *qualification* zao uwe umepasi sayansi ndio uingie pale, lakini

jambo la kusikitisha inasemekana kuna watu mpaka *Form II* na wengine wale waliopasi hasa wanaachwa nje kwa mujibu wa *qualification* zao hasa basi hawachukuliwi anachukuliwa mtu kafika *Form II* anakuja kusoma nini pale. Na hili najua Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii atakataa lakini lipo na aende akalifanyie utafiti yeye mwenyewe ataliona, tusikatae kila kitu tu lakini mengine tuyafanyie utafiti twende tukaone ukweli.

Zanziba sasa hivi tunasumbuliwa sana na maradhi ya sukari tunaomba utafiti ufanyike ionekane hasa Wazanzibar tunaathiriwa na nini hata watu wengi wakapata maradhi ya sukari.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine sote tutalisema wanawake hili arubaini elfu inatukera kweli kweli. Haitakuwa sisi tunaumwa na uchungu wa kujifungua, roho toka mtoto toka sikuzaa kwa hivi hivi natakiwa kufanyiwa upresheni mpaka nitoe arubaini elfu, jamaa yangu kutoka Matemwe na kutoka Tumbatu na mwengine Ukutini lakini huku Unguja akiwa Pemba halipi sasa hana arubaini elfu tunafanya nini? Hebu tuondosheeni hii huku sisi wanawake ndio tunaochangia uchumi mkubwa katika nchi hii, halafu tukikuzaeni nyie waume zetu, baba zetu na watoto wetu mtutozeshe shilingi arubaini elfu kwa nini hamuwatoleshi walevi huko mnatutolesha sisi tunaozalisha mali za watoto, hebu tuondoshe hii arubaini elfu tuone tutafika wapi. Hatuitaki hii arubaini elfu Mhe. Waziri tunasema hatuitaki eee!.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa nakuomba umalizie.

**Mhe. Najma Khalfan Juma:** Sasa nakuja kwenye viwanda vidogo vidogo lazima tuwe navyo kama vya *juice*, pipi, biskuti na samaki tuwaite watu waje kuwekeza.

Halafu nakuja mikopo kwa wanawake, sikuiona wakati sisi ndio tunaonyanyua uchumi wa nchi, jamani wanawake hebu tukusanyeni pesa zetu nyingi zinatoka nje kama nilivyosema miezi yetu mitatu mnazipeleka nje, lakini Zanzibar kuna washini wazuri tu wa nguo za kitoto wapo. Hebu Wizara ya Fedha na Uchumi ishirikiane na wanawake na watoto pamoja na Wizara ya Biashara watafuteni hawa muwape mikopo hawa wanawake halafu tuone watafanya nini, miezi kama hii wawe wameshashona nguo zao na wameshazitia madukani ziuzwe tutapunguza kupeleka pesa zetu nje.

Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi sana kwamba Uwanja wa Ndege Zanzibar umepanuliwa nafurahi kwamba ndege kubwa zitatua na serikali itaweza kupata mapato, lakini hiki kima cha uwanja wa ndege uliopo sasa hivi urefu wake basi naomba uchukuliwa na ukawekwe kule Pemba, iwe sasa Pemba uwanja wake unafika huu uliopo sasa hivi. Kwa hivyo mimi naiomba Serikali ifanye

ifanyavyo na uwanja wa ndege wa Pemba nao ukapanuliwe ufike kama huu uliopo Unguja hivi sasa tunaotumia, nyie hamuoni tabu siku za sherehe kule kuja na *vichata*. Mnaona tabu ndiyo sasa kama mnaona tabu ule uwanja upanueni halafu muweke taa humu pembeni ili mkija kule Pemba msione tabu kutua wakati wa mvua. Juzi ndege ilitembea nusu saa juu haiwezi kutua kwa sababu ya mvua na hapana taa pale uwanjani ni hasara ile, kwa hivyo hili litizamwe.

Jambo jengine naomba uchumi wa wanawake tunaochangia katika nchi hii upimwe panaletwa uchumi jumla jumla tu hapa sijui tumepata bilioni ngapi, hebu tupimeni sisi wanawake tunaichangia serikali ya nchi hii kiasi gani ya fedha.

Jambo jengine la mwisho leo nimekwenda kwenye Benki ya Watu wa Zanzibar sijapenda kwamba pale pahala pa kuhudumia wateja pana joto utafikiri jiko, sasa pale kutia viyoyozi angalau tukastarehe sisi wateja wako. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Mwenyekiti na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya upendeleo ili nimalizie muda. Mhe. Mwenyekiti tunachokizungumza hapa ni bajeti ya serikali ambayo maana yake ni namna serikali inavyoweza kukusanya mapato kwa mwaka na kwa upande wa pili ni namna serikali inavyoweza kutumia, kwa mujibu wa mipango yake iliyojiwekea. Lakini si hilo tu malengo ya wananchi au matarajio ya wananchi wanayoyategemea kupitia mpango huu wa serikali kwa mwaka.
Mhe. Mwenyekiti bajeti hii tunayoizungumza hapa ni muhimu sana kwa sababu mbeli kama walivyoeleza wenzangu, kwanza ni muhimu kwa kuwa mwaka huu tukijaaliwa ni mwaka wa uchaguzi mkuu ambao tunategemea mwezi wa kumi na moja tutapata serikali mpya, serikali hiyo tukijaaliwa matumizi yake yatatokana na bajeti hii.

Kwa hivyo kama ikiwa tunapitisha bajeti mbovu ni kusema kuwa serikali inayokuja itanza vibaya au kama tunapitisha bajeti nzuri serikali inayokuja itaanza vizuri, lakini vile vile bajeti hii umuhimu wake mkubwa ni kwamba inafunga ukurasa wa awamu ya sita tunakumbuka kwamba Mhe. Amani Abeid Karume anamaliza kipindi chake cha vipindi viwili ambapo awamu ya sita inamaliza muda wake.

Mhe. Mwenyekiti bajeti hii tunasema ina umuhimu na uzito wake sasa kwa hisia zangu na fikra zangu ni kwamba tuna tatizo la msingi, tatizo tulilonalo ni namna ya uwezo wa serikali katika kukusanya haulingani kabisa kabisa na hali halisi ya mahitaji ya kiuchumi kwa watu wetu. Wananchi siku zote huwa wana mategemeo na wanafuatilia mambo haya wananchi wana mategemeo

wanaangalia bajeti hii itakavyowasaidia wafanyakazi katika kupandishwa mishahara, lakini vile vile waliokuwa hawana ajira wanaangalia bajeti hii namna itakavyowasaidia kupata ajira, vipi huduma za afya zitaimarika kupitia bajeti hii. Lakini kama alivyosema mtaalam mmoja jana kwamba uchumi unaokuja hutengenezwa na bajeti iliyopo sasa ili tujenge uchumi kwa miaka iliyopo baadae inategemea ni namna gani bajeti tuliyonayo inaweka misingi katika kujenga uchumi unaokuja.

Sasa nasema hayo ndio matarajio na malengo ya bajeti tatizo tulilonalo ni kwamba tutaona kwamba uwezo na nguvu ya ukushanyaji hailingani na matarajio ama malengo waliyojiwekea wananchi katika uchumi. Sasa tufanye nini mimi nafikiria au wazo zuri tuseme sasa tukaeni tayari kama wawakilishi na serikali ikae tayari ili tuanze kujenga uchumi, uchumi tutaujenga vipi kwa sababu tutakubaliana kwamba hali ya uchumi kadiri kila aliyezungumza hapa tunakubaliana kwamba hali haiendi vizuri na mambo hayaendi vizuri, lazima tufike pahala tuseme sasa tufanye nini?

Mhe. Mwenyekiti misingi mikubwa ya kujenga uchumi kwa sasa ni utulivu wa kisiasa taifa lolote yale yaliyoendelea na yale ambayo yanaelekea kuendelea Mhe. Mwenyekiti, msingi mkuba au mhimili mkubwa wa kujenga uchumi ni utulivu wa kisiasa hatuwezi kujenga uchumi kama nchi ya Somalia. Kenya ilivyokuwa karibuni huwezi kujenga uchumi Zanzibar ilivyokuwa na tulivyokuwa katika miaka ya karibuni hatuwezi kujenga uchumi, Wazimbabwe hawawezi kujenga uchumi kwa walivyokuwa.

Sasa utulivu huu wa kisiasa aliotuletea Dk. Amani Abeid Karume pamoja na Maalim Seif ndio nyenzo kubwa sana ya kujenga uchumi, tutakapokuwa na utulivu wa kisiasa wa kikweli kweli Mwenyekiti tukakaa pamoja Wazanzibar wote kwa pamoja tukasahau itikadi ya vyama vyetu, tukasahau upande wa visiwa vya Unguja na Pemba huyu anatoka wapi na huyu anatoka wapi? Tukasahau mambo ya makabila hapa tutajenga uchumi na kipindi kifupi tukijaaliwa Zanzibar itaonyesha mfano katika bara letu la Afrika.

Mhe. Mwenyekiti hivyo basi tutakuwa na kura ya maoni tarehe 31/7/2010 nawaomba Wazanzibar wenzangu wote wawakilishi, wabunge na kila mtu na kila mdau tuhakikishe kwamba tunaifanyia haki kura hiyo ili tupate utulivu wa kweli ambao ndio nguzo kubwa sana ya kujenga uchumi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kitu chengine ambacho kinaweza kujenga uchumi wetu ni kero zilizomo katika Muungano hapa naeleza kwa urefu kabisa kwamba hata tukijitahidi vipi, kama kutakuwa na baadhi ya mambo hayajatatuliwa na wenzetu basi ni sawa na kamba ya kufungwa kiuno, kadri tunavyotaka kuendelea mbele kujenga uchumi wetu kama kero hizo hazijaondolewa itakuwa

ni sawa na kutwanga maji kwenye kinu hapo tunaweza kuanzia. Hili linatushangaza sana kwa nini kama ikiwa makero haya tumeshayaona kwa nini tusikubaliane kuyaondosha kuna tatizo gani, tuliungana kwa hiyari yetu na bado tunaupenda muungano na tutaupenda zaidi muungano lakini kama ikiwa kuna mambo tunahisi yanazuia maendeleo kwa upande mmoja kwa nini yasiondoshwe, au kwa nini wenzetu wawe katika kwenda kwao wawe wanagisa gisa tu kuna kitu gani?

Mhe. Mwenyekiti hizi ni nchi mbili kama walivyosema wanzangu keshokutwa tutakuwa na nchi tano katika muungano huu, lakini ikiwa tunashindwa kutatua matatizo yetu ndani ya nchi mbili ndugu wa damu je tutaweza kutatua kero hizi kwa nchi nyengine ambazo hata Kiswahili hawajui. Leo wote tunazungumza Kiswahili chama kinachotawala ni kimoja tu CCM tunashindwa kutatuta kero zetu, kesho na keshokutwa kuna vyama vyengine serikali zinaongozwa na RPF vyama vinatawaliwa na *FORD* kuna tofauti tofauti, lugha tafauti, imani tafauti kweli katika kipindi hicho tutakujaweza kuondosha kero zetu wakati leo ndugu baba mmoja mama mmoja hatukubaliani.

Kwa hivyo hapa ndio pa kuanzia tunawaomba wote wanaohusika kwa haraka inavyowezekana wakae na kila ambalo linaonekana hili ni tatizo kwa hapa Zanzibar ambalo linatokana na upande wa pili Mwenyekiti tumalizeni awamu hii lakini tuanzeni awamu mpya kwa kuondosha kero, hilo linawezekana kabisa kabisa kama kutakuwa na nia njema miongoni mwetu

Mhe. Mwenyekiti, la tatu nyenzo na nguzo kubwa ya uchumi ni kuwa na matumizi sahihi ya rasilimali zetu. Pamoja na umasikini unaoiona Zanzibar pamoja na udogo wetu lakini Zanzibar tuna rasilimali za kutosha kabisa kama iwapo tutazitumia vizuri, basi uchumi wetu unaweza ukawa wa mfano katika Bara la Afrika na Katika dunia ya tatu.

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya rasilimali kubwa ambayo kuwa tunaweza tukaitumia ni rasilimali watu. Iwapo tutawekeza katika watu wetu tulionao. Wazanzibari inasadikiwa sijui kwa sababu watu wanaishi katika visiwa lakini wana akili sana. Kama iwapo tutawekeza katika elimu basi sisi kazi yetu inatosha kuzalisha wataalamu na tukauza tu nje ya nchi na tukapata tija kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la elimu juzi tukiwa pamoja na wewe tulikwenda Malaysia, wenzetu wameendelea sana ambao hao tulikuwa pamoja katika uchumi wetu tulikuwa tukifuatana katika miaka ya 60. Lakini tukajiuliza siri yao ni nini, wakatwambia siri ya maendeleo yao ni elimu na kweli. Tulipata taarifa pale wana Vyuo Vikuu visivyopungua mia sita (600). Wenzetu wamewekeza sana katika elimu na sisi kama tunataka tuendelee ni lazima

tuekeze sana katika elimu na hususan elimu ya sayansi kwa sababu ndio dunia ya sasa ilivyo.

Kwa hivyo Dokta Mwinyi hilo lichukue na serikali hilo ilichukue kwamba ni lazima tuekeze katika elimu, tusifanye mchezo hilo halina mjadala wala halina mbadala. Ikiwa *serious on that* kwa kweli lazima tuelekee huko, lakini rasilimali yetu tuliyonayo nyengine ni bahari. Wenzangu kama walivyosikitika na mimi nasikitika. Juzi ilikamatwa meli ya Magufuli masamaki wengi sana, meli moja mahesabu yake sijui ni mangapi. Hivyo sisi bahari inayotuzunguka kwa nini serikali haijatuelekeza huko, kuna kitu gani kinachokwaza kutokuitumia bahari na kutokuingiza katika mipango yetu ya kujenga uchumi.

Mwanza wanasafirisha tani nyingi sana na wanaingiza fedha nyingi sana kwa samaki tu wale wa sangara na samaki wale wengine. Leo sisi hapa tuna samaki ambao wanasoko sana katika dunia. Mwenyekiti Mwalimu alisema Uchumi tunao na tumeukalia. Bahari ni lazima tuambiwe serikali ina mpango gani na ina malengo gani katika matumizi ya rasilimali yetu ya bahari.

Mafuta halikadhalika hatujaambiwa chochote, wenzangu wamezungumza na mimi naomba nisisitize kwamba ni rasilimali kubwa sana ambayo kama tutaitumia vyema Zanzibar hatutohitaji chengine isipokuwa mafuta tu yatatuendesha.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kilimo hatuwezi kukiacha kwa sababu kama tutakwenda vizuri katika kilimo mambo haya ya kuagiza chakula au mazao yatatupungukia tukipunguza kuagiza chakula nje hiyo itakuwa ni faida moja ya kiuchumi kwa watu wetu, fedha nyingi inatumika katika uagiziaji. Inawezekana kwamba mwananchi wa kawaida katika nusu ya mwaka au robo ya mwaka akaweza kutumia anachokizalisha katika shamba. Hiyo itatupa faida kubwa sana, lakini leo hata ukimkuta mkulima gani hana uwezo wa kutumia hata mwezi mmoja kitu anachozalisha katika shamba lake. Sehemu kubwa tunatumia katika kuagiza. Hilo linaleta dosari kubwa katika uchumi wetu. Tutakapoendeleza kilimo ikiwa pamoja na karafuu, suala la uzalishaji litakuwepo. Moja katika kasoro tuliyonayo ni kwamba hatuzalishi. Hili baadaye tutakuja kuona namna gani *Protocol* ya Afrika Mashariki hii inayokuja tarehe 1 Julai, inatwambia kwamba ikifika wakati huo uingizaji wa bidhaa katika nchi yetu ya Zanzibar itakuwa hakuna kodi. Sasa ikiwa hakuna kodi na kwa sababu sisi tegemeo letu leo ni kutegemea kodi katika uchumi hiyo itakuja kutuathiri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tufike pahala suala hili tuwe makini nalo. Suala la viwanda kwa Zanzibar lina historia ndefu, katika miaka ya 70 tunakumbuka vizuri, Zanzibar ilikuwa ikisafirisha nje takriban vitu vingi sana

kupitia viwanda vidogo vidogo, mambo ya nyaya za umeme, mambo ya viatu, sigara, sabuni. Moja katika ahadi waliochukua CCM wakati pale tunavunja Afro Shirazi Mama, CCM walisema watarithi mema yote yaliyotokana na Afro Shirazi Party na moja ambalo ni kubwa sana walilotuachia wenzetu ni viwanda, ahadi hiyo kwa kweli haikuweza kutekelezwa. Mimi bado nalilia ahadi ile iliyochukuliwa na CCM kwa Chama chetu cha Afroshirizi kati ya mema ambayo hatukuweza kuyaendeleza moja la viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba tuipitishe bajeti na *Ishallah* Dokta Mwinyi bajeti tutaipitisha kwa kishindo hilo usiwe na wasi wasi nalo na pia tukijaaliwa Mwezi wa 7 tarehe 31 tutakwenda kwenye kura ya maoni na *Ishallah* Wazanzibari watasema *Yes*. Tukitoka hapo tukijaaliwa mwezi wa 10 tutakwenda kwenye uchaguzi na baada ya ya uchaguzi Mwenyezi Mungu atatujaalia tutakuwa na serikali ya pamoja, serikali ya Wazanzibari, serikali yenye neema.

Mhe. Mwenyekiti, mategemeo yetu ni kwamba katika kipindi hicho haya yote tunayoyazungumza leo ambayo sidhani kama yatakuwa na jawabu, jawabu haitokuwa nzuri. Kipindi hicho tuje tukae tujenge uchumi wetu. Linawezekana kabisa kujenga uchumi ndani ya kipindi kifupi na tukawa ni mfano. Mawaziri watakaokuja kuchaguliwa kipindi hicho kama ni akina mama rangi za midomo hatuzitaki kipindi hicho kwa sababu wengine tutakuwepo tukijaaliwa Mwenyezi Mungu atatujaalia tuwemo. Tunataka watu wa kazi, hatutaki mambo ya hadithi hadithi. Waziri unatufanyia hivi na hivi unakuja na hadithi zile zile za mvinyo mpya katika chupa mpya. Mhe. Waziri tupishe, tunataka sasa tujenge uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hakushukuru sana, ahsante.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Omar Ali Shehe, kweli tulikwenda Malaysia, kweli tumeona hatua walizopiga wenzetu lakini hili kwa wanawake kutokutia rangi za midomo hiyo si hoja, hoja utendaji.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Mwenyekiti, naomba radhi. (*Vicheko*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa wajumbe kwa kuwa muda uliobaki hatuwezi kumsikia Mheshimiwa akichangia kwa hiyo kesho asubuhi tutaendelea na tutaanza na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji. Sasa naomba kuahirisha kikao hichi kwa siku hii ya leo mpaka hapo kesho tarehe 16/6/2010 siku ya Jumatano saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 1.40 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 16/6/2010 saa 3:00 asubuhi)*